# MAENDELEO YA KISWAHILI

## ASILI YA LUGHA YA KISWAHILI

Neno asili lina maana kuwa jinsi kitu au jambo lilivyotokea au lilivyoanza na tunapozungumzia asili ya lugha ya Kiswahili ina maanisha tunachunguza namna lugha hiyo ilivyoanza. Wataalamu mbalimbali wa lugha wamefanya uchunguzi juu ya asili ya lugha ya Kiswahili.

Uchunguzi huo umejenga nadharia mbalimbali zinazoelezea chimbuko la lugha ya Kiswahili.

Kwa ujumla historia kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili ina matatizo mengi na ndiyo maana kuna nadharia mbalimbali zinazoelezea juu ya asili ya lugha ya Kiswahili.

Miongoni mwa matatizo yanayoikabili historia ya Kiswahili ni pamoja na:

1. Hakuna uthibitisho kamili juu ya nadharia zinaelezea asili ya lugha ya Kiswahili na kuenea kwake.
2. Uchunguzi wa asili ya Kiswahili ulifanywa na wataalamu wa kizungu ambao waliandika historia ya Kiswahili jinsi walivyoelewa wao baada ya kupata ushahidi kidogo tu.
3. Wazawa hawakushirikishwa ipasavyo katika uchunguzi wa lugha ya Kiswahili.
4. Hapakuwa na kumbukumbu za kutosha kwa sababu babu zetu hawakujua kusoma wala kuandika hivyo basi kuna upungufu wa kumbukumbu.

Kutokana na matatizo hayo yanayoikabili historia ya Kiswahili kuna nadharia mbalimbali zinazoelezea historia ya lugha ya Kiswahili. Nadharia hizo ni kama vile:-

(i) Kiswahili asili yake Kongo

(ii) Kiswahili ni kundi au pijini

(iii) Kiswahili ni lugha ya vizalia

(iv) Kiswahili ni Kiarabu

(v) Kiswahili ni Kibantu.

1. **<u>KISWAHILI ASILI YAKE NI KONGO</u>**

Baadhi ya wataalamu hudai kuwa asili yake ni Kongo (Zaire). Madai haya yanaimarishwa zaidi na wazo jingine linalodai kwamba katika vipindi lengwa vilivyopata kuwepo sehemu za Pwani ya Afrika Mashariki hazikuwa zimekaliwa na watu. Lakini kutokana na hali ya uzito, ufugaji, na biashara inadaiwa kuwa wabantu walisambaa Afrika Mashariki kupitia Kigoma na baadhi ya sehemu za Uganda. Wakati wa kusambaa kwao walieneza pia lugha zao kikiwemo Kiswahili.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**UDHAIFU**

Madai kuwa asili ya Kiswahili ni Kongo hayana msingi kwa sababu mpaka sasa wataalamu wa nadharia hiyo hawajaweza kueleza na kuthibitisha kisayansi ama kihistoria juu ya lini hasa watu walianza kuishi Pwani ya Afrika Mashariki.

## II. KISWAHILI NI KRIOLI AU PIJINI

Baadhi ya wataalamu hudai kuwa asili ya Kiswahili ni tokeo la mwingilio baina ya wenyeji wa Pwani ya Afrika Mashariki na wageni wa kiarabu. Wataalamu hawa hudai kuwa Kiswahili ni lugha ya kati iliyozuka ili kurahisisha au kufanikisha mawasiliano katika shughuli ya biashara ya mwanzo. Wataalamu hawa husisitiza kuwa lugha ya Kiswahili haikuwepo kabisa kabla ya hapo. Wanaona lugha ya Kiswahili ilianza kama pijini na baadaye kukua na kuwa kama Krioli kutokana na lugha hiyo kuwa lugha ya mwanzo kwa wazungumzaji.

**Pijini ni nini?**

Ni lugha ambayo huzuka kutokana na kuwepo pamoja kwa makundi mawili yanayotumia lugha mbili tofauti. Ili makundi hayo yaweze kuwasiliana, huundwa lugha ambayo kitabia ni tofauti na zile zinazozungumzwa na makundi yanayohusika. Lugha hii inaweza kuwa na msamiati kutoka katika lugha moja kati ya hizo mbili, au inaweza ikawa na msamiati wenye uzito sawa. Lugha hii ndiyo huitwa Pijini. Pijini huzuka kutokana na vitu kama vile biashara, utumwa, ukoloni, n.k

**Krioli ni nini?**

Kwa kawaida watu wanaozungumza lugha ya pijini wanaweza kuzoeana na kuishi kwa pamoja hata kuoana. Watoto watakaozaliwa hutumia lugha ya pijini kama lugha yao ya kwanza. Lugha hii inayotumiwa na watoto hawa watakaozaliwa huitwa krioli. **Krioli ni pijini iliyokomaa.**

Wataalamu wa nadharia hii hutumia kigezo cha msamiati uliopo katika lugha ya Kiswahili ambao kwa kiasi kikubwa unatoka katika lugha ya Kiarabu. Ni kweli kuwa lugha hii inamchango mkubwa wa msamiati katika lugha ya Kiswahili.

**UDHAIFU**

Hutumia kigezo kimoja cha msamiati peke yake kama kigezo pekee ni udhaifu kwa kuwa lugha inaweza kutazamana kwa kutumia vigezo vingine, matamshi, maumbo ya maneno au miundo ya sentensi. Ukitumia vigezo mbalimbali vya uchambuzi wa lugha, lugha ya Kiswahili ina mfanano zaidi na lugha za kibantu kuliko madai yaliyotolewa na nadharia hii.

## III. KISWAHILI NI KIARABU

Kuna madai kwamba lugha ya Kiswahili asili yake ni Kiarabu. Wataalamu wa nadharia hii hutetea madai yao kwa hoja kuu tatu:-

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. Idadi kubwa ya maneno yaliyomo katika Kiswahili takribani 30% ni maneno yenye asili ya Kiarabu. Hivyo basi ni uthibitisho tosha kwamba Kiswahili kilianza kama pijini ya Kiarabu.
2. Neno lenyewe, Kiswahili; ambalo asili yake ni Kiarabu. Neno Kiswahili limetokana na neno ***'sahil'*** ambalo ni neno la Kiarabu lenye maana ya ***'Pwani***' na neon ***'Swahili***' hutumika likiwa na maana ya 'Pwani". Kwa hiyo neno, 'waswahili' lina maana 'watu wa pwani'.
3. Dini / Biashara / Mila na desturi. Inadaiwa kwamba kwa kuwa Kiswahili kilianzia Pwani na kuwa kuna idadi kubwa ya wenyeji wa Pwani ni waislamu kwa imani zao, na kwa kuwa uislamu uliletwa na waarabu, basi hata Kiswahili nacho kililetwa na waarabu.

## UDHAIFU

1. Kutumia kigezo cha msamiati ni udhaifu kwa sababu kila lugha huchukua msamiati kutoka lugha nyingine. Kiswahili hakikuchukua msamiati kutoka Kiarabu pekee pia lugha nyingine kama: Kiajemi, Kireno, Kihindi, Kijerumani na Kiingereza.
2. Lugha huchukua msamiati mwingi kutoka lugha fulani si kigezo cha kuhalalisha kuwa lugha fulani ina asili fulani mfano: Kiingereza huchukua maneno kutoka lugha ya Kifaransa, haiwezekani kuhitimisha kuwa Kiingereza ni Kifaransa.
3. Pia kutumia kigezo cha dini ni udhaifu. Kwa mfano hatuwezi kusema Kiingereza ni Ukristo kwa kuwa Waingereza ni Wakristo kwa imani yao. Pia nchi kama Senegal ambayo ina Waislamu wengi lugha ya Kiswahili haizungumzwi huko. Ni wazi kuwa Uislamu ungekuwa unafungamana na Kiswahili, kingezungumzwa kila sehemu ambapo Uislamu umeenea.

## IV. KISWAHILI NI KIBANTU

Nadharia hii hutumia ushahidi wa kiisimu na kihistoria kuchunguza lugha ya Kiswahili katika mfumo mzima wa kihistoria wa mgawanyiko na usambaaji wa lugha za kibantu . Nadharia hii inaungwa mkono na wataalamu kama ***Malcom Guthrie***, ***C. Meinhoff*** na ***C. Rohl***. Wataalamu hawa huhitimisha kuwa Kiswahili ni mojawapo ya lugha ya jamii kubwa ya lugha za kibantu. Nadharia hii ndiyo inaelekea kukubalika- kwa wengi kuwa ndiyo sahihi katika kuelewa asili ya Kiswahili. Kwa sababu nadharia hii imethibitishwa kwa hoja za **kiisimu** na hoja za **kihistoria**.

## A. USHAHIDI WA KIISIMU

Ushahidi wa kiisimu ni ushahidi unaothibitishwa kwa misingi ya sayansi ya lugha. Isimu huchunguza lugha kwa undani kwa kutumia tanzu zake. Baada ya kufanyiwa utafiti wa kina na wataalamu mbalimbali, ilithibitika kuwa asili ya Kiswahili ni kibantu kutokana na vigezo vifuatavyo**:-**

- **Utafiti wa Malcom Guthrie**

Ni mtaalamu wa isimu kutoka chuo kikuu cha London, aliyefanya utafiti wa kutafuta uhusiano kati ya lugha ya Kiswahili na lugha za kibantu kwa miaka 20 katika nchi za Kiafrika zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo zinasadikika kuwa ndipo wabantu wanapoishi.

Katika utafiti wake alichunguza mizizi ya maneno 22,000 kutoka lugha za Kibantu ikiwemo lugha ya Kiswahili

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Katika utafiti wake aligundua mambo yafuatayo:-**

(a) Mizizi ***2,300*** ilizagaa katika lugha mbalimbali za kibantu ikiwemo lugha ya Kiswahili.

(b) Mizizi 500 iliungana katika lugha zote 200 alizozifanyia utafiti.

(c) Alipolinganisha lugha hizo na lugha ya Kiswahili, zilionesha ulinganifu kama ifuatavyo:-

- Kiwemba (Zambia) kililingana na Kiswahili kwa 54%.

- Kiluba (Katanga) kililingana na Kiswahili kwa 51%

- Kikongo (DRC) kililingana na Kiswahili kwa 44%

- Kiswahili cha (A. Mashariki) 44%

- Kisukuma (Tanzania) 41%

- Kiyao (Tanzania, Msumbiji) 35%.

- Kirundi (Burundi) 43%

- Kisotha (Botswana) 20%

Mtaalamu huyu pia aligundua kadri unavyoshuka Kaskazini ya Katanga ndiyo msamiati unavyoachana zaidi,

- **Mfanano wa msamiati**

Ushahidi huu ulitokana na utafiti wa ***Prof. Maganga*** ambaye alibaini kuwa ***60%*** ya maneno ya Kiswahili yenye kuandikika na kutamkika, yana asili ya Kibantu. 30% ya msamiati wa lugha ya Kiswahili unatoka katika Kiarabu na ***10%*** inatoka katika lugha nyingine mfano: Kireno, Kiingereza.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Ni wazi kuwa msamiati wa Kiswahili na Kibantu hautofautiani sana, hasa katika matamshi:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | → | Maji | mtu |
| Kindali | → | amashi | umundu |
| Kizigua | → | manzi | mntu |
| Kijita | → | amanji | omanu |
| Kipare | → | mbombe | mndu |
| Kichaga | → | mringa | mndu |
| Kinyakyusa | → | amesi | mundu |
| Kihangaza | → | amazi | |
| Kipogoro | → | maishi | |

- **Miundo ya tungo:-**

Miundo ya tungo za maneno ya Kiswahili inafanana na miundo ya tungo za maneno ya Kibantu. ***Mfano***: miundo ya sentensi za Kiswahili huwa na muundo wa Kiima na kuarifu hali kadhalika miundo ya sentensi za Kibantu huwa na muundo huo huo.

***Mfano:-***

- Mama / anakunywa maji (Kiswahili)

  K A

- Mayo / aling'wa minze (Kisukuma)

  K A

- Jubha / ikonwa amesi (Kinyakyusa)

  K A

- Yubha / inywa lulenga (Kihehe)

  K A

- Mawe / ang'wa mazi (Kiha)

  K A

***NB:*** Pia miundo ya sentensi za Kiswahili hubadilika katika maumbo ya umoja na wingi.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Pia maumbo ya kibantu hubadilika katika maumbo ya umoja na wingi.

***Mfano:*** Watoto / wanakunywa maji (Kiswahili)

- Mwana / ikonwa amesi (Kinyakyusa)

K A

- Mwana / avana vinywa lulenga (Kihehe)

K A

- Bhana bhaling'wa minze (Kisukuma)-umoja

K A

- Bhana / bhaleng'wa minze (Kisukuma)-wingi

K A

- **Ngeli za majina**

Makundi ya majina mbalimbali katika lugha ya Kiswahili huwa na makubaliano kwa kufuata maumbo ya umoja na wingi pamoja na upatanisho wa kisarufi.

Tabia hizi za majina ya Kiswahili hujitokeza pia katika majina ya Kibantu;

(a) **Kwa kutumia maumbo ya majina.**

Majina mengi ya Kiswahili huwa na maumbo ya umoja na wingi, halikadhalika kwa majina mengi ya Kibantu.

| | | |
|---|---|---|
| ***Mfano:*** Kiswahili | m-toto | wa-toto |
| Kisukuma | ng'-ana | bh-ana |
| Kinyakyusa | mw-ana | b-ana |
| Kihehe | mw –ana | v-ana |
| Kiswahili | ki –ti | vi – ti |

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

| | | |
|---|---|---|
| Kinyakyusa | ki-goda | vi-goda |
| Kihehe | ki-kota | vi-kota |

(b) **Kigezo cha upatanisho wa kisarufi.**

Kwa kutumia kigezo hiki, nomino za Kiswahili na za kibantu hufuata upatanisho wa kisarufi kwa kupachika viambishi pia. Viambishi hivyo hubadilika kutokana na mabadiliko ya maumbo ya umoja na wingi.

***Mfano:*** Mtoto mzuri anakunywa maji

Watoto wazuri wanakunywa maji

Mwana mnunu ikonwa amesi

Bana banunu b**i**konwa amesi

Mwana mnofu inywa lulenga-umoja

Vana vanofu vinywa lulenga-wingi

- **Vitenzi vya Kiswahili na vya Kibantu**

Tabia ya vitenzi hivi hufanana. Mfanano huo hujitokeza katika vipengele vifuatavyo:-

(a) **Viambishi**

Lugha ya Kiswahili na kibantu, vitenzi vyake huwa na mzizi pamoja na viambishi awali na tamati.

| | | |
|---|---|---|
| ***Mfano:*** | Kiswahili | a – na - lim – a |
| | Kindali | a – ku – lim – a |
| | Kikurya | a – ra – rem – a |

1 - viambishi vya nafsi

2 - Viambishi vya wakati

3 - mzizi

4 - Viambishi tamati maana.

(b) **Vitenzi vya lugha ya Kiswahili na Kibantu vina tabia ya kunyumbuka**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kiswahili | Kucheka | kuchekesha | Kuchekelea | kuchekwa |
| Kinyamwezi | Kuseka | kusekesha | kusekelela | Kusekwa |
| Kindali | Kuseka | Kusekesha | kusekelela | kusekwa |
| Kipogoro | Kuseka | kusekesa | kusekelela | Kusekwa |
| Kibena | Kuheka | kuhekesha | kuhekelela | kuhekwa |

(c) **Mwanzo wa vitenzi**

Vitenzi vya Kiswahili na Kibantu huanza na viambishi vya nafsi mwanzoni.

***Mfano:*** Ni – nakwenda

- ni - sumwike

- ni – ngenda

(d) **Mwisho wa vitenzi**

Vitenzi vingi vya lugha ya Kiswahili na vile vya kibantu, huishia na irabu ('a') mwishoni.

***Mfano:-***

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kukimbia – a | Kuwind- a | Kushuk – a | kiswahili |
| Kupil-a | Kuhwim –a | Kutend – a | kisukuma |
| Kukimbil -a | Kufwin- a | Kuwik -a | kihehe |

B. **USHAHIDI WA KIHISTORIA**

Licha ya ushahidi wa kiisimu, pia kuna ushahidi wa kihistoria unathibitisha kuwa Kiswahili ni Kibantu.

Ushahidi huo unathibitishwa na wageni mbalimbali waliofika Afrika Mashariki na kudhihirisha kuwa Kiswahili kilizungumzwa Pwani ya Afrika Mashariki kabla ya ujio wa wageni.

Ushahidi huu ulitolewa na wageni mbalimbali waliofika Afrika ya Mashariki na kuthibitisha kuwa kabla ya kufika kwao, Kiswahili kilizungumzwa.Wageni hao ni kama wafuatao:-

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- **Ushahidi wa Marco Pollo**

Ni mwanataaluma wa Kizungu aliyejishughulisha na masuala mbalimbali ya Kijiogragia na kusafiri sehemu nyingine duniani.

Katika moja ya maandiko yake, anasema hivi; "Zanzibar ni kisiwa kilicho kizuri ambacho kinamzunguko wa maili 200" Watu wake wanaabudu Mungu. Wana mfalme na wanatumia lugha yao na hawalipi ushuru kwa mtu

Nukuu hii imenukuliwa kutoka kitabu cha "***SAFARI ZA MARCO POLLO***" ***(1958 – 301)***. [Penguin Books]

Pia katika kitabu chake cha Kijiografia ambacho hakikuchapishwa lakini kimetafsiriwa kwa Kirusi na Kifaransa lakini kina maneno kama vile; Ungudya ambako sasa ni Unguja. Zanguaba ambako sasa ni Zanzibar. Maneno mengine ni kama; kundi, firi, Omani, Murijani, na kisuka. Haya ni majina ya aina mbalimbali za ndizi zilizopatikana Zanzibar.

- **Ushahidi wa Al – Masoud (915 BK)**

Katika moja ya maandishi yake anazungumzia juu ya wakazi wa mwambao ambao walijulikana kwa jina la Waenji. Kwa dhana hii neno Zanzibar linatokana na neno Zanjibar, yaani pwani ya Zanji.

Al – Masoud anaonesha kwamba, Wazanji walikuwa na watawala kwa nguvu za Mungu. Viongozi hawa walikuwa wacha Mungu, Huenda neno Wakitumia / ina maana ya wafalme. Anasisitiza kuwa walisema lugha fasaha na walikuwa na viongozi walio hutubia kwa lugha yao. Kutokana na neno Zanji inawezekana kabla ya kuja kwa waarabu, Kiswahili kilikuwa Kizaramo au Kizanji.

- **Historia ya Kilwa**

Kimsingi habari hizi zinaeleza historia ya Kilwa, karne ya 10 mpaka 16 BK na zinahusiana na kutaja majina ya utani kama vile Mkoma watu, Nguo nyingi n.k Ambayo walipewa Masultan wa kwanza wa Kilwa ambao ni Ali Ilbin Hussein na mwanawe. Mohamed Ibin Ali kutokana na habari hizi huenda lugha ya Kiswahili ilianza kuzungumzwa kuanzia karne ya 10 au 11.

Maelezo ya kihistoria yanaeleza juu ya Sultani aliyeitwa Talt Ibin Al – Hussein aliyepewa jina la utani Hasha haefiki

- **Ushahidi wa Ibin Batuta (14 BK)**

Mohamed Bin Abdallah Ibin Batuta ana asili ya kiarabu alifika Afrika Mashariki kunako mwaka 1331 BK, Katika maandishi yake anaeleza maisha ya watu wa nchi ya Afrika Mashariki ingawa yeye aliita nchi ya Waswahili. Anataja miji kama vile Mogadishu, na Kilwa. Alisema, "Basi nilianza kusafiri baharini kutoka Mogadisho kwenda nchi ya Waswahili na Kilwa ambao umo

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

katika nchi ya Zanji. Tulifika Mombasa kisiwa kikubwa, mwendo wa siku mbili kutoka nchi ya waswahili, Watu hawajishughulishi na kilimo ingawa huagiza nafaka toka kwa waswahili."

- **Maandishi ya Morrice**

Maandishi haya yalijitokeza mwaka ***1779,*** Katika maandishi hayo Morrice anawagawa watu wa Afrika Mashariki katika makundi matatu, ambayo ni waarabu, wasuriana na waafrika. Anasisitiza kuwa masuriana na waafrika walishakaa na kuwa kundi moja. Wakaelewana na kusema lugha moja ya kisuriana. Kuna kuwa huenda kisuriana ndicho Kiswahili cha leo.

- **Ugunduzi wa Ali Idris**

Ugunduzi huu ulifanywa huko Sicily mwaka 1100 mpaka 1166 BK kwenye mahakana ya mfalme Roger II, Katika ugunduzi huu ilisadikika Kiswahili kiliandikwa kabla ya karne ya 10 BK. Al Idrisi alikuwa wa kwanza kugundua jina la zamani la Zanzibar kuwa ni Ungudya. Katika maelezo yake anaandika pia majina ya aina za ndizi mbalimbali zilizopatikana huko Ungudya kama vile kikombe, mkono wa tembo, sukari, na muriani.

- **Vitabu vya Periplus na Yu – Yanga Tsa - Tsu:-**

- **Kitabu cha Periplus**

Hiki kinahusu mwongozo wa bahari ya Hindi na inasadikika kuwa kiliandikwa karne I katika mji wa Alexander. Kitabu hiki kinataja habari za Azania yaani Afrika Mashariki na habari za vyombo vya baharini kama vile ngalawa, madema na mitepe. Kitabu hiki kinaeleza kuwa watu wageni hutozwa ushuru na wafanyabiashara wenyeji na wanaijua pia lugha ya wenyeji vizuri.

- **Kitabu cha Yu- Yanga Tsa - Tsu**

Kitabu hiki kinaeleza habari za upwa wa Afrika Mashariki na shughuli mbalimbali za Wachina hapa Afrika mashariki.

- **Chu – Fan – Chi**

Kilichapishwa 1226 na kinaeleza bahari za Zanzibar na shughuli mbalimbali za Wachina hapa Afrika Mashariki.

- **Ushairi wa Kiswahili.**

- **Utenzi wa Fumo Lyongo**

Hili ndilo shairi la zamani kabisa. Lilipata kuandikwa katika lugha ya Kiswahili na inasemekana liliandikwa karne ya 13 BK. Uwepo wa shairi hili unadhihirisha kuwepo kwa Kiswahili kabla ya hapo. Huenda kilitumika kabla ya karne ya 10 BK.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**LUGHA MAMA (LUGHA YA KWANZA), LUGHA YAPILI NA LUGHA RASMI**

**Lugha rasmi ni ipi?**

Ni lugha inayoteuliwa na serikali ili itumike katika shughuli za kiserikali. Kiswahili Tanzania ni lugha ya taifa pia ni lugha rasmi.

**Sifa za lugha rasmi:-**

(i) Yaweza kuwa lugha sanifu au isiwe sanifu lakini pia yaweza kuwa fasaha au isiwe fasaha.

(ii) Inaweza ikawa lugha ya taifa au isiwe lugha ya taifa.

(iii) Huwa haifuati kabila wala mchanganyiko wa makabila yaliyopo nchini.

(iv) Yaweza kuwa lugha ya kigeni kama vile kiingereza, Kifaransa, Kichina.

(v). Hutegemea utawala uliopo madakarani.

**Lugha mama (Lugha ya kwanza):-**

Ni lugha ambayo mtu hujifunza utotoni baada tu ya kuzaliwa, kabla ya kujifunza lugha ya pili. Mtoto hujifunza lugha hii kwa kusikiliza kutoka kwa wazazi au majirani. Lugha hii ni rahisi kujifunza kulingana na ya pili kwa sababu zifuatazo:

(i) Mtoto huwa na muda mrefu wa kujifunza (usio koma)

(ii) Mtoto hujifunza lugha katika mazingira halisi, mfano vile anavyojifunza vipo pale pale.

(iii) Uhusiano wa mtoto na wanaomzunguka kuwa mzuri.

(iv) Kuna kuwa na msaada wa kutosha katika kujifunza.

(v) Kuna kuwa na uzoefu katika lugha hiyo hiyo moja.

**Dhima ya lugha ya kwanza:-**

Kukidhi haja ya mawasiliano kwa watu wanaomzunguka mtoto.

***NB:*** Lugha ya kwanza inaweza kuwa lugha ya pili kwa watu wengine na lugha ya pili

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

inaweza kuwa ya kwanza kwa watu wengine. Mfano: Kiswahili ni lugha ya kwanza kwa Watanzania wote waliozaliwa mjini lakini yaweza kuwa lugha ya pili kwa Watanzania waliozaliwa vijijini.

**Lugha ya pili:-**

Lugha ya pili ni lugha ambayo mwanadamu hujifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza. Mara nyingi lugha ya pili huwa na athari ya lugha ya kwanza kuhusishwa na mazingira ya lugha ya pili. Kwa Watanzania walio wengi hasa waliozaliwa kijijini Kiswahili ni lugha yao ya pili.

**Matumizi ya lugha ya pili:-**

1. Kutaka kukidhi haja ya mawasiliano kwa jamii ambazo si wazungumzaji wa lugha ya kwanza.


2. Kutaka kujihusisha na jamii inayozungumza lugha hiyo ya pili.

***Mfano:*** tunajifunza Kiingereza ili kujihusisha na jamii nyingine.

**<u>ii CHIMBUKO LA KISWAHILI</u>**

Nadharia hii inazungumzia kuhusu mahali hasa ambapo lugha ya Kiswahili ilichipukia. Wataalam wa lugha ya Kiswahili wanatofautiana kuelezea mahali hasa ambapo ndiyo chimbuko la lugha ya Kiswahili ilichipukia Kaskazini, Mashariki mwa Kenya na ilitokana na Kingozi na kuna wengine wanadai kuwa Kiswahili chimbuko lake ni Bagamoyo mpaka Mzizima, eneo lililojulikana kama Dar es Salaam hadi Kilwa. Wataalam hawa wanadai lugha ya Kiswahili ilienea kama **Kishomvi**. Madai ya wataalamu hawa hayajawahi kuthibitishwa kwa hoja makini na tafiti zinaonesha kwamba madai hayo hayana ukweli yanahitaji tafiti zaidi. Kwa ujumla madai haya yanaweza kuwekwa kwenye mchoro kama ifuatavyo:-

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA




***NB:*** Kuna kundi la wataalamu wengine linalodai kuwa chimbuko lake ni sehemu mbalimbali za Pwani ya Afrika Mashariki. Mfano mtaalamu ***Freeman Grenvill*** katika makala yake inayoitwa ***Medieval For Swahili (1959)*** anadai kuwa lugha ya Kiswahili ilianza na kuinuka katika upeo wote wa Afrika Mashariki kama ambavyo baadhi ya maneno, majina ya watawala na maofisa wa serikali yanavyojitokeza katika fasihi.

Madai ya mtaalamu huyu yanaashiria kwamba watu walioishi katika maeneo mbalimbali ya upande wa Afrika Mashariki walikuwa wakizungumza lugha zao mbalimbali. Lugha zote hizi zilikuwa za kibantu na hazikutofautiana sana.

Watu hawa katika kuwasaidia hasa katika biashara walilazimika kurahisisha lugha zao kwa kiasi fulani ili waweze kuwasiliana na miongoni mwao. Urahisishaji huo wa lugha na kuzuka kwa lugha hiyo kubwa ni jambo lililotokea katika sehemu zote za upwa wa Afrika Mashariki. Matokeo yake kulizuka lugha ambazo zilijulikana kama lahaja za Kiswahili. Lahaja hizo zilizungumzwa kutoka kusini mwa Somalia hadi Kaskazini-mashariki mwa Msumbiji.

Hapo tunapata lahaja kama vile kitikwa, Kiamu, Chichifundi, Kimvita, Kimombasa, Kimtang'ata, Kimakunduchi, Kihadimu, Kitumbata na Kipemba. Lahaja hizo zinafanana zaidi na lugha mbalimbali za kibantu kuliko zinavyofanana na Kiswahili sanifu kwa kuwa Kiswahili sanifu kina maneno mengi ya mkopo.

## MASWALI

1. Kwa kutumia hoja madhubuti fafanua chimbuko la lugha ya Kiswahili.

2. Wanadai kuwa Kiswahili ni Kiarabu, wanahoja kubwa kuu tatu. Fafanua hoja hizo.

3. Kiswahili ni Kiarabu kwa jina lake, lakini ni Kibantu kwa asili yake, thibitisha kwa hoja za kiisimu.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**UFANIFISHAJI WA KISWAHILI**

i. Kipindi cha Wajerumani Katika kipindi cha Ukoloni wa Kijerumani, shughuli nyingi za ukuzaji wa Kiswahili kimaandishi zilifanywa na Wamisionari wa mashirika mbalimbali ya dini. Sera za mashirika hayo ya dini zilielekeza kuwa uenezi wa mafundisho, ya dini yafanywe kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kazi kubwa iliyofanywa na mashirika ya dini ilikuwa ni kufundisha lugha ya Kiswahili shuleni na pia kuhimiza matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kutolea mafundisho ya dini.

Utawala wa Kijerumani kwa wakati huo haukujishughulisha na kukikuza Kiswahili katika eneo la maandishi. Wajerumani walizingatia zaidi kukijua na kukitumia Kiswahili katika shughuli utawala. Hivyo, ilibidi kila akida, jumbe na liwali afahamu Kiswahili barabara ili aweze kutumiwa na utawala wa Kijerumani katika kufanya kazi mahali popote nchini Tanganyika wakati huo. Katika utawala wa Kijerumani, Kiswahili kilikuwa chombo cha kushughuliikia mawasiliano kati ya watawala na watawaliwa hata hivyo, utawala wa Kijerumani ulisaidia kukikuza na kukieneza Kiswahili kwa sababu Wajerumani ulisaidia kukikuza na kukieneza Kiswahili kwa sababu Wajerumani walisisitiza kwamba kila mtu aliye husiana nao moja kwa moja ilibidi atumie lugha ya Kiswahili kwa ajili ya mawasiliano.

ii. Kipindi cha waingereza Mwaka 1879 Askofu Edward Steere ambaye alikuwa Mwingereza wa Shirika la University Mission to Central Africa( U.M.C.A) aliandika toleo la kwanza la sarufi ya Kiswahili kilichozungumzwa Zanzibar. Kitabu hicho kiliitwa A Handbook of the Swahili language as spoken at Zanzibar. Sarufi hii imeendelea kutumiwa hadi karne ya ishirini. Pia, shirika la U.M.C.A lilieleza kutoa vitabu vingi vya dini kama vile sala na nyimbo ambavyo viliandikwa kwa Kiswahili. Vile vile, Shirika la U.M.C.A chini ya A. Madan ambaye alikuwa bingwa wa lugha lilifanikiwa kutayarisha na kuchapisha kamusi ya Kiswahili – kiingereza na kiingereza- Kiswahili pamoja na kuandika vitabu mbalimbali vya mafundisho ya dini ya Kikristo kwa lugha ya Kiswahili.

Usanifishaji wa Kiswahili Waingereza ndio waliochukua hatua ya kusanifisha lugha ya Kiswahili mara tu baada ya Tanzania Bara ( Tanganyika) kuwa chini ya utawala wa Waingereza. Juhudi zilifanywa ili kuteua lugha moja ya kienyeji itakayotumika katika elimu ya msingi kwenye nchi zote za Afrika Mashariki yaani Tanganyika, Kenya, Uganda na Zanzibar. Hatua ya kwanza ya kuelekea usanifashaji wa Kiswahili ilifanyika mwaka 1925 mjini Dar es salaam wakati Gavana wa Tanganyika alipoitisha mkutano wa wakuu wa elimu wa nchi zote za Afrika Mashariki ili kuzungumzia suala la lugha moja ya kufundishia elimu ya msingi.

Hata hivyo mkutano huo ulihudhuriwa na wajumbe kutoka Tanganyika na Zanzibar. Nchi za Kenya na Uganda hazikutuma wajumbe wake ingawa zilikuwa zimealikwa. Wajumbe wote waliohudhuria walipendekeza lugha ya kibantu itumike katika shule hizo. Kiswahili kilipendekezwa lugha ya kibantu itumike katika shule hizo. Kiswahili kilipendekezwa na kuchaguliwa kuwa lugha ya kufundishia. Hata hivyo, Kiswahili wakati huo kilikuwa na mkusanyiko wa lahaja nyingi. Kwa hiyo washiriki wa mkutano wa 1925 waliteua lahaja tatu kutoka miongoni mwa lahaja mbalimbali za Kiswahili ili zipigiwe kura na kupata lahaja moja. Hatua ya pili ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili ilichukuliwa pale mkutano mwingine wa nchi za Afrika Mashariki ulipoitishwa Juni, 5 , 1928 mjini Mombasa.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wajumbe wote kutoka Tanganyika, Kenya , Uganda na

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Zanzibar pamoja na mwanaisimu mashuhuri Carl Meinhof kutoka Chuo cha International Institute of African Language and Cultures. Kati ya mambo muhimu yaliyozungumzwa ilikuwa ni ripoti ya mkutano wa 1925. Katika hauta ya kwanza ya kuteua lahaja za Kiswahili kuliltokea lahaja kuu tatu za kugombania nafasi ya kuteuliwa ili lahaja moja iwe ya kusanifia lahaja ya Kiswahili sanifu. Lahaja zilizoteuliwa ni kimvita, kiamu na kiunguja. Baada ya mvutano mkubwa katika kikao cha halmashauri hiyo yenye wajumbe kutoka nchi zote nne kiamu kiliangushwa na kubakia kimvita na kiunguja. Baadae kiunguja kikashinda katika mjadala mrefu na kimvita kikaangushwa. Maafikiano ya ripoti hiyo yalikubaliwa na nchi zote baada ya marekebisho ya ripoti hiyo yalikubaliwa na nchi zote baada ya marekebisho Fulani kufanywa. Kiunguja kiliteuliwa rasmi kuwa lahaja ya kusanifishia Kiswahili, lahaja ambayo ilipendekezwa awali na Tanganyika katika mkutano wa 1925.

Kiunguja kiliteuliwa kwa sababu kilikuwa kimekwisha enea katika sehemu kubwa na kilionekeana kuwa na uhusiano mkubwa na lahaja nyingine za Kiswahili. Kiunguja kuteuliwa kuwa lahaja ya kusanifiwa lugha ya Kiswahili kutokana na sababu kuu nne kama ifuatavyo;

**Kwanza**, kiunguja kilikuwa kimekwisha enea sehemu kubwa sana na kueleweka katika nchi zilizokusudiwa yaani Zanzibar, Tanganyika, Kenya na Uganda.

**Pili**, lahaja ya kiunguja ilikuwa imekwisha tumika katika medani ya kitaaluma na kidini hasa Tanganyika tangu wakati wa wajerumani na sehemu kubwa kuenezwa na wahubiri wa dini ya kiislamu na kikristo.

**Tatu**, kimvita kilionekana kuwa kigumu kwa wageni wa lugha hii au watumiaji wa Kiswahili ikiwa lugha ya pili ingewapa taabu katika matamshi hasa kwa yale maneno yanayohitajika kutamkwa kwa ncha ya ulimi. Kwa mfano, neno njoo litamkwe “ndoo” na macho yatamkwe “mato” na mengine kadhaa. Kwa hiyo kiunguja kilishinda kwa sababu kilikuwa lugha nyepesi zaidi, kilichoenea sehemu kubwa sana, kimetajirika zaidi kimsamiati na kwa hiyo kilikidhi haja ya watumiaji wa jamii kubwa iliyokusudiwa.

**Na nne**, tabaka tawala yaani wakoloni wa kiingereza walipenda kiunguja iwe lahaja ya kusanifishwa Kishili na wao ndio walilopendekeza tangu awali kwenye kikao cha mwaka 1925. Pia katika kikao cha mwaka 1928, waingereza waliendelea na msimamo wao wa kutetea kiunguja iwe lahaja ya kusanifia Kiswahili.

Hatua ya tatu ya muhimu katika usanifishaji wa Kiswahili ilichukuliwa Januari 1, 1930 ambapo kamati iliyoundwa ilianza kazi zake rasmi. Kamati hiyo ilijulikana kwa jina la The Inter-Territorial language (Swahili) committee yaani kamati ya lugha ya Kiswahili za nchi za Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa mamlaka iliyopewa, kamati hiyo ilisimamia shughuli zote za kusanifisha lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo:

- Kusanifisha otografia itakayotumika kwa wote kwa kupata maafikiano kamili shughuli zote yaani Tanganyika, kenya, Uganda na Zanzibar
- Kudumisha ulinganifu wa sarufi kwa kuchapisha vitabu vya sarufi vilivyoafikiwa kwa pamoja
- Kuwatia moyo na kuwasadia waandishi ambao ni wenyeji wa lugha ya Kiswahili
- Kuwapa wale wote waliopo na ari ya kuwa waandishi ushauri juu ya uandishi wa vitabu wanavyokusudia kuandika.
- Kusahihisha lugha ya vitabu vya shule na vinginevyo ambavyo vimekwisha chapishwa mara masahihisho yanayohitajika
- Kutafsiri katika Kiswahili vitabu vya kingereza vilivyochaguliwa kutumiwa shuleni kama vitabu vya kiada na ziada

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

• Kuchunguza na pale inapokuwa lazima kusahihisha lugha ya vitabu vya ziada kabla ya havijachapishwa
• Kusoma na kuhakiki vitabu vya Kiswahili vilivyoteuliwa na kamati
• kuwapa waandishi wa vitabu maelezo ya taratibu za kufundishia za wakati uliopo katika Nyanja mbalimbali.
• Kujibu maswali yote kuhusu lugha ya Kiswahili na fasihi yake. Mbali na majukumu yaliyotajwa hapo juu, kamati ilitoa maazimio kadhaa. Baadhi ya maazimio hayo yalikuwa:-
• Kuanzia mwaka 1932, kiunguja kitumike katika shughuli zote za elimu ya chini na serikalini. Lahaja zitakazokubalika ni zile tu za kiunguja kilichosanifiwa
• Lahaja ya Zanzibar ( kiunguja ) pamoja na marekebisho yote yatakayofanyikaikubalike kkuwa lugha sanifu.
• Maneno ya kibantu yatatumika kila inapohitajika, pia maneno ya kiarabu na ya lugha nyingine yaliyojikuta katika matumizi yasipiuuzwe.
• Kitabu cha steere cha Swahili Exercises ma sehemu ya sarufi kiitwacho Handbook pamoja na kamusi ya madan vikubalike kuwa Kiswahili sanifu.

1. Kiswahili kuwa lugha ya taifa nchini Tanzania Baada ya kupata uhuru hapa Tanzania bara, Kiswahili kilipandishwa hadhi na kuteuliwa kuwa lugha ya taifa. Mnamo septemba 1962 Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu J.K. Nyerere alihutubia Bunge kwa mara ya kwanza kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

2. Kiswahili kutumika kufundishia Elimu Kama tulivyoona hapo juu, baada ya Kiswahili kuteuliwa na kuwa lugha ya Taifa,mwaka 1966 kiswahili kilifanywa kuwa lugha rasmi ya kufundishia katika shule za msingi pamoja na vyuo vya ualimu daraja la tatu “A” Tangu uhuru hadi sasa pia, Kiswahili ni somo mojawapo la kitaaluma katika shule za sekondari, taasisi mbalimbali na katika vyuo vikuu ndani ya nchi na hata nchi za nje. Mnano mwaka 1970, serikali ilianzisha idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwa madhumuni ya kutayarisha walimu wenye shahada katika somo la Kiswahili ili waweze kufundisha Kiswahili katika shule za sekondari na vyo vya elimu nchini Tanzania.

**1. Kiswahili kutumika katika kampeni mbalimbali za kitaifa**

Kampeni za kitaifa ni harakati za kufanya mambo haraka kwa watu wengi ili umma ufaidike. Mara baada ya uhuru hasa katika kipindi cha Azimio la Arusha, Tanzania iliendesha kampeni mbalimbali za kitaifa kama vile; kupanga ni kuchagua 1969, uchaguzi ni wako 1970, wakati wa furaha 1971, mtu ni afya 1973, chakula ni uhai 1975 nakadhalika. Kampeni zote za kitaifa ziliendeshwa na zilienezwa kwa lugha ya Kiswahili na watu wengi waliweza kujifunza msamiati mbalimbali juu ya uchumi, siasa, elimu, afya, uchaguzi nakadhalika.

**2. Vyombo vya habari**

Kama tulivyoona katika juhudi za kukuza na kukieneza Kiswahili nchini Tanzania kabla ya uhuru, vyombo vya habari ni mojawapo ya mambo yaliyochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania. Matangazo kwa njia ya redio yalianza baada ya mwaka 1950 hapa Tanzania bara, kwanza kama sautiya Dar es salaam, halafu baadaye kama sauti ya Tanganyika. Pia katika enzi za kabla ya uhuru hapa Tanzania bara magazeti ya Kiswahili yaliyokuwa yakitolewa kusomwa na wananchi ni kama vile: ***Mambo leo, habari za leo, tazama, baraza, rafiki yetu na kiongozi.***

**3. Sherehe na mihadhara mbalimbali ya kiutawala, kijamii, kisiasa na kidini**

Harakati za kiutawala na mambo ya kisiasa tangu uhuru hadi sasa huendeshwa katika lugha ya kiswahili. Kwa mfano, Kiswahili hutumika bungeni, mahakamani na kwenye mikutano ya kampeni ya kisiasa hususani kwenye kipindi cha uchaguzi. Pia, shughuli za sheherehe mbalimbali za vyama ambapo wageni rasmi au viongozi wakuu hutoa hotuba zao kwa kutumia lugha ya kisahili. Jambo hili limetoa na linaendelea kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiswahili.

**4. Kuundwa kwa taasisi (vyombo) mbalimbali za kukuza, kuimarisha na kuendeleza** lugha ya Kiswahili Nchini Tanzania tangu uhuru hadi sasa

Kama tuliyvoona hapo juu, baada ya lugha ya Kiswahili kupata hadhi ya kutambuliwa na kuwa lugha ya Taifa, taasisi, mashirka na vyama mbalimbali viliundwa kwa makusudi ya kuendeleza, kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania. Baadhi ya vyombo hivyo ni hivi vifuatavyo

1. **Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)**

Mwaka 1970, profesa George Mhina aliyekuwa Mkurugenzi wa kwanza mzawa wa TUKI aliyetaja madhumuni ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili kuwa ni

- Kushughulika na ukuzaji wa maneno ya Kiswahili na utengenezaji wa kamusi ya Kiswahili/ mnamo mwaka 1981 TUKI ilichapisha kamusi ya Kiswahili- Kiswahili. Na mwaka 2004 TUKI ilitoa toleo la pili la kamusi ya Kiswahili ya Kiswahili- Kiswahili.
- Kuendesha uchunguzi wa lugha kwa madhumuni ya kukukza na kustawisha Kiswahili
- Kuhifadhi ufasaha wa lugha ya Kiswahili
- Kuwatia moyo watu wanaojishughulisha na uandishi wa vitabukatika lugha ya Kiswahili
- Kutafsiri maandishi yafaayo katika Kiswahili
- Uhariri wa vitabu na utoaji wa jarida la Kiswahili na jarida dogo liitwalo mulika.

Ili kutekeleza majukumu hayo hapo juu, TUKI ilikuwa na sehemu kuu nne ambazo ni fasihi, isimu, uchapishaji na kamusi.

- Sehemu ya fasihi ilijishughulisha na uchunguzi wa fasihi simulizi na fasihi andishi
- Sehemu ya Isimu ilijishughulisha na utafiti katika sarufi na matumizi ya Kiswahili pamoja na utafiti wa lahaja mbalimbali Kiswahili.
- Sehemu ya istilahi na tafsiri ambayo ilishugulikia fani mbili yaani istilahi na tafsiri
- sehemu ya Kamusi ilishughulikia uundaji wa kamuzi mbalimbali pamoja na kuandaa istilahi ya masomo mbalimbali

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

NB. Kuanzia mwaka 2009 TUKI imebadili jina na kuitwa Taasisi ya Taaluma za Kiswahil (TATAKI)

**Majukumu**

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) ni taasisi ya utafiti na ufundishaji iliyopewa jukumu la kutafiti na kufundisha nyanya zote za lugha ya Kiswahili, fasihi na utamaduni, na uchapishaji wa matokeo ya utafiti huo. TATAKI vile vile ina jukumu la kutekeleza mipango ya sasa nay a muda mrefu ya muda mrefu ya elimuna maendeleo ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Malengo**

Malengo makuu ya Taasisi ya taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam ni haya yafuatayo;-

(i) Kufanya utafiti katika Nyanja mbalimbali za mofolojia ya Kiswahili, sintaksia, fonolojia, ismujamii na lahaja

(ii)kufanya utafiti katika leksikografia ya Kiswahili na kutunga kamuzi za jumla na za masomo

(iii)kufanya utafiti na kutunga istilah mpya kwa ajili ya taaluma mbalimbali na /au kwa ajili ya maeneo maalum ya kitaaluma

(iv)kuratibu na kutoa huduma za tafsiri kwa ajili ya ofisi za Serikali, mashirika ya umma, viwanda, taasisi na watu binafsi ndani na nje ya nchi.

(v)Kufanya utafiti wa fasihhi simulizi na fasihi andishi, sanaa za maonyesho, mila na destruri na utamaduni wa mtanzania na wa jamii za Afrika Mashariki

(vi)Kushirikiana na asasi nyingine katika kuendeleza lugha ya Kiswahili na kutoa huduma za ushauri katika Nyanja mbalimbali za lugha ya Kiswahili na fasihi

(vii)Kuchapisha maandiko ya kufundishia Kiswahili katika shule na vyuo

(viii)Kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakuwa na msingi mzuri kuwa lugha ya kufundishia katika shule na katika ngazi ya elimu ya juu.

(ix) Kuendeleza Kiswahili kwa kutumia teknolojia mpya.

**(ii) Chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA)**

Chama hiki kilianza kabla ya uhuru tarehe 29/3/1959, lakini kazi zake zilijitokeza rasmi hasa baada ya uhuru. Madhumuni ya chama cha UKUTA yalikuwa:

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Kuhifadhi na kustawisha lugha ya Kiswahili fasaha na ushairi wake kwa misingi ya kibantu pamoja na kustawisha ushairi ukiwa stadi maalum inayosaidia elimu ya Kiswahili kwa faida ya Taifa zima
- Kamsha na kkuchochea ari za watu wanaotaka kuwa watalamu katika fani za ushairi
- Kustawisha utamaduni wa michezo ya ngojera na kuigiza
- Kuamsha juhudi za wale wanotaka kutunga vitabu vya elimu mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili na vya ushairi

Katika uhai wake, chama cha UKUTA kilijishughulisha zaidi uendeshaji wa sanaa za ushairi na ngonjera na kutoa vitabu kadhaa vilivyoitwa Ngojera za ukuta

**(iii) baraza la Kiswahili Tanzania ( BAKITA)**

BAKITA iliundwa kwa mujibu wa sheria ya Bunge ya mwaka 1967 ili kutoa mwongozo wa lugha ya Kiswahili nchini. Wanachama wake hutoka katiak Wizara mbalimbali za Serikali, mashirkka na watu binafsi. Kazi za BAKITA NI:

- Kushirikiana na vyama na vyuo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vinavyohusika na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili na kuunganisha juhudi na kazi zao
- Kutilia nguvu mafanikio ya peo za juu katika kkutumia lugha ya Kiswahili na kuzuia kadri iwezekanavyo matumizi yake mabaya
- Kukuza maendeleo na matumizi ya Kiswahili sanifu na fasaha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Kushirikiana na Wizara/idara zinazohusika katika kuunda au kutoa tafsiri za maneno ya Kiswahili
- kutoa jarida la Kiswahili linaloongoza matumizi sahihi ya maneno na maendeleo yake.

BAKITA ina kamati ya kusanifu lugha ambayo iliweka utaratibu ulianza kutumika mwaka 1974 baada ya agizo la Waziri Mkuu wa wakati huo. Utaratibu huo umekuwa ukifanyiwa marekebisho ili kwenda na wakati.

Utaratibu huo unazingatia yafuatayo:-

- Istilahi mpya zinatakiwa zipatikane kutokana na Kiswahili chenyewe pamoja na lahaja zake
- Kama istilahi hizi haziwezi kupatikana kuktoka katika Kiswahili, juhudi zinafanywa na kuzitafuta istilahi hizi kutoka katika lugha za makabila ya kibantu
- Vile vile lugha za makabila yetu ambayo si ya kibantu hufanyiwa uchunguzi ili kuzipata istilahi mpya
- Neno jipya linaundwa kwa kuunganisha silabi chache kutoka katika maelezo ya neno hilo
- Maneno mawili au matatu huunganishwa na kupaa neno moja na misingi ya lugha ya Kiswahili

Vile vile, Baraza la Kiswahili Tanzania hutayarisha mijadala redioni kuhusu matumizi bora ya maneno, na wakati mwingine hushughulika na uchunguzi katika matumizi ya lugha ya Kiswahili

**(iv) idara ya Kiswahili- Chuo kikuu cha Dar es salaam**

Idara ya Kiswahili ilianza mwaka 1970 baada ya/chuo Kikuu cha Dar es salaam kuzaliwa rasmi. Lugha itumiwayo kufundishia masomo ya fasihi, matumizi, miundo na nadharia za isimu ni

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kiswahili madhumuni ya idara yalikuwa ni kawaandaa wataalamu wenye shahada katika masomo ya Kiswahili ili waweze kutumia katika Nyanja mbalimbali za maendeleo nchini. Masomo ambayo yamekuwa yakitolewa na idara hii ni fasihi, matumiz, miundo na nadharia za Isimu. Masomo yote haya hufundishwa katika lugha ya Kiswahili tangu idara ya kishwahili ianzishwe, imetoa wahitimu wengi ambao wanafundisha somo la Kiswahili katika shule za Sekondari na vyuo mbalimbali vya elimu ya juu, pia idara imetoa wahitimu wa shahada ya pili (uzamili) (M.A) na shahada ya tatu ( uzamivu ) (Ph.D)

**(v) taasisi ya Kiswahili na lugha za kigeni Zanzibar (TAKILUKI)**

Taasisi hii ilianzishwa kwa mujibu wa sheria Na.04 ya mwaka 1979 na kupewa hadhi kuwa shirika. Taasisi ya Kiswahili na lugha za kigeni ( TAKILUKI) inafanya kazi chini ya udhamini wa Wizara ya Elimu- Zanzibar. Baadhi ya kazi za TAKILUKI ni;

- Kutoa mafunzo na masomo ya Kiswahili kwa kiwango cha juu kwa watumishi wa Serikali kwa ujumla na kuwaingiza katia kunga za Kiswahili fasaha
- Kuendesha mafunzo ya masomo ya Kiswahili na lugha za kigeni kwa wanafunzi wenyeji na wageni kutoka nje ya Tanzania.
- Wanafunzi kigeni hupewa mafunzo ya lugha ya Kiswahili katika ngazi ya msingi kati na juu
- Kufanya utafiti wa lahaja, fashihi simulizi na fasihi andishi ya kiswahili

---

# FASIHI KWA UJUMLA

**NADHARIA YA FASIHI**

**SANAA**

Sanaa ni uzuri unaojitokeza katika umbo lililosanifu umbo ambalo msanii hulitumia katika kufikishia ujumbe aliokusudia kwa jamii / hadhira.

**AINA ZA SANAA**

**a) Sanaa za ghibu (muziki)**

Inategemea na matumizi ya ala za muziki (vifaa, sauti) uzuri wa umbo la sanaa ya muziki upo katika kusikia. Sanaa hii hailazimishi fanani (msanii) na hadhira kuwepo mahali pamoja kwa wakati mmoja. Mtunzi hufanya kazi kwa wakati wake na hadhira husikiliza kwa wakati wake.

**b) Sanaa za ufundi**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Sanaa hizi hutokana na kazi za mikono. (Mfano: uchoraji, ususi, ufinyanzi, uchongaji, uhunzi, utalizi/udalizi n.k.)

Mfano; - uchoraji hutegemea sana kuwepo kwa kalamu, karatasi, kitambaa, brashi, rangi n.k. uchongaji huhitaji mundu, gogo, tupa, n.k. Uzuri wa umbo na sanaa za ufundi upo katika kuona. Sanaa hii hailazimishi fanani na hadhira kuwepo mahali pamoja kwa wakati mmoja.

**c) Sanaa za maonesho**

Ni kazi mbalimbali za Sanaa ambazo hutegemea utendaji (mfano: ngoma, maigizo, majigambo, matambiko n.k) sanaa zilizomo kwenye kundi la sanaa za maonesho ni lazima ziwe na sifa zifuatazo:-

-Fanani

-Dhana inayotendeka

-Hadhira

-Mandhari


Sanaa za maonesho zinalazimisha fanani na hadhira kuwepo mahali pamoja kwa wakati mmoja, kwani uzuri wa umbo la sanaa hii upo katika kuona utendaji.

**a) Fasihi**

Sanaa hii inategemea ufundi wa matumizi ya lugha. Msanii ni lazima awe na uwezo wa kutumia vionjo vyote vya lugha (mfano; methali, misemo, tamathali za semi, nahau, vitendawili n.k)

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kufikisha ujumbe unaokusudiwa kwa hadhira inayokusudiwa. Sanaa hii pia hailazimishi fanani na hadhira kuwa pamoja, mahali pamoja.

**KIELELEZO CHA SANAA**




Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kila kipengele cha Sanaa kinatofautiana na kingine kwa umbo na matumizi. Fasihi ni kipengele cha sanaa kinachotumia maneno kuumba huo uzuri wa kisanaa

**TOFAUTI KATI YA FASIHI NA TANZU ZINGINE ZA SANAA**

**i. LUGHA**

Kazi zote za fasihi zinaundwa kisanaa kwa kutumia lugha inayotamkika na inayoandikika ambayo hubeba ujumbe fulani tofauti na sanaa zingine kama vile.

- Ufinyanzi hutumia udongo
- Uchoraji hutumia kalamu, rangi, karatasi au kipande cha nguo.

**ii. WAHUSIKA**

Kazi ya fasihi hulazimika kuwa na wahusika wake ambao matukio mbalimbali yanayohusu jamii inayowazungukia. Hutumika kutoa dhamira ya mwandishi, Pia hutumiwa kuwasilisha tabia za watu waliomo ndani ya jamii

**iii. MANDHARI**

Fasihi huwa na mandhari ambayo huonyesha tukio linapofanyika. Mandhari inaweza kuwa ya kubuni au ya ukweli.

**iv. UTENDAJI**

Utendaji hujitokeza hasa katika kazi ya fasihi simulizi ambazo hushirikisha hadhira na fanani mahali pamoja na kwa wakati mmoja, Hapa fanani huweza kuonesha matendo katika usimuliaji wake.

**v. FANI NA MAUDHUI**

Fasihi ina sehemu hizi mbili za fani na maudhui ambazo hutegemeana na hufungamana. Fani ni namna msanii anavyosema kuhusu kile kinachosemwa wakati maudhui ni kile kinachosemwa na msanii.

**USANAA WA FASIHI**

**Usanaa wa fasihi hujitokeza katika vipengele vifuatavyo:**

1. **Mtindo**

Sanaa katika fasihi hujidhihirisha katika namna ya kueleza jambo, Hapa kinachoangaliwa zaidi ni zile mbinu mbalimbali zinazotumiwa na msanii katika kueleza jambo husika. Jambo huweza kuelezwa katika fumbo kwa kupitia; shairi, tamthiliya, hadithi, kitendawili n.k.

1. **Muundo**

Huu ni mpangilio mzuri wa visa na matukio. Matukio katika kazi za fasihi hupangwa kiufundi ili yaweze kuwasilishwa vizuri kwa hadhira au jamii husika.

1. **Uteuzi mzuri wa "lugha":**

Iliyojaa vionjo mbalimbali kama vile nahau, misemo, tamathali za semi, taswira na ishara. Lugha inaweza kuchekesha, kukosoa, kukejeli, kubeza, kushawishi n.k

1. **Uundaji mazuri wa "wahusika".**

Wahusika huumbwa kulingana na nia na lengo la mwandishi kwa hadhira wake.

1. **Ujenzi mzuri wa "Mandhari".**

Kazi ya fasihi ni lazima iwe kwenye madhari maalum. Mandhari ikijengwa vizuri husaidia sana kujenga hisia inayokusudiwa na mwandishi kwa hadhira wake ili iwezeshe pia kufiksha ujumbe mahsusi uliokusudiwa.

**FASILI ZA FASIHI**

**FASIHI NI KIOO**

Fasihi ni kioo kwa kuwa fasihi inaweza kufananishwa na kioo. Kioo katika maisha ya kawaida huweza kumuonesha binadamu mazuri aliyonayo au mapungufu aliyonayo ili aweze kujikubali au kujikataa. Hivyo fasihi pia ina uwezo wa kuonyesha mazuri au mapungufu yaliyomo ndani ya jamii, aidha kwa jamii au kwa baadhi ya vikundi vilivyomo ndani ya jamii ambavyo huweza kuwa tofauti na mahitaji ya jamii nzima.

**Udhaifu:**

-Udhaifu unaojitokeza katika fasihi hii ni kwamba fasihi ina uwezo wa kuonesha mambo kama ni mabaya au mazuri lakini haina uwezo wa kuonesha njia ya kutatua matatizo hayo kama kilivyo kioo.

**Udhaifu wa fasili ya fasihi ni hisi**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Je ni mara ngapi mwanafasihi ataguswa ndipo aweze kuandika kazi ya fasihi? Je ni mwandishi pekee ndiye anayetakiwa kuguswa? Ukweli ni kwamba sio kazi zote zinazoandikwa zinataokana na mguso unaompata mwandishi.

1. **FASIHI NI MWAMVULI**

Fasili ya fasihi ni mwamvuli ilifananishwa na mwamvuli kwa jinsi inavyoweza kumhifadhi binadamu kwa jua au mvua lakini nadharia halisi ya fasili kufananishwa na mwamvuli ni katika uelekeo wa kwamba fasihi inauwezo wa kulinda amali za jamii zisipotee na zisiweze kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.

**Udhaifu**: - fasili hii ilionesha udhaifu wa fasihi kutokuwa na uwezo wa kulinda amali za jamii yaani mila na desturi zilizopotea kwani mila na desturi ndani ya jamii huwa zinaenda na wakati na hubadilika kulingana na mahitaji ya wakati huo.

iii. **FASIHI NI HISI**

Dhana hii ilikuwa na maana kwamba kazi ya fasihi inapoletwa mtoaji/ msanii ni lazima awe anaguswa na jambo fulani na ndipo aweze kuandika kazi hiyo.

1. **FASIHI NI KIELELEZO CHA KISANAA**

Fasihi inatazamwa Kama ni ubunifu au ufundi wa aina fulani unaojidhihirisha katika maandishi.

**Udhaifu:** - fasili hii huzingatia zaidi utoaji wa burudani tu na hauzungumzii lolote juu ya uelimshaji wa nini kifanyike juu ya tatizo alilolionesha msanii.

1. **FASIHI**

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha ambayo msanii huitumia ili kuweza kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Fasihi huwa ina umbo timillifu, Mfano kazi ya fasihi inaweza kuwa tamthiliya (igizo), hadithi au ushairi.

Uhai wa lugha katika kazi ya fasihi inaongeza mvuto. Lugha inaweza kupewa uhai huo kwa kutumia tamathali za semi kama vile tashibiha, tasfida, sitiari, kejeli, dhihaka, balagha kijembe n.k. vipengele vingine vinavyotawala ufasihi ni uundaji wa wahjusika, maatumizi ya picha, mandhari, utendaji, n.k

**Mfano**:-

Mtoto aloumbika, mara mtoto laini

Shingo yake ya birika, watabasamu moyoni

Kweli asali tamu, wajua ilivyoundwa

Hapa unaweza kupata ujumbe kwa kupitia maswali mbalimbali.

- Mhusika ameumbwaje?
- Shingo yake inafananishwa na nini
- Uzuri wa mototo umeoneshwaje?
- Asli imetumika kwa sababu gani?
- Swali lililo kwenye mstari wa mwisho limeulizwa kwa sababu gani?

**MADHUMUNI YA FASIHI**

Fasihi ni kazi inayotokana na jamii na ipo kwa ajili ya jamii.

Kazi ya fasihi na fasihi yenyewe huathiriwa na mazingira na maendeleo ya jamii.

**MADHUMUNI**

**Fasihi hushughulikia mahusiano ya jamii, hivyo basi fasihi:-**

1. Hueleza ukweli wa maisha ya jamii
2. Hujenga udadisi kujielewa na kuelewa watu wengine
3. Huendeleza, hudumisha na kurithisha utamaduni wa jamii
4. Huonesha jamii njia na mitindo mbalimbali ya kujieleza
5. Huburudisha kupitia mvuto ulimo ndani ya LUGHA, MUUNDO na MAUDHUI yake.
6. Huijenga jamii kifikra na kisiasa ili kuwezesha kutoa maamuzi na kuwa na msimamo wa maamuzi hayo.

**DHIMA YA FASIHI**

1) Huelimisha, katika kupitia maonyo (huonya) hutohamisha ukweli, huelekeza, hutoa mawaidha na kuonesha mwanga wa migogoro.

2) Huburudisha kupitia maliwazo (huliwaza), hufundisha,hubembeleza, huhamasisha, hutuliza mawazo.

**DHIMA YA MWANAFASIHI**

1) Huelimisha

Hufanya kazi ya kuelimisha kwa kukosoa, kutia hamasa, kuonya, kueneza mawazo na falsafa za jamii

2) Huburudisha

3) Huhifadhi na kurithisha amali za jamii.

4) Hudumisha na kuendeleza lugha

**MATUMIZI YA FASIHI**

Matumizi ya fasihi hutegemea sana msimamo na mikabala ya wasimulizi na waandishi. Kwa kawaida mtunzi hujiambatisha na tabaka Lake. Kwa hali hii ndiyo maana:

1) Mwandishi wa tabaka la watawala kutetea kwa kusifia tabaka hilo

2) Mwandishi wa tabaka la wakandamizwaji ataandika maudhui ya kujikomboa yaani kulikomboa tabaka lake.

3) Anayetokana na udhamini, utunzi wake hulazimishwa kutetea tabaka lisilo lake ama kwa hofu, kwa malipo au yote kwa pamoja.

**UHURU WA MTUNZI WA KAZI ZA KIFASIHI**

Ni hali ya mwandishi wa fasihi kuwa huru na wazi kutoa mawazo yake na hisia zake kwa jamii bila ya kupingwa na tabaka lolote.

Au ni ile hali ya kutunga au kuandika kazi yake bila kushinikizwa na mtu, watu au taasisi fulani yenye nguvu kiuchumi, kisiasa na kitawala. Mtunzi wa kazi ya fasihi anakuwa na uwezo wake binafsi wa kufanya maamuzi juu ya fani na maudhui ya kazi yake.

**NGUZO KUU ZA DHANA YA UHURU WA MTUNZI WA KAZI ZA KIFASIHI**

**1) UTASHI**

Ni hali ya kuamua kuazimia au kukusudia jambo bila kushurutishwa au kuyumbishwa.Moja ya dhima ya mtunzi ni kuiamsha jamii iweze kutambua unyonyaji, ukandamizaji na uonevu uliomo ndani ya jamii ili iweze kuchukua hatua ya kukomesha hali hizo. Hivyo mtunzi anapotimiza dhima hii anaweza kukabiliana na tabaka kandamizi. Hapo ndipo utashi wa mtunzi unapoweza kumwelekeza kusonga mbele na jukumu lake au kuwa kasuku wa kusifia tabaka tawala au kandamizi kwa kufunika maovu ya tabaka hilo au kujiondoa kabisa kwenye ulingo wa fasihi.

Mfano Ngugi wa Thiong’o aliwahi kuhukumiwa na serikali ya Kenya alipoandika tamthiliya ya “THIS TIME TOMORROW” kwa kukosoa uovu wa tabaka tawala. Utashi umemfanya mpaka leo aendelee na msimamo wake ule ule.

**2) FALSAFA**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mwandishi anapaswa kuwa na falsafa moja inayoeleweka ambayo huyafanya maandishi yaonekane kama kazi moja yenye mwelekeo maalum. Mwandishi akipoteza uhuru huweza kuyumbishwa kirahisi; Mfano mwandishi anaweza kuandika kuhusu ujamaa, kesho akaandika kuhusu mapenzi, kesho kutwa kuhusu ubepari

Mwandishi asiye huru huwa ni mtumwa wa hali mbalimbali za maisha zinazomfanya ayumbeyumbe huku na kule.

### 3) SANAA

Mwandishi anapaswa kuwana weledi wa misingi ya aina ya utunzi wa sanaa anayotaka kuitumia kufikisha ujumbe wake. Mfano: Akitaka kufikisha ujumbe kwa njia riwaya ni lazima ajue barabara misingi ya uandishi wa riwaya vinginevyo msanii hatokuwa na uhuru wa kisinaa maana hatakuwa na namna yenye nguvu ya kukisema hicho alichonacho.

### 4) LUGHA

Msanii ambaye hana weledi wa lugha na misingi ya lugha anayoitumia ni lazima atajikuta amefungwa. Hatakuwa na uhuru wa kusema kile kilichomo nafsini mwake kwa ufasaha na kwa mafanikio.

## DHIMA YA UHURU WA MWANDISHI

1. Mwandishi awe huru kuikosoa jamii au kulikosoa tabaka lolote linalokwenda kinyume na maadili ya jamii
2. Mwandishi awe na falsafa inayoeleweka na utashi
3. Kuikomboa jamii kutoka katika fikra mbovu za kugandamizwa, kunyonywa na kuonewa na tabaka tawala.
4. Uandishi wa kikasuku kupungua
5. Unaifanya fasihi kuwa chombo cha kuikomboa jamii KIUCHUMI, KISIASA, KIUTAMADUNI, KIJAMII NA KIFIKRA.
6. Mwandishi anakuwa na uhuru wa kuisukasuka jamii bila matatizo yoyote.

## UDHAMINI

Udhamini wa kazi ya fasihi ni kitendo cha mtu au chombo fulani kukubali kufadhili au kugharamia kazi ya mtunzi ili iweze kuchapishwa na hatimaye kusambazwa mahali mbalimbali hadi iwafikie walengwa.

## AINA ZA UDHAMINI

1. **UDHAMINI WA KISHAWISHI**

Huu ni udhamini ambao mdhamini humshawishi mtunzi wa kazi ya fasihi aidha kwa fedha au masilahi mengine. Hali hii humfanya mtunzi kwa hiari yake kuingia katika udhamini.

2. **UDHAMINI WA NGUVU**

Huu ni udhamini ambao hutolewa na vyombo vya dola. Mtunzi huingia katika udhamini huu kwa lazima. Dola hudhamini watunzi ili waweze kuandika kile kilichoagizwa na dola. Hivyo mtunzi huandika na kuingia katika udhamini huu kwa nguvu ya dola kwa kuogopa aidha kazi zake kuzuiwa au kuondolewa kabisa katika ulimwengu fasihi.

3. **UDHAMINI WA MTUNZI MWENYEWE**

Huu ni udhamini ambao mtunzi mwenyewe hujisimamia binafsi katika kugharamia gharama zote za uhariri, uchapaji na usambazaji wa kazi zake. Mara nyingi hufanywa na watunzi wenye uwezo

4. **UDHAMINI WA MAKAMPUNI YA UCHAPISHAJI**

Yapo makampuni mbalimbali ya uchapishaji ambayo hupokea miswaada kisha wanaithamini, wanaihariri, wanaichapisha na kuisambaza kwa wasomaji. Makampuni haya hutoa fedha kwa ajili ya mambo yote hayo kwa matarajio ya kurudisha pamoja na faida wakati wa mauzo ya kazi inayohusika.

## DHIMA YA UDHAMINI WA KAZI YA FASIHI .

(a) Kuwawezesha watunzi wasiokuwa na uwezo wa kifedha kuchapisha kazi zao na kuzifikisha kwa hadhira.

(b) Kuibua vipaji vya watunzi. Kwa kawaida kuna watu wengi wenye vipaji lakini hawavitendei haki kwa vile hawana uwezo wa kuendelea na hatua za mbele kama vile uchapishaji na usambazaji.

(c) Mdhamini hujitangaza. Udhamini humuwezesha mdhamini kujitangaza ama kibiashara au kupata heshima miongoni mwa jamii.

(d) Ni njia ya kuleta kipato kwa wadhamini. Kwa mfano kwa makampuni ya uchapishaji.

(e) Kuwapatia watunzi fedha za haraka kabla na baada ya kazi kuuzwa.

(f) Kuwainua watunzi chipukizi kwa kuwawezesha kufikisha kazi zao kwa hadhira ili ujumbe uliokusudiwa uwafikie waliokusudiwa.

(g) Kuwafanya watunzi chipukizi kufahamika.

## ATHARI ZA UDHAMINI WA FASIHI.

**Udhamini wa kazi za fasihi una athari mbalimabali, zifuatazo ni baadhi ya athari hizo :-**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(a) Mtunzi huandika kazi yake kulingana na matakwa ya mdhamini. Kwa mfano iwapo udhamini uliotolewa na kazi zilizo katika lugha ya kiingereza, msanii anayetumia lugha ya Kiswahili kuandika kazi zake hawezi kufaidika na udhamini huo.

(b) Mtunzi hushindwa kuandika mambo kulingana na mtazamo wake halisi juu ya jamii inayo mzunguka.

Mtunzi hushindwa kukosoa uovu hasa unapokuwa unamhusu mdhamini wa kazi yake.Kwa mfano serikali au tabaka tawala.

(c) Kukua kwa fasihi pendwa kwa mfano riwaya pendwa na, kudumaa kwa fasihi dhati mfano riwaya dhati. Hali hii inatokana na msukosuko wa kibiashara. Fasihi pendwa inauzwa kirahisi sokoni. kwa kuwa na maudhui yenye msisimko kwa mfano upelelezi, usambazaji, mauaji, mapenzi n.k.

(d) Mapana ya kijographia na utafiti wa fasihi kabla ya kuandikwa hutegemeana na uwezo wa kifedha wa mdhamini.

(e) Uhuru wa mwandishi hutoweka.

---

# MAENDELEO YA FASIHI SIMULIZI

**UWASILISHAJI NA UENEZAJI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI**

**FASIHI SIMULIZI**:

Fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia mazungumzo na matendo katika kuwasilisha ujumbe Fulani kwa watazamaji au wasikilizaji. Mazungumzo hayo huweza kuwa ya kuimbwa kutendwa au kuzungumzwa, Aina hii ya fasihi imepokelewa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo.

Msimulizi katika fasihi simulizi mbali na kutumia mdomo wake hutumia viungo vyake vya mwili kama mikono, miguu, ishara mbalimbali katika uso wake na hata kupandisha na kushusha sauti yake. Kwa ujumla anaweza kutumia mwili wake mzima katika kuwasilisha na kufanikisha ujumbe wake kwa hadhira yake ambayo huwa ana kwa ana. Isotoshe anafaulu katika kutoa picha halisi ya dhana anayotaka kuiwasilisha kama ni ya huzuni, furaha, kuchekesha n.k.

Zaidi ya kusimulia, kuimba na kuigiza msanii wa fasihi simulizi huwa na nafasi ya kushirikisha hadhira yake kama wahusika katika sanaa yake. Anaweza kutimiza hayo kwa kumfanya mshiriki mmoja kuigiza jambo fulani au kufanya hadhira yote kuimba au kufanya matendo mbalimbali.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Ufundi wa aina hii huhitaji umahiri wa hali ya juu. Hali hii humpa msanii wahakiki wake hapohapo.

Kwa upande mwingine hadhira nayo huwa na nafasi na uhuru wa kushiriki au kuuliza maswali pale ambapo hawakuelewa, Vilevile wanapata fursa ya kuonesha hisia zao. Kuhimiza, kukumbushana na kwa hali hiyo fasihi simulizi huwa na uwezo wa kufundisha zaidi. Kwa kuzingatia maoni ya kirumbi (1976) hivyo kutokana na maelezo yaliyotangulia tunaafikiana nae kwamba fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia mazungumzo na matendo katika uwasilishaji wa ujumbe ulikusudiwa kwa hadhira. Mazungumzo hayo huwa katika mfumo wa masimulizi, kwa kuimbwa, kutambwa, kughaniwa na kutongolewa.

Fasihi simulizi hueleza jamii kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa, Fasihi huzungumzia mambo ambayo huzunguka jamii husika. Fasihi simulizi huathiri malezi ya watu kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo na matendo.

Fasihi simulizi huenda sambamba na mabadiliko ya jamii na kwa hivyo nayo hubadilika kimaudhui na kifani kufuatia mabadiliko ya mifumo ya KISIASA, KIJAMII na KIUCHUMI. Fasihi simulizi ni utanzu wa kisanaa ulio hai na ambao hukua na kubadilika kutokana na mabadiliko ya wakati na ya mifumo ya jamii.

Hivyo fasihi simulizi ni tukio linafungamana na muktadha (mazingira) fulani ya jamii kutawaliwa na mwingiliano wa mambo yafuatayo:-

**a) MSIMULIZI (FANANI)**

Huyu ni mtu ambaye anaitamba hadithi, kuimba wimbo kutoa methali au vitendawili.

**b) WASIKILIZAJI AU WATAZAMAJI (HADHIRA)**

Hawa huwa ni washiriki katika kutazama au kusikiliza fani za fasihi simulizi na mara nyingine huwa wanatumiwa na fanani kama wahusika wa fani yake.

**c) MAHALI (MANDHARI)**

Hapa ni jukwaa au mahali ambapo tukio la fasihi simulizi linatendeka mahali hapo panaweza kuwa nyumbani, uwanjani n.k.

**d) TUKIO.**

Ni shughuli ya kijamii ambayo ndiyo muktadha wa utendaji huo wa sanaa mathalani harusi, kazi Fulani, sherehe, msiba, ibada n.k. utendaji huo waweza kuwa katika usimulizi wa hadithi, kutega vitendawili kuimba wimbo/nyimbo au kutoa methali.

**e) WAKATI**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Ni muda maalumu wa kihistoria au majira maalum ya utendaji huo.

**UHIFADHI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI**

**Fasihi simulizi inaweza kuhifadhiwa kwenye maandishi na kanda za sauti kwa madhumuni ya kumbukumbu. Tunaweza kutambua fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:-**

1. Kama ilivyoelezwa hapo awali inategemea mdomo wa msimulizi (mtendaji) na masikio ya hadhira.
2. Fasihi simulizi ni hai kwa sababu inategemea uhusiano wa ana kwa ana wa msimulizi(mtendaji) na hadhira yake kwa hiyo lazima uwepo utendaji wa maneno au wa muziki au wa matendo utakaowasilisha tungo za mtendaji kwa hadhira yake. Utendaji huu hutegemea sana kiimbo shadda milio na vihisishi.
3. Fasihi simulizi inatendwa hivyo lazima iwe na mtendaji. Huyu anaweza kuwa mwimbaji, msemaji au mtendaji. Kazi yake ni kuanzisha au kueneza tungo au kazi zote mbili. Mtendaji huyu hutumia vifaa vya kusikika au kuonekana katika kujieleza, kwa mfano wimbo toni za miondoko kwa njia hii anakuwa karibu sana na hadhira yake.
4. Kwa kuwa kila mtu anaweza fuatilia kwa kiasi na kwa kuwa fasihi simulizi inategemea kumbukumbu za mtu binafsi hadhira inapotumia na kueneza tungo za fanani pia huimbwa usanii na kuzijenga tungo hizo kwa namna zao. Jambo hili hufanya kazi ya fasihi ielezwe kwa namna kadha kutegemea mazingira na masimulizi.
5. Kukabiliana na hadhira moja kwa moja kuna athari katika tungo za fasihi simulizi, fanani huweza kubadilisha tungo katika utendaji wake kadri apendavyo ili mradi akuze uzuri wa kazi yake au alete athari Fulani inayokidhi haja ya wakati ule.
6. Mwambatano wa tungo na mazingira maalum ni muhimu mazingira huathiri sana usanii wa tunngo na maudhui yake. Zipo tungo ambazo huambatana na matukio maalumu na hata kama zimepitwa na wakati huweza kugeuzwa zikasadifu kipindi mahususi.

Fasihi simulizi ina tabia ya uhai na hutegemeana na sanaa za maonyesho na ghibu yaani sanaa ya muziki, Tabia hii inaitwa hali ya utegemezi. Hii ni kwa sababu huchota uhai wake kutokana na vitendo na vitabia vya fanani, mahadhi, toni za muziki na vipengele vingine vya sanaa za maonyesho.

Bila kuzingatia vipengele hivi vya utendaji kazi ya fasihi simulizi inaweza kuchapwa kwa mfano bila mahadhi, madoido, upigaji ngoma, miondoko ya uchezaji na mazingira ya tukio unamotumiwa wimbo unaweza kukosa uhai wake.

**TANZU ZA FASIHI SIMULIZI**

Kuna makundi mawili muhimu ya tanzu ya fasihi simulizi, kundi moja linahusu tanzu zenye mwelekeo wa kishairi na kundi jingine linashughulikia tanzu za kinathari au zenye sifa za kihadithi.

Tanzu za kishairi zina sifa nyingi za ushairi kuliko tanzu zenye lugha ya kinathari, Ushairi aghalabu hutumia lugha ya kitamathali na mkato. Pia ushairi una mizani ulinganifu wa sauti na mapigo.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Matteru (1987) amesema kwamba katika muktadha wa fasihi simulizi zenye kutumia mapigo kwa utaratibu maalumu. Mapigo haya yanaweza kuwa ya muziki au yoyote yale yaliyopangwa kwa muwala wa uwazi.

Tanzu kama nyimbo, maghani, methali, vitendawili, misimu hupatikana katika kundi hili la ushairi, Kwa upande mwingine matteru (1987), anasema kwamba tunzu za kinathari zinajumlisha tungo zote za fasihi simulizi zenye kutumia lugha ya kawaida. Matteru anamlizia kwa kusema kuwa "nathari" hujumlisha tanzu na fani kama hadithi, ngano, tarihi, visasili, vigano, masimulizi.

**MASIMULIZI / HADITHI**

Tanzu mbalimbali za hadithi zinaingia hapa, mfano ngano, hekaya n.k. simulio la kihistoria na la kiasili kama vile VISAKALE (Masimulizi ya kimapokeo/wahenga/ mashujaa), kumbukumbu, VISASILI (hadithi za zamani zenye kuwakilisha imani na mtazamo wa jamii).

Hadithi au masimulizi ambayo yanatumia lugha ya mjazo au nathari pia mtiririko wake huwa mwepesi na sahihi. Zipo hadithi za kubuni na za kihistoria.

**UMUHIMU WA HADITHI KATIKA FASIHI SIMULIZI**

i. Hutumiwa kuipa jamii mwelekeo. Simulizi au hadithi hufumbata mtazamo wa jamii pamoja na falsafa yake nzima na ndiyo kielezi cha jamii husika.

ii. Hutumiwa kuyaendeleza maadili ambayo huwa kama nguzo kuu ya wanajamii. Kila hadithi huwa na funzo maalum.

iii. Huonya, huadhibu, huelimisha, huishauri na kuinasihi jamii kupitia wasifu wa wahusika.

iv. Simulizi au hadithi hutumika kuirithisha jamii elimu thamani na amali muhimu kutoka kizazi hadi kizazi. Tanzu za fasihi simulizi huwa nyezo kuu ya kurithisha elimu ya jadi katika jamii husika.

v. Hutumiwa kama burudani

vi. Hutumiwa kuendeleza uhusiano uliopo kati ya wanajamii na hasa uhusiano wa kushirikiana tofauti na usomaji wa vitabu.

vii. Hukuza uwezo wa watoto kuyakumbuka mambo. Huboresha uwezo wao wa kumbukumbu n.k.

**KUHAKIKI KAZI ZA FASIHI SIMULIZI**

**Sifa kuu za kimtindo zinazotumika katika uhakiki wa hadithi / simulizi ni:-**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

## i. DHAMIRA NA MAUDHUI

Ndani ya dhamira tunapaswa kulitambua wazo kuu au lengo kuu la hadithi ni jumla ya mambo yaliyomo ndani ya hadithi hiyo, yanayoibuka katika kuuendeleza wazo hilo kuu.

## ii. MSUKO

Huu ni muundo wa hadithi yenyewe, Hapa tunaangalia jinsi matukio ya hadithi yalivyopangwa kuanzia mwanzo kwenye kitangulizi. Mvuto wa hadithi ambao mgogoro kati ya wahusika waliopo. Kuwepo kwa taharuki, harakati zao hadi kwenye kilele cha hadithi au upeo na hatimaye mwisho wake.

## iii. USISIMUZI

Hapa tunachunguza uwezo wa hadithi wa kuweza kuiteka hadhira yake.

## iv. URUDIAJI

Kwa kawaida urudiaji unaweza kuwa wa vipengele vya muundo, mfano: virai, maneno, sentensi, vifungu fulani, nyimbo n.k. pia huwepo urudiaji wa mawazo, fikra, maoni n.k . Sababu za urudiaji huwa ni kufanya mambo yaliyozungumzwa kukumbukia au kusisitiza jambo fulani.

## v. MATUMIZI YA NYIMBO

**Nyimbo hutumika kwa kiasi kikubwa katika hadithi na kufanya kazi zifuatazo:-**

- Kuonyesha au kusisitiza kiini au wazo kuu katika hadithi au simulizi inayohusika.
- Hushirikisha hadhira katika hadithi inayotambwa.
- Huongeza uhai wa usimulizi kwa kushirikisha hadhira.
- Huwapambanua wahusika mbalimbali wanaopatikana katika hadithi hiyo.
- Kuondoa ukinaifu unaotokana na kuutumia mtindo wa aina moja kwa kipindi kirefu.
- Kuwazindua wasikilizaji ambao huenda wakawa wamelala au kusinzia wakati hadithi inatambwa.
- Hutumika kama kiliwazo katika hadithi za kitanzi

## vi. VILIWAZO / UCHESHI

Ni sehemu ya hadithi ambayo huwa imekusudiwa kuituliza hadhira kidogo hasa kwenye hadithi zinazozungumzia masuala ya kusikitisha au ya kitanzia, Kiliwazo kinaweza kuwa kifungu kilichojaa ucheshi kilichokusudiwa kuondoa kwa muda ile hali ya kusikitisha. Nyimbo hutumiwa pia kama kiliwazo.

## vii. TAMATHALI ZA SEMI

Hadithi huwa na ufundi wa kisanaa ambao hujitokeza kwa matumizi ya lugha yenye mvuto na iliyochanganya matumizi ya tamathali mbalimbali za semi. Mfano sitiari, tashibiha, tashititi, tashihisi, tafsida n.k

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. **USIMULIZI – HAKIKI / TUNDUIZI**

Mtambaji wa hadithi hutoa maoni kuhusu hadithi anayoisimulia. Msimulizi anaweza kutoa maoni yake kuwahusu wahusika wanopatikana hadithini au kuyahusu matukio fulani yaliyoko hadithini, kwa kiasi fulani huweza kuathiri usimulizi huu.

**ix. WAHUSIKA**

Kuna wahusika wa aina mbili katika hadithi. Wahusika binadamu na wahusika wanyama ambao wanapewa sifa za binadamu (mazimwi, majitu n.k.)

Katika usimulizi wa hadithi, mpaka ulipo kati ya ulimwengu wa kawaida wa binadamu na wanyama hufutwa.

Binadamu wanoweza kulingana, kujadiliana, kuzungumza na kuhusiana kwa jumla na wanyama. Katika hadithi simulizi wanyama wakubwa huweza kushindwa na wanyama wadogo. Hii ni namna ya kuwakejeli wasiotumia akili zao. Viumbe wakubwa wa kudhaniwa kama mazimwi majitu husawiri kama viumbe wanaoongozwa na tamaa kubwa, ulafi na uovu ulikithiri. Hii ni njia mojawapo ya kuziakisi sifa ambazo zinaonekana mbaya katika jamii.

Aidha kuna hadhira za aina mbili hadhira tendi na hadhira tuli. Hadhira tendi hushiriki katika usimulizi wa hadithi mfano katika nyimbo kupiga makofi, kucheza, kuitikia, kubadilisha wasimuliaji, kuuliza, kujibu maswali na kucheza. Hadhira tuli yenyewe huwa haishiriki kwa namna yoyote ile inasikiliza tu.

**x. TANAKALI SAUTI**

Mtambaji katika utambaji wake huweza kutumia sauti ambazo zinaeleza hisia au kuchora picha ya kutokea kwa jambo fulani.

Pia hutumiwa kutia utamu, mvuto na msisimko wa lugha ya mtambaji, mfano mara cheche akatwaa zumavi akapiga, kanga pia singizia moto ,ti,ti,ti......., nikamtwaa nikamfungafunga na majani ya mgomba nikampiga pu, pu, pu,...

**xi. ISHARA NA TASWIRA**

Ishara ni matumizi ya vitu Fulani kuvisimamia vingine yaani huashiria vitu vingine tofauti.

Mfano:- mti mkubwa kuashiria uhusiano uliopo kati ya watu na miungu katika jamii kadhaa.

Taswira ni matumizi ya lugha ambayo inamfanya msikilizaji au hadhira iweze kuunda picha akilini. Mtumiaji anaweza kutumia picha au tamathali za semi. Mfano sitiari kuunda picha hizi.

**xii. UTOKAJI KANDO**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Ni mbinu ambayo mtambaji au msimulizi anatoka kando ya utambaji wake na kutoa maoni kuhusiana na  kitu kisichohusiana na hadithi moja kwa moja.

Kuna utokaji kando wa nje ambao unatokana na sababu zilizo nje ya hadithi yenyewe, mfano kutokana na hadhira

Utokaji kando ambao inasababishwa na nia ya kutoa maoni kuhusu tukio fulani au kitu Fulani katika hadithi yenyewe mfano kutokana na hadhira.

Utokaji kando ambao unasababishwa na nia ya kutoa maoni kuhusu tukio fulani au kitu fulani katika hadithi yenyewe. Huu ni utokaji kando wa ndani. Hii inahusiana na usimulizi tunduzi.

**MAIGIZO(DRAMA ) SANAA ZA MAONESHO**

Maigizo yanatumia watendaji kuiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine ili kuburudisha na kutoa ujumbe fulani. Ni sanaa inayopatikana katika makabila.

Drama za kiafrika huambatana na ngoma, utambaji, hadithi, nyimbo na matendo ya kimila (jando na unyago), kuna maigizo yanayofungamana na michezo ya watoto, matanga, uwindaji, kilimo n.k.

**MAIGIZO YA WATOTO**

Watoto wanapocheza hufanya maigizo ya matendo ya kimaisha wanayoyaona katika jamii zao mfano kulima, kufanya biashara, harusi, matanga n.k. hizi ni sanaa za maonesho zenye kuwaburudisha na kuwaelimisha watoto licha ya kukuza vipaji vyao vya ubunifu.

**MAIGIZO YA MSIBANI**

Katika baadhi ya makabila, watani au wajukuu wa marehemu hupaswa kufanya maigizo yanayohusiana na maisha, matendo au tabia za marehemu. Hii huwapunguzia wafiwa huzuni yao mbali na kutoa mafunzo fulani kwa watu waliopo msibani, Mfano tabia mbaya, maigizo hayo hupinga tabia mbaya.

**MAIGIZO YA SHEREHE**

Sherehe  kuu za jamii ni kama vile kuzaliwa kwa mtoto, mtoto kupewa jina, jando na unyago, harusi, kubadilisha rika, kuanua matanga, sherehe za kisiasa (mfano kutawazwa kwa mtemi), sherehe za kidini (mfano kuwakaribisha mwezi mwandamo) n.k. kila sherehe huwa na sanaa zake za maonesho ambazo wakati mwingine huambatana na maigizo.

**MAIGIZO YA KIDINI**

Maigizo hayo hufanywa wakati wa ibada, matambiko na shughuli nyingine za kidini katika maigizo ya aina hiyo mzimu au miungu huwa ndiyo hadhira ya igizo linalofanyika.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Uigizaji ni muhuimu sana katika fasihi simulizi katika uigizaji huu watendaji huiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine ili kutoa ujumbe fulani. Uigizaji huu unaweza kuwa na nia ya kukejeli, kudhihaki, kukosoa au hata kuwaburudisha. Uigizaji hautegemei sauti tu bali pia maliba mahususi kama majusoo au Barakoa (maski) pamoja matendo yasiyoambatana na sauti kama michezo bubu ambayo inatilia mkazo mkubwa kwenye matendo.

Utambwaji wa hadithi unawasilishwa kwa hadhira kwa utendaji wa kisimulizi/ kitambwaji mashairi ni uigizaji au dhana ya aina Fulani.

Mvinga ni sherehe za kiutamaduni na huweza kuhusisha matambiko, miviga hufumbata maigizo ya aina fulani kutegemea sherehe inayohusika.

**VITANZU AU VIPERA VYA MAIGIZO AU DRAMA**

**i. MICHEZO YA JUKWAANI**

Hapa pana mpangilio na mazungumzo baina ya watu na matendo yao, mazungumzo hayo hujenga kisa ambacho kinaonesha mgogoro fulani, kuna aina ya michezo inayoambatana na sauti na isiyoambatana na sauti kama vile ucheshi bubu, michezo bubu n.k.

Onyesho bubu, Kimsingi vitanzu hivi huhusisha utendaji ambao unategemea matumizi ya ishara za mikono na sehemu nyingine za mwili pasipokuwa na maneno.

**ii. MAJIGAMBO**

Haya ni maigizo ambayo yanaonesha kujitapa (yaani kujigamba) kwingi kwa mtu ambaye labda ni shujaa au ambaye ametenda mambo ya kishujaa au yenye uzito fulani. Wahusika wanaopatikana katika majigambo ndiyo watambaji au wasimuliaji wa majigambo yenyewe. Ni kawaida ya majigambo kuwa na lugha nzito iliyojaa tamathali yenye taswira au picha za undani na yenye nia na mawazo mazito.

**iii. VICHEKESHO**

Ni mpangilio wa maneno ambayo yanawasilisha ujumbe fulani maalum kwa njia ya kuchekesha au kufurahisha. Kimuundo vichekesho huwa vifupi na havihitaji uchambuzi mpevu au wa ndani ili kupata maana nyingine ya ndani. Lugha yake huweza kuwa nyepesi na iliyojaa picha ambazo watazamaji wana uwezo wa kuzitambua.

**iv. NGONJERA AU USHAIRI WA KIMASEMEZANO**

Ngonjera ni mpangilio wa tungo za kishairi za kujibizana. Ili ushairi huu uwe sehemu ya majibizano lazima uambatane na utendaji yaani wanaohusika wanaotumia ishara za mikono, mwili, ishara za uso na nyingine ili kuwasilisha ujumbe wao. Ikiwa ngonjera haziambatani na matendo au utendaji haziwi tena sehemu ya maigizo bali sehemu ya ushairi. Mshairi mmoja anaweza kutongoa au kutunga ubeti na kutenda matendo yanayoambatana na kiini cha ubeti

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

wako, ngonjera, huweza kutumiwa kuwatia watazamaji au hadhira hamasa ya kutenda jambo au hata kuwasilisha maarifa fulani kwao.....

### v. MAZUNGUMZO

Mazungumzo ni maongezi ya kimajibizano yanayotokea baina ya watu wawili au zaidi kigezo kikuu cha kuyafanya yawe ya kifasihi ni kuwapo kwa usanii na ufundi katika muundo wake na jinsi yanavyowasilisha ujumbe wake. Hapo juu tumeona mazungumzo ni sehemu muhimu ya michezo ya jukwaani lakini yanaweza pia kuangaliwa kivyake.

Katika jamii nyingi mazungumzo hupatikana kwa njia mbalimbali. Njia kuu za kimisingi ni kuwako kwa hotuba, malumbano kati ya watani, ulumbi au usemaji wa kiufundi wa wanajamii tofauti na pamoja na mawaidha. Hivi ni vipengele vyepesi kueleweka kwa sababu vimeenea katika jamii nyingi.

## VIPERA VYA TANZU YA HADITHI KATIKA FASIHI SIMULIZI

### 1. NGANO

Hizi ni hadithi za kimapokeo zinazotumia wahusika kama vile wanyama, majoka, binadamu, mawe, miti n.k.

Fanani wa ngano hutumia maneno ya kuvuta hadhira kwa vile huanza na PAUKWA...... ambapo hadhira hujibu PAKAWA. Fanani huanza kusimulia hadithi yake baada ya utangulizi ambao huwavutia, huwachangamsha na kuwafanya waache kazi nyingine au kusinzia na kusikiliza ngano hiyo.

Mtambaji wa ngano wakati akiendelea kuhadithia anaweza kuuliza hadhira yake kama "niendelee? au nisiendelee? Kauli hiyo huwafanya hadhira wasisimke na kuuitikia kwa sauti" ENDELEA!!!. Ngano hufuata muundo rahisi na wa moja kwa moja. Kwa kawaida lengo kuu la ngano ni hadithi ya kuwaasa watoto ndiyo maana humalizia kwa kuwatia moyo kama vile wakaishi kwa raha mstarehe, wakazaa na kuzaa, maisha yakawa mazuri, amani ikatawale n.k.

### ii. TARIHI(VISAKALE)

Hizi ni hadithi ambazo husimuliwa kutokana na matukio ya kihistoria. Matukio hayo yanaundwa kisanaa ili kuvutia watu katika jamii. Tarihi inahusu matukio yanayoweza kuwa ya furaha au huzuni na ni ya kusisimua ili kuwakumbusha watu walikotoka. Fanani wa tarihi mara nyingi pia huanza kusema "paukwa"na hadhira kuitikia "pakawa". Kuna baadhi ya masimulizi ya tahiri ambayo huanza kwa nyimbo au majigambo ambayo huwafanya wasikilizaji kuwa makini na matukio yanayosimuliwa. Mara nyingi wahusika wa tarihi ni binadamu ambao hupewa uwezo mkubwa au mdogo mno ili kuyakinisha matukio yanayozungumziwa na kuyawekea mantiki. Tahiri anaweza kusimulia kuhusu historia ya mfalme, koo za kitawala, kumbukumbu za kutokea kwa ukoo Fulani, magonjwa, vita, njaa.

### 1. VISASILI

Hizi ni hadithi za kale zenye kuwakilisha imani na mtazamo wa jamii inayohusu asili ya ulimwengu na mwenendo wake, kuhusu asili yao wenyewe, maana na shabaha ya maisha yao. Hadithi hizi husimulia mambo yanayohusiana na maumbile ya watu, wanyama, miti na vitu visivyo na uhai.

Wahusika wa visasili ambao si binadamu hupewa hadhi na uwezo wa binadamu. Kwa mfano hadithi inayohadithiwa chanzo cha chura kuwa na mabakamabaka, au jongoo kuwa na mwili ung'aao na mwororo ni kisasili. Visalili husimulia mianzo au asili ya matendo ya kufkirika, imani au mtazamo fulani katika jamii usimulizi wa visasili pia huambatana na nyimbo.

iv**. VIGANO**

Ni hadithi fupi zinasimuliwa kwa lengo la kuelezea makosa au uovu wa watu fulani na kutoa maadili yanayofaa. Hadithi hizi hutumia sana nahau na methali katika kutoa maadili kwa hadhira iliyokusudiwa. Maadili hayo hutolewa kama kielelezo wakati wa maongezi au kumkanya mtu.

Wahusika katika vigano ni wanadamu hata wanyama, kwa kawaida vigano hujengwa juu ya tukio moja ambalo hutumiwa kuelezea juu ya maisha halisi katika jamii husika. Mara nyingi vigano havienei sana kwa jamii kwa sababu hutumiwa na muktadha wa mazungumzo.

**TAMTHILIYA**

**TAMTHILIYA NI NINI?**

Tamthiliya au drama ni fani iliyokusudiwa kutendwa jukwaani kwa ajili ya hadhira fulani, hivyo kwa lugha ya kawaida, tamthiliya huitwa mchezo wa kuigiza. Kwa kawaida tamthiliya huwa na masimulizi ambayo huigizwa na wahusika wa pande mbili au zaidi zinazogongana.

Mgongano huo husababisha mgogoro ambapo unaposuluhishwa na kutanzuliwa, mchezo huwa umemalizika. Tamthiliya ni sanaa ya maneno. Hivyo ina sifa za kawaida za sanaa za maonesho ambazo ni:-

Dhana inayotendeka, watendaji, hadhira, kusudio la kisanaa, uwanja/jukwaa, muktadha wa kisanaa, ubunifu/ umathilishaji,

**Tofauti kati ya tamthiliya na sanaa nyingine za maonesho inaelezwa na mlama kama ifuatavyo:-**

"Tamthiliya ni aina moja wapo ya sanaa za maonyesho ambazo usanii wa utendaji wa utendaji wake hutegemea zaidi, MATENDO na UONGEAJI, tofauti na aina nyingine kama ngoma ambazo hutegemea zaidi uchezaji ngoma na upigaji muziki. Tamthiliya ni ule utungo ambao unaweza kuwa umeandikwa au haukuandikwa ambao unaliweka wazo linalotoka kuwasilishwa katika umbo la tukio la kuliwezesha kutendeka mbele ya hadhira".

Kwa mujibu wa maelezo hayo kitu kikubwa kinachoipambanua tamthiliya na sanaa nyingine za maonesho kama vile ngoma, ni msisitizo wake kwenye VITENDO na MAZUNGUMZO YA

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

WAHUSIKA islilahi ya tamthiliya inatokana na neno "mithali" ambalo lina maana ya mfano au ishara ya kitu fulani".

Hivyo kaitika tamthilia ya kitu kimoja humathilishwa au huwasilishwa na kitu kingnine mathalani katika mchezo wa KINJEKITILE, mwigizaji wa sehemu ya KINJEKITILE huwakilisha muhusika aitwae KINJEKITILE katika mchezo na mhusika huyo wa mchezo huwasilishwa kwa kiasi Fulani KINJEKITILE wa historia.

## AINA ZA TAMTHILIYA

### Zipo aina nyingi za tamthiliya kama ifuatavyo:-

1. **TANZIA**

Tamthiliya ya kijadi ya ulaya ilikuwa na Matawi mawili makuu, TANZIA na KOMEDIA. Tanzia ni tamthiliya ya majonzi kuhusu anguko la mhusika mkuu. Anguko au kifo hicho huweza kusababiswa na udhaifu wake binafsi wa kitabia, kosa fulani alilofanya au mazingira fulani yaliyomzidi uwezo au mchanganyiko wa baadhi ya sababu hizo kwa mfano anguko la kinjekitile na matokeo ya kosa lake binafsi (kuwafanya watu kuyaamini zaidi maji) na mazingira ya kihistoria ( kisiasa na kijamii ambayo hana uwezo nayo)

2. **KOMEDI / RAMSA**

Komedi au ramsa ni kinyume cha tanzia. Hii ni tamthiliya inayoishia katika furaha. Mhusika mkuu wa tamthiliya hupambana na matatizo ya kila aina kiasi cha kukaribia kushindwa lakini hatimaye hushinda na kufanikiwa katika malengo yake. Tamthiliya Shakespeare, mabepari wa venisi, shida ni ramsa.

Komedi hupendwa sana na vijana hata watu wazima kwani huwa na mvuto na ucheshi na huweza kuelimisha bila kuleta majonzi au kukatisha tamaa zipo pia tamthilia ambazo zinachanganya sifa za tanzia na komedi.

3. **VICHEKESHO**

Vichekesho ni aina ya tamthiliya gezwa au faraguzi (zinazotungwa hapo kwa hapo bila kuandikwa), tamthilya hizi ziliaza miaka ya 1920 kwa lengo la kuburudisha wakazi wa mijini, wakati wa mapumziko.Tamthiliya hizo kwa kawaida zilikuwa na vituko vya kuchekesha na viliwasuta watu waliofikiriwa kuwa WASHAMBA, WAJINGA na WASIOSTAARABIKA.

Hivyo mara nyingi tamthiliya hizo zilimuonyesha mhusika anayetoka shamba na kuja kuzuzuka mjini. Vichekesho viliendelea na hata baada ya uhuru bado vipo ila dhamira zake zilibadilika, Baadhi ya vichekesho siku hizi huigizwa radioni, kwenye televisheni kwenye vilabu vya pombe.

4. **MICHEZO BUBU**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hii ni aina ya tamthiliya isiyotumia maneno, waigizaji hutumia ishara na vitendo tu, na hadhira hujua kinachotokea kwa kuzisoma ishara hizo. Tamthiliya hizi hufaa sana katika jamii zenye mchangnyiko wa watu wasiozungumza lugha moja. Zikiandaliwa vizuri na kuchanganywa na sauti za muziki au ngoma huvutia sana.

5. **DRAMA NGANO**

Zipo drama ngao za aina mbili, kwanza ni zile tamthiliya gezwa ambazo watoto au watu wazima huzibuni kutokana na ngano zetu za kiafrika. Ngano au hadithi simulizi huigizwa jukwaani kama drama badala ya kutambwa au kusimuliwa tu. Hii ni njia  nzuri sana ya kupata michezo ya vijana shuleni. Watoto wenyewe huweza kuitunga  na kuiigiza michezo hiyo kwa kuwa ngano nyingi huhusu wanyama (kwa kujipamba maleba, sauti n.k) ili kuwaigiza wahusika wanaowapenda ( kwa mfano sungura) siku hizi televisheni za ulaya zinatumia sana mbinu hii hususani katika filamu za vikatuni na vikaragosi/wanasesere (puppets).

Aina ya pili ya drama – ngano ni tamthiliya ya kimajaribio zinazojaribu kuigiza fani za jadi za kiafrika katika umbo la tamthiliya za kizungu. Katika tamthilia hizo huweza kuwepo mtambaji ambaye huanza kwa kusema PAUKWA na mwitikiaji akajibu PAKAWA kisha mchezo huendelea kwa njia ya masimulizi na maigizo, mifano mizuri ni tamthiliya za E.Hussein za JOGOO KIJIJINI na NGAO ZA JADI" na tamthiliya za Penina Mhando za "LINA UBANI" na "NGUZO MAMA".

6. **DRAMA – NGOMA**

Drama- ngoma ni maigizo yanayoambatana na kufungamana na uchezaji wa ngoma (dansi) hadithi ya drama huigizwa kwa miondoko ya ngoma na nyimbo badala ya masimulizi na mazungumzo ya wahusika. Hii ni fani inayokubaliana sana na sanaa za maonesho za kiafrika na kwa vyovyote huweza kuwavutia na kuwasisimua watoto. Aidha hutoa nafasi kwa hadhira yenyewe kushiriki katika igizo badala ya kuwa watazamaji tu.

7. **MICHEZO YA REDIO.**

Michezo ya redio ni tamthiliya zinazotegemea sauti zaidi ya macho hivyo zinahitaji mbinu maalum za kuvutia sikio ili zifanikiwe .Hadhira huwasikiliza waigizaji wanapoongea na husikia sauti au vishindo vya mambo yanayotendeka lakini huwaoni watu hao au kuyashuhudia matukio hayo .Njia hii ya maigizo huweza kuwafikia watu wengi katika eneo kubwa.

8. **MICHEZO YA SINEMA, RUNINGA**

Hizi ni aina ya tamthiliya za kisasa zilizokusudiwa kuoneshwa katika sinema au televisheni kwa hadhira pana . Utunzi wa tamthiliya hizi unahitaji ufundi maalum, kwani uhitaji maelekezo mengi kuhusu jukwaa, mandhari, na matendo ya wahusika. Mazungumuzo ya wahusika huwa ni machache kuliko ilivyo katika mchezo wa redio au katika tamthiliya ya kawaida.

9. **TAMTHILIYA GEZWA /FARAGUZI (IMPROVISED DRAMA)**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Hii ni michezo inayoandaliwa bila ya kuandikwa. Waigizaji hujitungia maneno yao papo kwa papo wakati wa onesho. Njia hii hufaa sana vijijini na shuleni hupunguza sana matatizo ya ukosefu wa tamthilia zilizoandikwa. Aidha huwa hakuna lazima ya kukariri, watoto / vijana wenyewe kujitungia michezo yao na kuigiza bila ya msaada wa mtu mzima. Hii ni njia nzuri ya kupata tamthiliya nyingi za watoto na vijana. Hata hivyo tamthiliya hizi hudai ubunifu wa uwezo mkubwa wa lugha kutoka kwa waigizaji.


**VIJENZI VYA TAMTHILIYA**

**Kwa mujibu wa kanuni za ki-Aristotle, tamthiliya yoyote kwa kawaida huwa na vipengele vifuatavyo:-**

(i). hadithi (simulio) (ii) vitendo (iii) waigizaji wanaomathilisha wahusika wa hadhithi (iv) daiolojia (mazungumzo), Siku hizi daolojia yaweza kuwa ya maneno au ishara.

**(i) HADITHI(SIMULIO)**

Tamthiliya husimulia hadithi au kisa Fulani, Hadithi hiyo yaweza kuwa ni ya kubuni au tukio la kweli la kihistoria, au mchanganyiko wa yote mawili. Hadithi hiyo kwa kawaida kuhusu mzozo fulani unaohusisha pande mbili : upande wa mbabe (shujaa wa hadithi ) au nguli (mtendaji mkuu) na upande wa mpinzani wa mbabe/nguli. Hadithi hiyo husukwa kwa namna inayoujenga mgogoro wa pande hizo mbili hadi kufikia mwisho wake. Mtiririko wa matukio kwa kawaida huwa na umbo la piramidi lenye hatua.




**HATUA ‘’A’’ CHANZO.**

Katika hatua hii ndiyo huwa mwanzo au utangulizi wa mchezo. Katika hatua hii mambo yafuatayo hujitokeza:-

-Usuli wa mgogoro wa tamthiliya huelezwa .

-Hali ya tamthliya (ya majonzi, ya miujiza, ya nderemo) hudhihirishwa.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**(ii) VITENDO**

**KITENDO**

Tamthiliya hugawanyika katika sehemu kuu ziitwazo vitendo, Kila kitendo (act) huzingatia tendo kuu ndani ya mchezo, kwa mfano katika mpangilio wa matukio ulioelezwa hapo juu kila kipengele kingeweza kuwa kitendo kimoja. Hivyo tamthiliya yenye mpangilio huo kijadi ulitakiwa kuwa na vitendo vitano .katika tamthiliya ya kijunani kumalizika kwa kitendo kuliashiriwa na kuingia kwa wazumi (chorus) jukwaani. Siku hizi zipo tamthiliya zenye kitendo kimoja, vitendo viwili, vitatu, vitano, na hata zaidi.

**ONESHO**

Kila kitendo hugawanyika katika sehemu ndogo ziitwazo ‘’maonesho‘’, Onesho moja kwa kawaida huwasilisha tukio moja linalotendeka mahali pamoja, kwa kawaida onesho moja hutenganishwa na jingine kwa kuzingatia mantiki ya kile kinachosimuliwa, tukio moja likimalizika onesho nalo huwa linamalizika. Wakati wa maigizo, jukwaani mabadiliko ya maonesho huashiriwa kwa kufunga pazia au kuzima taa au kwa wahusika kuondoka jukwaani.

**(iii). WAHUSIKA NA WAIGIZAJI**

Usawiri wa wahusika wa tamhiliya hufanywa kwa njia ya matendo na mazungumzo, kwani fursa ya kutoa maelezo marefu haipo. Wahusika wa tamthiliya hawana tofauti kubwa na wahusika wa hadithi, huweza kuwa mviringo, bapa, watu wa tabaka la juu, wanyonge n.k. Tamthiliya huwa na wahusika wakuu na wahusika wadogo.

**-WAHUSIKA WAKUU**.

Mbabe /nguli: huyu ni shujaa wa tamthiliya ambaye matendo mengi yanahusu maisha na majaliwa yake kwa KINJEKITILE (E.Hussein 1969) ndiye mbabe au nguli (Prolagonist), yaani mhusika kiini au mtenzi mkuu.

Katika tanzia ya kijadi, mbabe aghalabu alikuwa mtu wa tabaka la juu ambaye kama tulivyokwisha elewa aliangamia kutokana na ama hila (dosari) fulani kwa tabia na maamuzi yake ama kwa sababu ya kusaka na mazingira yanayomzidi uwezo ama yote mawili wa mfalme Odipade .

Mkinzani (antagonist), Mhusika mkuu anayepambana na mbabe au nguli. Muwi (villain) mhusika muovu kwa mfano shyloak wa Shakespeare, mabepari wa venis.

**-WAHUSIKA WADOGO.**

Hawa aghalabu huwa ni wengi na baadhi yao huwa na jukumu dogo tu katika tamthiliya wahusika wadogo hutokea mara kwa mara ni:-

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**MFOILI**-Mhusika anayewekwa sambamba na nguli na aliye na sifa tofauti na za nguli kwa lengo la kuwa na kumpambanua nguli vizuri zaidi.

**MSIMULIZI**-huyu ni mhusika anaye tumiwa na mtu kutoa maelezo na ufafanuzi kuhusu matendo na matukio katika michezo. Katika baadhi ya michezo, Katika baadhi ya michezo mhusika huyu hupewa jina jingine kama mwimba.

**CHIZI (clown)** -Mhusika mcheshi ambaye hufanya vitu vya kipumbavu na kusema maneno ya kijingajinga ili kuiburudisha hadhira na wakati mwingine kutoa ujumbe fulani.

**WAIGIZAJI** - Waigizaji pengine huitwa wamathilisha ni watu wanaotokea jukwaani mahala pa wahusika wa mchezo na kwa vitendo na tabia za hao wahusika wamahilisha .waigizaji hawana budi kuteuliwa vizuri ili wawakilishe na kuwasilisha sawa sawa umbo, hali, hisia,tabia , mawazo, na matendo ya wanaomathilisha.

**(iv) DAIOLOJIA (MAZUNGUMZO YA WAHUSIKA)**

Hadithi ya tamthiliya husonga mbele kwa njia ya vitendo na mazungumzo ya wahusika. Mazungumzo ya wahusika ndio huitwa daiolojia, Mafanikio ya michezo mingi hutegemea namna mtunzi anavofaulu kuweka daiolojia inayovutia na kuaminika.

Daiolojia ni lazima iwe na maneno machache yaliyoteuliwa vizuri ili kuisogeza mbele hadithi au kudhihirisha jambo fulani alilokusudia mtunzi.

Baadhi ya tamthiliya huwa na monolojia pia, Katika monolojia mhusika huzungumza mwenyewe kudhihirisha mawazo aliyonayo moyoni. Zipo pia tamthiliya zinazotumia masimulizi ambapo hutokea masimulizi na kusimulia au kusimulia mambo yaliyotokea, mithili ya mtambaji wa hadhithi au utendi, Mbinu hii hutumika katika drama tendi. Baadhi ya tamthiliya za Kiswahili kwa mfano M.Mulokozi katika MKWAWA WA UHEHE zimetumia mbinu hizi.

**(v) MBINU NYINGINEZO**.

Mbinu nyinginezo zinatumiwa na watunzi wa tamthiliya zimekwisha elezwa, tamthiliya za Kiswahili, hasa zile zilizoandikwa zimeiga baadhi ya mbinu za kimagharibi. Nyingi zina muundo wa ki-Arislotle zinatumia daiolojia, zina vitendo, maonyesho na migogoro inayosuluhishwa mwishoni, Baadhi ya tamthiliya zimejaribu kuiga mbinu za Sanaa za maonyesho za jadi za kiafrika. Miongoni mwa wanamajaribio hao wa mwanzo ni Ebrahim Hussein. Mtunzi huyu alijaribu kutumia mbinu za utambaji wa ngano katika maigizo yake ya NGANO ZA JADI na JOGOO KIJIJINI. Mpaka sasa wataalamu hawajakubaliana kama tungo hizo mbili ziitwe tamthiliya au tendi .

Penina Mhando pia, katika tamthiliya zake za LINA UBANI na NGUZO MAMA, vilevile alijaribu kutumia utambaji wa ngano. Mbinu ya majigambo ilitumiwa na Mhando na wenzake katika ‘’HARAKATI ZA UKOMBOZI ‘’ na Mbogo katika ‘’SUNDIATA ‘’. Mbinu ya tendi simulizi ilitumiwa na mlokozi katika mkwawa wa uhehe.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Hii ni mifano ya baadhi ya mbinu ambazo watunzi wa tamthiliya wanaweza kutumia ili kuzifanya tungo zikaribiane zaidi na utamaduni wa wale waliowaandika.

**KUTUNGA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI.**
Dhana ya utungaji:
Kutunga ni kitendo cha kutoa mawazo ubongoni kisha kuyadhihirisha kwa kuyaandika au kuyasimulia.

**Hatua za Mwanzo za kuzingatia katika kutunga kazi za kifasihi**.
i). Kuwa na jambo ambalo unaona linasababisha au lina mvuto kwa jamii.Kisha unafanyia utafiti kujua chanzo chake na kwa nini linaendelea kuwepo.
ii).Baada ya utafiti ni kufanya maamuzi ya njia gani au tanzu gani aitumie kufikisha ujumbe kati ya ushairi , hadithi, semi na maigizo.
iii).Atumie kipera gani kutoa kutoka katika tanzu aliyochagua .Mfano kama ni ushairi atumie nyimbo au ngonjera.
iv).Kulijenga jambo jambo katika fani na maudhui ili kupata mbinu sahihi ya uwasilishaji wa kazi yako kwa hadhira.
v). Mtunzi kujikita hasa katika maudhui ya jambo lako unalotaka kuliwasilisha .Mfano nini dhamira yako.
vi).Mtunzi unaangalia namna ya kuwasilisha maudhui yako, hapa unashughulikia vipengele vya fani yaani muundo , mtindo ,mandhari ,wahusika na matumizi ya lugha.
Hapa mtunzi anatakiwa atumie ufundi na ubunifu wa hali ya juu ili kazi yake ielimishe na kusisimua.
vii).Baada ya fani na maudhui kushughulilkiwa mtunzi aangalie namna ya uwasilishaji wake.Kuangalia kanuni na taratibu za kipera ulichotumia.
viii).Mtunzi unaanza kuandika yale unayotaka kuelimisha jamii kwa kufuata taratibu za uandishi.
ix). Mtunzi unasoma kuangalia kama kile ulichokidhamiria ndicho ulichikitunga.
x).Fanya mazoezi namna ya kuwaslisha hiyo kazi.
Mfano:-
Namna ya kutunga igizo la kifasihi simulizi
i.Kwanza kuteua wahusika watakao sawiri matendo ya tabia zao:-
-Mhusika mkuu hujitokeza mara kwa mara na matendo mengi yanamuhusu yeye.
-Wahusika wadogo huwa wengi.
- -Kuteua waigizaji wazuri watakaofanya vizuri katika kuiwasilisha.
-Wahusika wajengwe kwa kuzingatia utendaji wao.
- ii.Kuteua lugha itakayotumika.
- iii.Kuteua mandhari nzuri katika uwasilishaji wake.
- iv.Kuangalia muundo na mtindo wa igizo lake.

---

# MATUMIZI YA SARUFI

**NADHARIA ZA SARUFI**

Dhana ya sarufi ya lugha imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali wa sarufi.

Mtaalamu James Salehe Mdee (1999) sarufi ya Kiswahili sekondari na vyuo anafafanua maana ya sarufi kuwa ni mfumo wa kanuni za lugha zinazomwezesha mzungumzaji kutunga sentensi sahihi na zenye kukubaliwa na wazawa wa lugha. Kanuni hizi hujitokeza katika lugha ya mzawa wa lugha inayohusika ambaye anaifahamu barabara lugha yake. Sarufi inajumuisha mfumo wa sauti maumbo ya maneno muundo na maana.

Mtaalamu Mbundo Msokile (1992) na khamisi (1978) wanasema sarufi ni mfumo wa taratibu na kanuni zinazotawala matumizi sahihi ya matamshi, maumbo ya maneno, miundo ya tungo na maanda ya miundo ya lugha. Ni mfumo wa taratibu zinazomwezesha mzungumzaji wa lugha kutoa tungo sahihi na pia inamwezesha mtu yeyote anayezungumza kuelewa tungo zinazotolewa na mtu mwingine anayetuma lugha hiyo hiyo.

F. Nkwera (1978) anasema sarufi ni utaratibu wa kanuni zinazomwezesha mzawa au mtumiaji yeyote wa lugha kuelewa tungo zinazotolewa na mtu mwengine anayetunza lugha hiyo hiyo. Kufafanua nakuzielewa kwa undani tungo mbalimbali zitumikazo katika lugha hiyo pamoja na kutoa tungo sahihi na zinazoeleweka

**HITIMISHO**

Kwa ujumla maana zote zilizotolewa na wataalamu wote ni maana sahihi za sarufi ila tunaweza kuhitimisha kwa sarufi ni kanuni, sheria au taratibu zinazotawala lugha katika viwango yote vya uchambuzi wa lugha yaani kiwango cha sarufi matamshi (fonolojia) sarufi maumbo (mofolojia) sarufi miundo (sintaksia) na sarufi maana (semantiki)

**AINA ZA SARUFI**

Ujumla sarufi inaweza ikagawanywa katika aina kuu zifuatazo

**SARUFI MATAMSHI (UMBO SAUTI)**

Sauti katika lugha yaani jinsi ambavyo vitamkwa au sauti za lugha zinavyoungana ili kujenga maneno yanayokubalika katika lugha husika.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**N.B:** Sarufi matamshi hujishughulisha na uchambuzi wa sauti zilizomo katika lugha. Namna zinavyotamkwa, mahali zinapotamkwa na namna sauti hizo zinavyopangwa; ili kujenga maneno ya lugha Fulani.

Lugha mbili tofauti zinawezakuwa na sauti zinazofanana lakini zikatofautiana katika utaratibu wa kuzipanga sauti hizo. Kila lugha ina utaratibu wake wa mpangilio wa sauti ili kujenga ama mofimu, silabi au maneno. Sauti zitumikazo katika lugha zinaweza kugawanywa katika makundi mawili

i. Irabu, mfano a, e, i, o, u
ii. Kansonati, mfano k, g, ch, i, d

**FONIMU**

Fonimu ni kipashio kidogo kabisa cha kifonilojia ni kitamkwa cha msingi cha kifonolojia kinacho badili maana ya neno

Mfano: kata, Pata, Pata } k, p, na b

Paga, Tanda, Pata } p, t na g

K, P, B ni fonimu kwani ndio zinafanya maneno hayo kutofautiana kimaana.

T na g ni fonimu zinazofanya maneno haya kutofautiana kimaana.

Irabu na konsonanti zinapotumika katika luga huitwa alfabeti.

Irabu ni sauti za lugha ambazo hutamkwa bila kuwepo kwa kizuizi chochote kwenye mkondo wa hewa utokao mapafuni kwenda nje kupitia chemba ya kinywa na pua..

**SIFA ZA IRABU**

1. Irabu hutolewa kwa mrindimo wa ujenzi sauti

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

2. Irabu zinapotamkwa midomo ya mtamkaji huviringwa na kutandazwa

3. Utamkaji wa sauti hizi utegemea mkao wa ulimi katika chemba ya kinywa.

**KONSONANTI**

Ni sauti ambazo hutamkwa kwa kuzuia mkondo wa hewa katika sehemu mbalimbali kinywani hasa kwa kutumia ulimi.

i. Konsonanti ghuna: ni zile ambazo hutamkwa zikiwa na mrindimo mkubwa wa nyuzi sauti

ii. Konsonanti zisizosighuna(sighuna): ni zile ambazo hutamkwa zikiwa na mrindimo mdogo wa sauti

Katika Kiswahili sanifu, kuna konsonanti 23 na viyeyusho viwili hizo ni b, ch, d, dh, f, g gh, j, k, l,  m, n, h, ny, ng, p, r, s, sh, t, th, v, z.

**Na viyeyusha viwili ambavyo ni :**

**SILABI**

Ni kitamkwa au sehemu ya neno ambayo hutamkwa mara moja na kwa pamoja kama sehemu ya fungu moja la sauti.

**Silabi zinagawanyika katika makundi mawili**

i. Silabi funge
ii. Silabi humo

**i. SILABI FUNGE**

Ni silabi zinazoishia na konsonanti

**ii. SILABI HURU**


Ni kitamkwa katika lugha (sauti katika luhga)

**ALOFONI**

Ni  vitamkwa tofauti yaani sauti zinabadili maana ya neno. Mfano

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA




Bh na b ni alafoni zinazobadili maana ya neno

2. **SARUFI MAUMBO** ( mofolojia)

Sarufi maumbo hujishughulisha na namna maneno ya aina mbalimbali yanavyoundwa katika lugha. Maneno katika lugha hujengwa kwa kuunganisha vipengele vidogo vya maneno ambavyo hubeba dhana mbalimbali kama vile nafsi,wakati,wingi,umoja, uyakinishi na kauli mbalimbali n.k

Vipande hivi vidogo vya maneno vijengavyo neno hufahamika kama mofimu, katika kila lugha kuna utaratibu wake wa kuzipanga mofimu ili kujenga maneno yenye maana katika lugha husika. Kwa kawaida mofimu hupangwa kwa kufuata utaratibu maalumu utarabu huo hujengwa kama utaratibu wa mpangilio kwa kufuata kanuni na huo utaratibu wa mpangilio wa mofimu usipofuata maumbo ya maneno yasiyokuwa na maana yaani yaliyokataliwa na wazawa wa lugha husika. Utaratibu wa kuzipanga mofimu ili kuzalisha maneno yenye maana katika lugha husika hutuzalia kanuni maumbo kwa mfano katika lugha ya Kiswahili mofimu za umoja na wingi katika nomino huwekwa mwanzoni katika utaratibu huu haukubaliki katika luhga ya kiingereza, katika lugha ya kiingereza mofimu za umoja na wingi huwekwa mwishoni mwa nomino. Mfano

Boy – boys

Girl – girls

Idea – ideas

**N:B** Kwa ujumla sarufi maumbo (mofolojia) hujishughulisha na jinsi ambavyo mofimu mbalimbali zinavyoungana ili kujenga maneno yatumikayo katika lugha. kipashio cha msingi katika mofolojia ya lugha ni mofimu.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

3. **SARUFI MIZINGO/UMBO TUNGO (**Miundo maneno / sintaksia) uchunguzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa maneno hayo sintaksia huchunguza sheria au kanuni zinazofuatwa katika kuyapanga maneno ya lugha yaani mpangilio wa neno moja baada ya jingine kwa namna ambayo itayafanya maneno hayo yalete maana inayokubalika katika lugha inayohusika wakati mwingine mpangilio wa maneno unaweza ukawa sahihi yaani ulizounda utaratibu lakini ukazalisha tungo zisizo kuwa na maana hiyo zitakuza mpangilio wa maneno wenye kuleta maana.

**N:B** Katika lugha ya Kiswahili kanuni kubwa ya kisintaksiani ni ile inayosema, kila sentensi iliyo sahihi na yenye kukubalika kwa wazao wa lugha ya Kiswahili sharti iwe na muundo wakiima na kiarifu au kikundi nomino na kikundi kitenzi.

## 4. SARUFI MAANA (UMBO MAANA SEMANTIKI)

Tawi hili la sarufi huchunguza maana inayoonekana wazi na maana iliyofichika huchunguza muundo wa tungo ili kupata maana iliyofichika. Katika lugha kila neno tungo huwa na maana yake. Kwa mfano, mtoto amelalia uji. Neno amelalia kama lilivyotumika, Katika sentensi hii halina maana moja na hivyo kuifanya sentensi hiyo kuwa na maana zaidi ya moja, mara nyingi maana ya neno hutegemea matumizi ya neno katika muktadha Fulani.

**N.B.**: Lugha inaweza ikafanya kazi sawasawa ambazo taratibu na kanuni za lugha husika zimefutwa. Taratibu hizo ni zile zinazohusu matamshi, maumbo, muundo na maana. Taratibu hizi ndizo humwezesha mzawa au mtumiaji yeyote wa lugha kutoa tungo sahihi na zinazoeleweka kwa matumizi mengine ya lugha na kuelewa tungo zinazokataliwa na watumiaji wengine wanaotumia lugha hiyo hiyo.

## VIPASHIO VYA LUGHA

Lugha hujengwa na vipashio mbalimbali ambavyo vinatabia ya kujengana yaani vipashio vidogo huungana kujenga vipashio vikubwa zaidi.lugha ina vipashio vikuu vitano ambavyo ni

**Mofimu - Neno - Kirai – Kishazi – Sentensi**

Vipashio hivi wakati mwingine hufahamika kama tungo isipokuwa kipashio kidogo kwa vingine vyote katika lugha ni mofimu na kipashio kikubwa kuliko vingine vyote ni sentensi vipashio vyote katika lugha vina muundo maalum unaoonesha jinsi vinavyojenga vipashio

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

vikubwa kuliko vingine vyote ni sentensi, vipashio vyote katika lugha vina muundo maalumu unaonekana jinsi vinavyojengwa isipokuwa mofimu

**MOFIMU**

Mofimu ndio kipashio cha msingi kinachoshughulika katika mofolojia ya lugha kwa maana mbalimbali za mofimu. Baadhi ya wataalamu hujaza mofimu kwa kutumia kigezo cha muundo wa mofimu na wengine hufasili kwa kutumia kigezo cha kazi au dhima zinazobebwa na mofimu husika.

**MAANA YA MOFIMU**

Mofimu ni sehemu ya neno au neno zima lenye maana ya kisarufi au maana ya kileksika

**AU**

Mofimu ni kipashio kidogo cha kimofolojia chenye kubeba maana iliyo ya kisarufi au ya kileksika

Mofimu hupangwa kwa kuzingatia utaratibu maalumu ili kujenga maneno yenye maana utaratibu huo hufahamika kama kanuni. Utaratibu wa upangaji wa mofimu ukikiukwa huzalisha maumbo yasiyokubalika katika lugha husika.

**Mfano:** a – na – som – a neno hili linakubalika katika lugha kwa sababu mpangilio wake wa mofimu umezingatia kanuni lakini mpangilio wake ungekuwa vinginevyo husingekuwa na maana

**Mfano**: som – na – a –a tungezalisha umbo lisilokuwa na maana. Kila lugha inautaratibu wake wa kuzipanga mofimu

**N.B** Wakati mwingine mofimu huwa na maana sawa na neno, mofimu hizo huitwa mofimu huru au mofimu za kilekisika. Mofimu hizi husimama zenyewe bila kutegemea mofimu nyingine na huwa na maana kamili.

**AINA ZA MOFIMU**

Mofimu zinaweza zikagawanywa katika makundi mawili kwa misingi ya kikazi yaani mofimu za kileksika na mofimu zakisarufi. Pia zinaweza kugawanywa katika makundi mawili kwa msingi wa kimuundo na kupata mofimu huru na mofimu tegemezi.

1. **MOFIMU HURU** (Mofimu sabili/mofimu za kileksika)

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hizi ni mofimu ambazo husimama zenyewe zinaumbo dogo zaidi bila kupoteza maana. Aina hiyo ya mofimu hujitokeza katika aina mbali mbali za maneno;

Mfano baba, Mama, kaka, na winnie ni nomino

-chafu, bovu, fupi, zuri na tamu ni vivumishi.

-Hata, lakini, kama, mpaka, au- viunganishi

-Arifu, tafiti, samehe- vitenzi

Mofimu zote huru huwa na kazi ya kileksika

**2. MOFIMU TEGEMEZI**

Hizi ni mofimu ambazo haziwezi kusimama ili kukamilisha dhana iliyokusudiwa. Mofimu tegemezi hujumuisha mofimu awali, mzizi, na mofimu tamati.Mpangilio wa

mofimu hizo au mfungamano wa mofimu hizo huunda neno. Mofimu hutumika katika kuunda maneno

N.B Mofimu tegemezi zinapofungana huunda neno tegemezi, mfano: a – na - som – a anasoma, nam – pend – a – nampenda

Mofimu huru huunda neno huru mfano, Baba, mama starehe, jaribu n.k Mfungamano wa mofimu huru na mofimu tegemezi hujenga neno changamano. Mfano; mw – ana – nchi

Mw – ana – anga

**KUBAINISHA MOFIMU**

Kubainisha mofimu ni kuligawa neno katika mofimu zinazolijenga neno na kueleza kazi za kila mofimu ubabaishaji huo wa mofimu hufuata hatua zifuatazo

1. Kutambua aina ya neno – Yaani kama neno hilo ni tegemezi au neno changamano, Neno huru huundwa na mofimu huru na neno tegemezi huundwa na mofimu tegemezi na neno changamano huundwa na moja huru na mengine tegemezi

N: B Neno huru huwa halivunjwi vunjwi kwani huundwa na mofimu huru


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

2. Kulitenga neno na kulivunja vunja katika mofimu zinazojenga neno hilo yaani hujenga mofimu awali, mzizi na mofimu tamati.

   N: B Mofimu awali, mzizi na mofimu tamati hupatikana katika maneno tegemezi na maneno changamano


3. Kueleza kazi ya kila mofimu
   Mfano: Bainisha mofimu katika maneno yafuatayo
   Hatukupendi
   Hili ni neno tegemezi




   ii. 1- Mofimu awali kianzishi, nafsi ya kwanza wingi
   2 - Mofimu awali rejeshi kwa mtendwa
   3 - Mofimu awali rejeshi kwa mtenda
   4 - Mofimu mzizi
   5 - Mofimu tamati kanushi

6. Asiyekujua


   i. Hili ni neno tegemezi




   iii. 1. Mofimu awali nafsi ya tatu umoja
   2. Mofimu awali kanushi nafsi ya tatu umoja wakati uliopo
   3-Mofimu ya urejeshi kwa mtenda
   4-Mofimu awali ya urejeshi kwa mtendwa
   5-Mofimu mzizi
   6. Mofimu tamati

C. Kikikitangulia

i. Hili ni neno tegemezi




Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

ii 1. Mofimu awali nafsi ya tatu umoja

2. Mofimu awali kanushi ya nafsi ya tatu umoja wakati uliopo

3 Mofimu ya urejeshi kwa mtenda.
4. Mofimu mzizi


5. Mofimu tamati

5.

7.

**d. Nimejikata**

i. Hili ni neno tegemezi




ii 1 – Mofimu awali ya nafsi ya kwanza umoja

2 - Mofimu awali inayoonesha hali timilifu

3 – Mofimu awali ya urejeshi wa kujitendea
4 -Mofimu mzizi
5 -Mofimu tamati

**e. Sipendeki**

Hili ni neno tegemezi

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

-Si- pend - ek –i
1 2 3 4

1. - Si – mofimu awali kanushi nafsi ya kwanza umoja wakati uliopo.
2. - pend- mofimu mzizi
3. -ek- mofimu tamati ya kutendeka
4. -i- mofimu tamati ya ukanushi

**DHIMA ZA MOFIMU**

Mofimu huwa na dhima au kazi mbalimbali zinazotumika katika maneno.

**Kazi za mofimu ni kama zifuatazo:-**

1. Kuongeza msamiati katika lugha au kubadili maneno kutoka kategoria moja kwenda kategoria nyingine.

**Mfano:** Nyumba – Nyumbani

Soma – somo

Soma – msomi

Taifa - taifisha.

2. Kuongeza maana ya ziada au kupanua maana ya neno

**Mfano:** Taifa – Utaifa

3. Kudokeza dhana ya umoja na wingi

**Mfano:** Mtu – watu

iii. Ni majina yenye umbo la umoja lakini umbo la wingi hakuna

| **Mfano:** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| | Ukuta | Kuta |
| | U – Funguo | Funguo |
| | U-Kucha | Kucha |

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

| | |
|---|---|
| U-kope | kope |

iv. Ni maneno ambayo yana umbo dhahiri la wingi lakini umbo la umoja halipo

| **Mfano: Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ukuta | Kuta |
| U- Funguo | Funguo |
| U-Kucha | kucha |
| U-Kope | kope |

v. Ni nomino ambazo zina umbo dhahiri la wingi lakini umbo la umoja halipo

| **Mfano: Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Boga | Ma-boga |
| Jembe | ma-jembe |
| Debe | Ma-debe |
| Tako | Ma-tako |
| Panga | Ma-panga |

iv. Ni majina yanayokuwa na mofimu ya wingi wala umoja

| Mfano: **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Boga | ma – maboga |
| Debe | ma - debe |
| Tako | Ma-tako |
| Panga | Ma-panga |

v. Ni majina yanayokuwa na mofimu ya wingi wala umoja

| Mfano: **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Shule | Shule |
| Ng'ombe | Ng'ombe |
| Mbuzi | Mbuzi |
| Kuku | Kuku |

**N.B:** Mofimu kapa hujitokeza katika kundi la pili (2) na kundi la tatu (3) ambapo katika kundi la pili (2) katika umoja majina yana mofimu (2). Mofimu ya kwanza inaonesha umoja na mofu ya pili inaonesha mzizi wa neno.

Katika wingi mofu ya wingi ni kapa ambayo hufuatiwa na mofu ya pili inaonesha mzazi wa neno. Katika wingi mofu ya wingi ni kopa ambayo hufuatiwa na mofu mzizi na kuzifanya nomino hizo kuwa na mofu mbili. Mofu ya kwanza ni kapa ambayo hudokeza wingi na mofimu ya pili ni mzizi. Japokuwa mofu ya wingi ni kapa yaani haiandikwi wala kutamkwa athari yake ipo.

**DHIMA ZA MOFIMU**

**1.Kuonesha udogo wa kitu au ukubwa wa kitu**

Mfano: Kijiti-jiti

**Kuondoa upatanisho wa kisarufi ambao hutawaliwa na nomino ya kiima na kitenzi.**
Mfano: Kiti kimevunjika.
Utaratibu huu haufai.
Sheria hii haifai.

**Kudokeza nafsi mbalimbali**.
Mfano: ni....na....som....a-nafsi ya kwanza umoja.
Tu....na....som....a-nafsi ya pili umoja
U-na-som-a- nafsi ya pili wingi
A-na-som-a- nafsi ya tatu umoja
wa-na-som-a- nafsi ya tatu wingi.

**4. Kudokea njeo/wakati**
Mfano: Atakuja- Wakati ujao
Atakapokuja- Wakati uliopo timilifu.
Amekuja- Wakati uliopita timilifu.
Alikuja- Wakati uliopita.

**5.Kudokeza hali mbalimbali katika tungo**.
Mfano: Hucheza- Hali ya mazoea.
Akija- Hali ya masharti.
Angekuja

**6.Kudokeza urejeshi kwa mtenda mtendwa mtendwa kujitenda au tendo kwa mtenda.**
Mfano: Aliyenipiga- Inaturejesha kwa mtenda.
Aliyenipiga- Inaturejesha kwa mtenda.
Aliyesomea-Inaturejesha kwa mtendewa
Nimejikata- Inarejesha tendo kwa mtenda (kujitenda)

**7.Kuonesha ukanushi.**
Mfano: Hakuja
Sisomi

8. Mofimu hudokeza kauli mbalimbali
Mfano: Kauli ya kutendwa- Pigw-pig-w-a

Kauli ya kutendewa-pig-iw-a

Kauli ya kutendea-pig-i-a

Kauli ya kutenda-pig-a

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kauli ya kutendeana-pig-an-a

Kauli ya kutendeshwa-pig-ian-a

Kauli ya kufungamanisha-gandamana

Kauli ya kutendwa-choma-chomoa
-funga-fungua

Kauli ya kutendaka-fumba- fumbata
-ambaa-ambata

4. **Kuonesha udogo wa kitu au ukubwa wa kitu**

Mfano: Kijiti – jiti

5. **Kuondoa upatanisho wa kisarufi ambao hutawaliwa na nomino ya kiima na kitenzi**

Mfano: Kiti kimevunjika.

Utaratibu huu haufai.

Sheria hii haifai.

6. **Kudokeza nafsi mbalimbali**

**Mfano:** ni ......na.... som ....a – nafsi ya kwanza umoja

Tu... na...som...a-------------nafsi ya pili umoja

U-na-som-a -------------- nafsi ya pili wingi

A-na-so-a------------------- nafsi ya tatu umoja

wa – na—som—a-----------nafsi ya tatu wingi

7. **Kudokeza njeo/wakati**

**Mfano:** Atakuja – Wakati ujao

Atakapokuja – Wakati uliopo timilifu

Amekuja - Wakati uliopita timilifu

Alikuja - wakati uliopita

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

8. Kudokeza hali mbalimbali katika tungo

Mfano: Hucheza – hali ya mazoea

Akija – Hali ya masharti

Angekuja

9. **Kudokeza urejeshi kwa mtenda mtendwa mtendwa jujitenda au tendo kwa mtenda**

Mfano: Aliyenipiga – Inaturejesha kwa mtenda

Aliyenipiga – Inaturejesha kwa mtendwa

Aliyesomea - inaturejesha kwa mtendewa

Nimejikata – inarejesha tendo kwa mtenda (kujitenda)

10. **Kuonesha ukanushi**

Mfano: Hakuja

Sisomi

11. **Mofimu hudokeza kauli mbalimbali**

Mfano: Kauli ya kutendwa – Pigwa - Pig- w-a

Kauli ya kutendewa pig-iw –a

Kauli ya kutendea- pig –i – a

Kauli ya kutenda –Pig –a

Kauli ya kutendeana – Pig – an –a

Kauli ya kutendeshwa – pig-ian –a

Kauli ya kufungamanisha - gandamana

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Kauli ya kutendwa - choma - chomoa

-Funga - fungua

Kauli ya kutendaka - fumba - fumbata

Ambaa – ambata

**ALOMOFU**

Alomofu ni maumbo zaidi ya moja au maumbo tofauti ambayo huwakilisha mofimu moja kisanji ambayo hufanya kazi moja kisaruji alomaju hutokea mazingira maalum baadhi ya mazingira hutabirika mengine hayatabiriki kabisa. Alomofina kwa kawaida kubadili maana ya neno.

**UTOKEAJI WA ALOMOFU**

1. **Mazingira ya kifonolojia (matamshi**)

Kwa kutumia utawala au mazingira tunaweza kupata mofimu na alama yake kwa vitenzi vya lugha ya Kiswahili vinaponyumbuliwa huzalisha kauli mbalimbali, kauli hizo hudhihirika kutokana na kuwepo kwa mofimu mahususi zinazoonesha kauli husika.

**Kauli ya kutendewa**

Kauli hii inahusisha tendo ambalo hutendwa na muhusika Fulani kwa niaba ya wahusika mwingine. Maumbo ambayo huonesha kauli hiyo ya kutendwa ni (-iw-) (-ew-) na (-liw-) na (-lew-). Mambo haya hufahamika kama alomofu na utokeaji wake hutegemea athari za kimatamshi za kitenzi husika

Mfano: Lima - Lim – iw –a

Suka - suk – iw – a

Cheza – chez – ew –a

Paka - pak – iw – a

Soma – som – ew –a

Kimbia – kimb – liw –a

Tafiti – tafit – iw –a

Zoa – zo – l-ew –a

Chomoa – chomo – lew –a

**Mofimu ya kauli ya kutendewa ina alomofu tano ambazo ni**

(-iw-) hii hutokea ikiwa mzizi wa kitenzi unaishia na konsonanti na mzizi huo una irabu a,e,I,o,u.

- (ew-) hii hutokea ikiwa mzizi wa kitenzi unaishia na konsonanti na mzizi huo unairabu e au o
- (-liw-) hutokea ikiwa mzizi wakitenzi unaishia na irabu i, a , au u
- (-lew-) hutokea ikiwa mzizi wa kitenzi unaishia na irabu a au e
- (-w-) hutokea kama mzizi wa kitenzi unaishia na irabu- i -lakini kwa vitenzi vya kuchukua yaani visivyokuwa na asili ya kibantu.

2. **Mazingira ya kileksika**

Kwa kutumia mazingira ya kileksika alomofu zinaweza kutokea katika ngeli za majina kwa mfano katika ngeli ya kwanza na y apili yaani m/w inaweza kuona alomofu ageli ya kwanzakama ifuatavyo:-

| **NGELI II** | **NGELI 1** |
|---|---|
| Wa –tu | M-tu |
| Wa-ke | M-ke |
| Wa-nafunzi | Mw-anafunzi |
| Wa-elevu | Mw-elevu |
| Wa-wezeshaji | Mw-ezeshaji |
| Wa-imbaji | Mw-imbaji |
| Wa-ongozaji | Mw-ongozaji |
| Wa-uguzi | Mu-uguzi |
| Wa-umbaji | Mu-mbaji |

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Katika ngeli ya kwanza mofimu m –inaonesha umoja .katika ngeli hiyo ya kwanza ambayo kiwakilishi chake ni mofimu m- kuna maumbo matatu ambayo hufanya kazi ya kuonesha umoja katika ngeli- I- maumbo hayo ni;

Kwa hiyo ngeli ya I ina alomofu tatu alomofu ni (m-) (mw-) (-mu-)

- Alomofu (m-) hutokea inapofuatwa na konsonanti
- Alomofu (m-) hutokea inapofuata  na irabi a, e, i, o
- Alomofu, (mu-) hutokea inapofuatwa na irabu- w

3. **Mazingira ya kisarufi**

Kwa kutumia mazingira ya kisarufi tunaweza kupata mofimu na alomofu zake hasa katika mofimu njeo.  Mofimu rejea inawakilishwa na maumbo yafuatayo.

a-li – soma

a-me – soma

a-na-soma
a-     Ta- soma

Mofimu njeo inaolomofu nne alomofu hizo ni  (-li-) (-me-) (-na-) na (-ta-)

- Alomofu (-li-) na (-ta-)
- Alomofu (-me-) hutokea kuonesha wakati uliopita  timilifu
- Alomofu (-na-) hutokea kuonesha wakati uliopo
- Alomofu (-ta-) hutokea kuonesha wakati ujao.

**N.B**: ingwa alomofu ni maumbo yanayotofautiana hufanya kazi moja kisarufi. Maumbo hayo hutokea katika mazingira maalumu ambayo yanaweza yakatabirika au yasitabirike kabisa mazingira hayo yanaweza kuwa ya kifonolojia au mazingira ya kileksika na mazingira ya kisarufi.

**VIAMBISHI**

Baadhi ya watu huchanganya dhana ya viambishi na dhana ya mofimu. Lakini ukweli ni kwamba mofimu na viambishi ni dhana  mbili tofauti zenye mabwiano Fulani pia. Kwa  ujumla viambishi vyote ni mofimu   na mofimu zote ni viambishi

**SWALI: VIAMBISHI NI NINI?**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Viambishi ni mofimu zinazoandikwa kwenye mizizi wa neno ili kukamilisha muundo wa neno husika. Katika lugha ya Kiswahili viambishi vinaweza kuandikwa kabla ya mzizi wa neno na baada ya mzizi wa neno.

kwa hiyo katika lugha ya kiswahili viambishi hutokea kabla ya mzizi wa neno na baada ya mzizi wa neno

**AINA ZA VIAMBISHI**

**Lugha ya Kiswahili ina viambishi vya aina mbili**

1. **VIAMBISHI AWALI/TANGULIZI**

Hivi ni viambishi ambavyo hutokea mwanzoni mwa mzizi wa neno na huwa ni vya aina mbalimbali

**A.Viambishi idadi /ngeli**

Viambishi hivi hupatikana mwanzoni mwa majina vivumishi kwa lengo la kuonesha idadi yaani wingi na umoja, Mfano :

M – cheshi    wa –zuri

M – tu    wa - tu

Ki – ti    vi-ti

m- ti    mi - ti

**N:B** Wakati mwingine katika majina na vivumishi huweza kuandikwa, viambishi ambavyo hudokeza ukubwa wa nomino na vivumishi. Hivyo wakati mwingine majina na vivumishi huandikwa viambishi ambavyo hudondokea udogo wa majina na vivumishi.

Mfano: ji – tu    ma – jitu

Ju –mba    ma – jumba

Ki - toto    vitoto

Ki –vulana    vi – vulana

Ki – zuri    vi – zuri

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**B. Viambishi awali vya ukanushi**

Viambishi vya ukanushi kwa kawaida huwekwa mwanzoni mwa vitenzi ili kukanusha vitenzi husika. Viambishi ambavyo huandikwa katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili ili kuonesha ukanushi wa tendo ni viambishi,

“Si” “ha” na “bu”

Kiambishi “ha” hutumika kukanzisha kitenzi kilichofanywa na nafsi ya kwanza wingi nafsi ya pili wingi na nafsi ya tatu katika umoja na wingi. Katika nafsi ya pili hutumika alomofu “ku” ambayo hukanusha nafsi ya pili umoja

**Mfano:** ni - na --- imba ---si ---imbi

U – na – imba – hu – imbi

Tu - na –imba --- ha –tu --- imbi

m- na – imba – ha -- mu--- imbi

wa ---na – imba --- ha ---wa –imbi

C**. Viambishi vipatanishi / nafsi**

Hivi ni viambishi ambavyo huwekwa kabla ya mzizi wa kitenzi na kubadilika kutegemeana na aina ya neno linalopatanishwa na kitenzi husika, kazi ya viambishi hivi ni kuonesha nafsi. Mfano;

Ni – nasoma tunasoma

A - nasoma m – mnasoma

U- nasoma wa – nasoma

1. **Viambishi vya njeo /wakati**

Kiambishi cha njeo ni kiambishi ambacho huwekwa katika kitenzi ili kuwakilisha muda ambapo tendo husika limetendeka. Mfano tendo kama limefanyika wakati uliopita huwakilishwa na kiambishi (-li-) katika uyakinishi na kiambishi (-ku) tendo hilo linapokanushwa

| | |
|---|---|
| Ni- li—soma | Si – ku - soma |
| U – li- soma | hu – ku - soma |
| A – li- soma | ha – ku-soma |
| Tu – li – soma | hatu-ku-soma |
| M-li – soma | ham-ku-soma |
| Wa – li- soma | hawa-ku-soma |

1. **Viambishi vya hali**

Hivi ni viambishi ambavyo huwekwa kabla ya mzizi ambavyo hutumika kuonesha muda au kipindi maalum ambao tendo, lilifanyika viambishi vya hali hueleza kama tendo linaendelea kufanyika kama hufanyika mara kwa mara kama limemalizika kufanyika

1. **Hali ya kuendelea kwa tendo**

Hali ya kuendelea kwa tendo huwakilishwa na kiambishi (-na-) ambacho huwekwa kabla ya mzizi wa kitenzi

Mfano ni - na – imba

Tu – na-imba

U-na-imba

M-na-imba

A-na-imba

Wa-na-imba

1. **Hali timilifu**

Hali hii huwakilishwa na kiambishi"me" katika uyakinishi na kiambishi "ja" katika ukanushi. Mfano:

| | |
|---|---|
| Ni – na-soma | Si – ja- soma |
| Tu-me-soma | hatu-ja-soma |
| M-me-soma | ham-ja-soma |
| A-me-soma | ha-ja-soma |
| Wa-me-soma | hawa – ja-soma |

1. **Hali ya mazoea**

Hali ya mazoea huwakilishwa na kiambishi (-hu-)

Mfano: hu – soma

hu – imba

hu –cheza

hu – cheza

hu- lala

1. **Hali ya masharti**

Hali ya masharti huwakilishwa na viambishi (-ki-) (-nge-)

Mfano: kiambishi (-ki-) hudokeza uwezekano

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Tu- Ki-shinda – tukishinda tutafurahi

A-ki-ja – akija nitamwambia

Kiambishi (-nge-) hudokeza matumaini kidogo

A-nge-nilipa-Juma pesa yangu ningenunua gari.

Kiambishi (-ngali-) hudokeza kutokua na matumaini yeyote au kuwepo kwa matumaini kidogo kuliko yale yanayodokezwa na kiambishi (-nge-); mfano ningalijua kua nitafeli mtihani ningalisoma kwa bidii.

1. **Viambishi vya mtenda**

Hivi ni viambishi ambavyo hurejesha tendo kwa nomino ya mtenda, viambishi hivi hutegemea aina ya nomino inayorejeshewa

Mfano: ali – ye – piga

Uli-o-vuna

Vili-vyo-anguka

**g.Viambishi vya urejeshi kwa mtendwa (yambwa)**

Hivi ni viambishi ambavyo hurejesha tendo kwa nomino ya mtendwa wa jambo

Mfano: ali – ye-pigwa

Ali – o- vunjwa

Vili – vyo – angushwa

**h**. Viambishi virejeshi kwa mtendewa (kiambishi yambiwa)

Hivi ni viambishi ambavyo hurejesha tendo kwa nomino ya mtendwa jambo

Mfano: ali – ye-somewa

1. **Viambishi vya urejeshi wa kujitendea**

Hivi ni viambishi ambavyo hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi na huwakilishwa na kiambishi (-ji-) ya kujitendea ambavyo hutumika katika umoja na wingi na pia katika uyakinishi na ukanushi

**Mfano:**

| | |
|---|---|
| nili – ji-somea | siku – ji- somea |
| Nime- ji-kata | sija-ji-kata |
| Nina-ji-somea | si – ji-somei |
| Ana-ji-somea | ha-ji-somei |
| Una-ji-somea | ha-ji-somei |
| Tun-ji-somea | hatu-ji-somei |
| Tuta-ji-somea | hatuta-ji-somea |
| Mta-ji-somea | hamta-ji-somea |
| Wali-ji-somea | hawaku-ji-somea |

2. **VIAMBISHI KATI**

Viambishi kati ni viambishi ambavyo hupachikwa ndani ya mzizi wa neno na hivyo kuukata mzizi katika sehemu kuu mbili (2)

**N.B;** Viambishi kati huwepo katika lugha ya Kiswahili kwa sababu maneno ya lugha ya Kiswahili kwa tabia yake hawaruhusu upachikaji wa viambishi kati ya mzizi, viambishi hivi hutokea katika lugha nyingine mfano kiebrania.

3. **VIAMBISHI TAMATI**

Hivi ni viambishi ambavyo huiweka baada ya mzizi wa neno. Navyo ni vya aina kuu mbili (2)

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(a) Viambishi tamati maana

(b) Viambishi tamati vijenzi

1. **Viambishi tamati maana**

Viambishi tamati maana ni viambishi ambavyo hukamilisha maana ya neno. Viambishi hivi huwa haviadhiri maana ya awali ya neno yaani havijengi dhana mpya katika neno

Mfano: a-na-som-a

Tend –a

Kata –a

Kat –a

1. **Viambishi tamati vijenzi**

Hivi ni viambishi ambavyo hujitokeza mwishoni mwa mzizi wa neno ili kujenga dhana mpya

Mfano: piga – pig -o

Mcheza – Mcheza-ji

Soma – som -a

Viambishi tamati hufanya kazi mbalimbali kama vile kudokeza kauli mbalimbali za vitenzi

**i. Kauli ya kutenda**

Hii ni kauli ambayo hueleza jambo lililotendwa na mtenda. Viambishi ambavyo hubainisha kauli ya kutenda ni viambishi tamati maana ambavyo huwa ni vimalizio vya mzizi wa kitenzi

Mfano gand – a

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Pig – a

Som –a

**ii.Kauli ya kutendwa**

Kauli hii hueleza kuwa mtu, watu au vitu Fulani vimetendwa jambo Fulani, Alomofu ambazo huwakilisha kauli ya kutendwa ni (-wa) (-liw) (-lew-)

Mfano: pig – w-a

Sem – w-a

Chom- w-a

O – lew – a

Vu – liw – a

Ambi – w-a

**iii.Kauli ya kutendewa**

Kauli hii huonesha kuwa mtu Fulani ametenda kwa niaba ya mtu mwingine, Alomofu ambazo hutumiwa kuonesha kauli ya kutendewa ni (-iw-), (ew-) (-liw-) (-lew-)

Mfano: lim – iw-a

Chez-ew-a

Som-ew-a

Kimbi-liw-a

Zo-lew-a

Va-liw-a

Chomo-lew-a

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**IV. Kauli ya kutendea**

Kauli hii huonesha kuwa tendo limefanyika kwa manufaa, kwa niaba au kwa faida ya mtu mwingine alomofu za kauli ya kutendea ni (i) (-e-) (-li-) (-)

Mfano: pig – i-a

Lal – i-a

Ruk-i-a

Chez-e-a

Zo-le-a

o-le-a

**V. Kauli ya kutendesha**

Kauli hii huonesha wababaishaji ambao huwezakuwa na mhusika au wahusika Fulani wanaosababisha kufanyika kwa tendo la mhusika na wahusika wengine. Kauli hii huonesha mtu fulani wanavyosababisha kufanyika kwa tendo kwa mhusika na wahusika wengine. Kauli hii huonesha mtu Fulani anamsababishia mtu mwingine kufanya jambo Fulani za utendaji (-ish) (esh-) (-lish) (-lesh-) (sh) na (-z)

**Mfano** : imb – ish –a

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kimbi – z –a

Tembe – z-a

Pit – ish –a

ru – sh –a

**VI. kauli ya kutendesha (usababishaji**)

Ni kauli ya wasababishi ambao huwezakuwa ama mhusika au wahusika Fulani wanaosababisha kufanyika kwa tendo kwa mhusika au wahusika wengine. Kauli hii huonesha mtu fulani ana msababisha mtu mwingine kufanya jambo Fulani.

Og – esh –a

Zo-lesh-a

Ka-lish – a

Va-lish-a

Shon-esh-a

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Som-esh-a

Chem-sh -a

**Vii. Kauli ya kutendana**

Kauli hii huonesha wahusika Fulani kuhusika na tendo Fulani ambapo mhusika wa kwanza anamtenda mhusika wa pili, lakini pia mhusika wa pili ana mtendea mhusika wa kwanza katika jambo hilo hilo.

Adhari ya tendo linalofanyika huwa kwa pande zote mbili yaani mtu wa kwanza na mtu wa pili. Kauli hii hudhihirishwa na kiambishi (-an-) ambacho hutokea baada ya mzizi wa kitenzi.

Mfano: pend – an-a

Suk – an –a

Sukum – an –a

Sem – an – a

Ruki – an –a

**Viii. Kauli ya kutendeana**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kauli hii huhusisha tendo linalofanywa na watu wawili ambapo mhusika wa kwanza anafanya tendo Fulani wka mambo ya mhusika wa pili na muhusika wa pili anafanya tendo hilo hilo kwa niaba ya muhusika wa kwanza. Kiambishi kinachodhihirisha kauli hii ni (-an-) ambayo hutokea kati ya kiambishi kinachofuata baada ya mzizi wa kitenzi na kiambishi tamati maana

Mfano: suk – i – an –a

Sem-e-an-a

Som-e-an –a

Zo-le-an-a

Va-li-an-a

O-le-an-a

**ix. Kauli ya kutendana (kufungamana)**

Hili ni kauli ambayo hurejelea hali, ambapo watu au kitu hukaa pamoja kwa muda mrefu. Mofimu ya kauli hii katika lugha ya Kiswahili ni (-am-) ambayo hujitokeza katika vitenzi vichache

Ung – am-a

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Ach – am –a

**x. Kauli ya kutendwa**

Hi ni kauli ambayo huonesha kinyume cha tendo. Na kauli hii hudhihirishwa na kiambishi (-o) na (-u-)

Mfano: umb – u –a

Teg – u – a

Chom – o –a

Kunj – u-a

Pang – u –a

**Xi Kauli ya kutendana (kishikanishi)**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hii ni kauli inayoonesha mshikamano yaani tendo la kufanya watu au vitu kushikana na mofimu inayodhihirisha kauli hi ni (-at-)

Mfano:Pak-at-a

Kam-at-a

Fumb – at – a

**SHINA NA MZIZI**

Mzizi /kiini ni sehemu ya neno inayobakia baada ya kuondoa aina zote za viambishi yaani viambishi vya awali vyote na viambishi tamati vyote.

Mzizi ni sehemu ya muhimu ambayo hubeba maana ya msingi katika neno

**AINA YA MZIZI**

Kuna aina kuu mbili (2) za mzizi

1. **Mzizi fungo/tegemezi**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Huu ni mzizi ambao hauwezi kujitegemea yaani huwezikusimama peke yake kama neno na kuleta maana

Mfano: som — a

Chom – a

Pend -a

(a) (chom-), ( som) na (pend-) ni mzizi tegemezi ambayo haiwezi kusimama yenyewe bila kuleta maana

2. **Mzizi huru/sahihi**

Huu ni mzizi ambao unaweza kusimama peke yake kama neno na kuleta maana.

Mfano: Jembe

Ng'ombe

Winnie

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Marcus

Abel

Concepta

**Shina ni nini?**

Shina ni sehemu ya neno (mzizi asilimia waneno) ambayo hufungamanishwana irabu mwishoni isiyokuwa na maana maalum kisaruji

| | | |
|---|---|---|
| **Mfano:** | **Neno** | **shina** |
| | Mtoto | toto |
| | Wanacheza | Cheza |

**AINA ZA MASHINA**

1. **Shina sahili /huru**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hili ni shina ambalo huundwa na mofimu moja tu ambayo pia huwa ni mzizi wa neno. Mfano ng'ombe, kuni, tafiti

2. **Shina changamano**

Ni shina ambalo huundwa na mzizi pamoja na kiambisi mwishoni, Mfano cheza soma, na kimbia.

3. **Shina ambatani/ ambatana**

Hili ni shina ambalo linaundwa na mofimu mbili ambazo zote huwa ni mzizi

Mfano: mwana + nchi

Pima + Maji

**NB:** Katika lugha ya Kiswahili wakati mwingine hulingana na mzizi na mofimu. Kulingana kwa dhana hizo hakuna maana kwamba dhana hizo ni sawa.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**DHANA YA MOFU**

**Dhana ya mofu inafafanuliwa na wataalamu mbalimbali wa sarufi kama ifuatavyo;**

Mtaalamu (Nick 1949) anafafanua mofu kuwa ni umbo la neno ambalo huwakilisha mofimu na ambalo hudhihirika kifonolojia na kiothografia.

Mofimu ambazo elementi dhahania, huwakilishwa na mofu ambazo hudhihirika kifanolojia zikiwa na sauti za kutamkwa, au kiothografia zikiwa ni alama za kuandikwa.

**TUKI (1990)** wanafafanua kuwa mofu ni kipashio cha kimofolojia kiwakilichasho mofimu

**marealle (1978)** anafafanua kuwa mofu ni vipande vya neno ambavyo husitiri mofimu. Kila mofu inamaana Fulani, Vipande hivyo vya maneno huwa na maana maalum katika kila neno hutegemeana na jinsi lilivyotumia.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**N.B:** Kutokana na maana hizo tatu za mofu tunapata mambo ya msingi kabisa ambayo hutumika kupambanua na dhana ya mofu. Pia kutokana na maana hizi tatu tunapata sifa za msingi zinazotumika kupambanua dhana ya mofu.

## SIFA ZA MOFU

1. **Mofu ni sehemu halisi ya neno**

Mofu ni maumbo halisi ya maneno ambayo hutamkwa na watu wanapozungumza au kuandikwa, Kwa hiyo mofu ni umbo halisi ambalo linaweza kusikika linapotamkwa na linaweza kuonekana kwa macho ijapokua limeandikwa.

2. **Mofu hudhihirika kifonolojia na kiathografia**

Mofu ni umbo halisi la neno na kwa kuwani ni umbo halisi la neno basi mofu hudhihirika kifonolojia zinapotamkwa na kimaandishi zinapoandikwa.

3. **Mofu huwakilisha maana**

Kila mofu huwakilisha maana Fulani, Neno lolote lile katika lugha yoyote ile litakuwa na maana,

Maana hiyo huwa imesitiriwa katika mofu zinazolijenga neno hilo.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hii ina maana kuwa kila neno lenye maana Fulani lazima maana hiyo itakuwa imewakilishwa na mofu Fulani. Pia hakuna neno lolote katika lugha yoyote ambalo litakauwa ni neno lenye maana bila kuwa na mofu angalau moja.

4. **Mofu ni kipashio kidogo kabisa cha neno**

Mofu ndiyo sehemu ndogo kabisa katika neno ambayo hubeba maana na sehemu hiyo haiwezi kugawanyika katika sehemu ndogo zaidi zilizo na maana. Mofu ni umbo ambalo ni kubwa kuliko fonimu lakini ni dogo katika neno.

**N.B:** Lakini katika lugha ya Kiswahili wakati mwingine mofu hulingana na neno. Mofu ni vile viambishi mbalimbali ambavyo huwa vinawekwa kwenye mzizi wa neno pamoja na mzizi wenyewe. Kila kiambishi cha neno pamoja na mzizi wenyewe.Kila kiambishi cha neno ni mofu na mzizi wa neno pia ni mofu. **Mfano:**

Mofu huainishwa kwa kutumia vigezo vikuu viwili

1. Kigezo cha maana yaani maana zinazowakilishwa mofu
2. Kigezo cha mofolojia ya mofu

Kwa kutumia kigezo cha maana kuna aina tatu (3) za mofu

1. Mofu huru
2. Mofu funge
3. Mofu tata

Kwa kutumia kigezo cha mofolojia kuna aina kuu tatu (3) za mofu

1. Mofu changamano
2. Mofu funge
3. Mofu tata

Kwa kutumia kigezo cha mofolojia kuna aina kuu tatu (3) za mofu

1. Mofu changamano
2. Mofu mzizi
3. Mofu kopa

1. **MOFU HURU**

Mofu huru ni mofu ambazo zinaweza kukaa zenyewe kama maneno yenye maana inayoeleweka bila kusaidiwa na mofu nyingine,

Mfano: Nomino (kaka) (paka) sungura)

Vivumishi (safi) (udhaifu)(hodari) Imara) Zuri

Vielezi ((Haraka) (Juzi) Leo

Vitenzi (afiti) Samohe) Ariful)

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Viunganishi (halafu) (pia) (ila)

## II. MOFU FUNGE

Hizi ni mofu ambazo haziwezi kutumika peke yake kama neno kamili bali hutumika kama kiambishi ambacho huambatana na mofu nyingine ili kukamilisha neno

Mofu funge inasifa mahususi

1. Haiwezi kusimama peke yake ikajitegemea kwa kawaida
2. Kwa kawaida mofu funge ni mofu tegemezi hivyo ni lazima iambatane na angalau mofu nyingine moja ili iweze kujitosheleza kimaana. Baadhi ya wanaisimu huiita mofu tegemezi
3. Maana ya mofu funge hutegemea muktadha wa mofu kimahusiano na mofu nyingine. Mofu tegemezi kazi zake huwa zimefungwa kwenye muktadha maalumu na zinapoondolewa kwenye muktadha huo hukosa maana na ni vigumu kujua bila kuweka katika muktadha wa neno.

Mfano; Kula – (ku) + (l) + (a)

Kunjwa – (ku) (nyw) + (a)

Mpe – (m) + (pe)

Sikusoma – (si) + (ku) + (som) +(a)

Mofu hizi ni mofu tegemezi kwa sababu haziwi wazi kusimama zenyewe

**III. MOFU TATA**

Hizi ni mofu ambazo huwa na maana zaidi ya moja na hivyo husababisha tungo kueleweka kwa namna zaidi ya moja

Mfano: Juma alimpiga John mpira

1. Juma alimpiga mpira kwa kuelekezakwa John
2. Juma alitumia mpira kama kifaa cha kumpigia Johari
3. Juma alipiga mpira kwa niaba ya John
4. Juma alimpiga John kwa sababu ya mpira

Maana hizi nne zimesababishwa na mofimu tata (-i-) Ambayo inajitokezakatika sentensi alimpigia

**IV MOFU CHANGAMANO**

Hizi ni mofu ambazo huundwa angalau na mashina au mizizi miwili ya neno ambayo katika mazingira na kila mmoja hujitegemea,

**Mfano**: Kiona mbali Mofolojia ya neno hili ina uweo kutazamwa kwa namna kuu mbili

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. **Namna ya kwanza: linaweza kutazamwa kama neno lenye mofu tatu (3)**

(ki-) + (on-) + (-a-) + (mbali)

1. **Linaweza kutazamwa kama neno lenye mofu tatu (3)**

(ki-) + (-on-) + (-mbali-)

(ki-) + (-onambali)

Katika neno kuona mbali kuna mizizi miwili, linaweza kutazamwa kama neno moja lenye mzizi mmoja

(-onambali) hii ni mofu changamano kwa sababu huundwa na mizizi miwili ambayo katika mazingira mengine inaweza kutenganishwa na kila mzizi kujitenga enyewe.

**V. MOFU KAPA**

Hizi ni mofu za kipekee ambazo hazina umbo hazitamkwi tunapozungumza wala haziandikiwi tunapoandika, wala hazionekani kabisa katika neno lakini athari za nafuu hizo huwa miongoni mwa wazungumzaji.

**NB:** Ingawa mofu kapa hazitamkwi wala kuandikwa, hazisikiki wala kuonekan kwa macho lakini maana zake huwa zipo na tunazipata zinapotumika katika maneno ; kwa mfano tukichunguza maumbo ya umoja na wingi katika majina ya Kiswahili, Majina hayo yanaweza yakagawanywa katika makundi mawili (2)

1. Ni majina yenye maumbo dhahiri ya umoja na wingi

Mfano m – pira mi – pira

m-ti mi –ti

ki – ti vi – ti

**ALOMOFU**.

Alomofu ni maumbo zaidi au maumbo tofauti ambayo huwakilisha mofimu moja kisarufi ambayo hufanya kazi moja kisarufi, alomofu hutokea mazingira maalum baadhi ya mazingira hutabirika mengine hayatabiriki kabisa. Alomofu kwa kawaida hubadili maana ya neno.

**UTOKEAJI WA ALOMOFU**

Mazingira ya kifonolojia (matamshi)

**Mfano:** Mtu anaposikia neno "funguo" anajua ni zaidi ya moja.

**vi. MOFU MZIZI**

Mofu mzizi ni kiini cha neno. Mofu mzizi ndio hubeba maana ya msingi katika neno. Mofu huwa haibadiliki neno linapoandikwa mofu nyingine

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Mfano;(u) +(Funguo) na (wa) + (toto)

Funguo na toto ni mofu mzizi

**N:B** Uainishaji wa aina hizo za mofu huzingatia maana zinawakilishwa na mofu na kigezo kwa kigezo cha kimofolojia.

**TUNGO**

Neno tungo hutokana na kitenzi tunga, Wanasema hufasiri kuwa tungo ni matokeo ya kuweka na kupanga pamoja vipashio vidogo ili kujenga vipashio vikubwa zaidi katika lugha. Katika sarufi tungo ndogo kuliko tungo nyingine za neno ambalo huundwa kutokana na kuwekwa pamoja mofimu kuwa tungo kubwa kuliko nyingine zote ni tungo.

**AINA ZA TUNGO**

Katika lugha ya Kiswahili kuna aina kuu nne za tungo ambazo huainishaji wake au mpangilio wake unazingatia hali ya tungo. Tungo hizo hupangwa kuanzia tungo ndogo hadi kubwa zaidi,

1. Tungo neno ambayo hujengwa na mofimu
2. Tungo kirai ambayo hujengwa na maneno
3. Tungo kishazi ambayo hujengwa na maneno au kirai
4. Tungo sentensi ambayo hujengwa na tungo kirai au kishazi

**1. TUNGO NENO**

Neno ni mkusanyiko wa silabi , au silabi hutamkwa au huandikiwa na kuleta maana

**Mfano:** Ng'ombe

Tafiti

Anatembea

Taifa

**N:B** : Neno hujengwa na mofimu moja au zaidi, Neno linalojengwa na mofimu moja huitwa neno sahili au huru na neno linalojengwa na mofimi zaidi

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

ya moja huitwa neno changamoto. Maneno mengi katika lugha ya Kiswahili ni changamana,

**AINA ZA MANENO**

Wataalamu wa lugha ya Kiswahili wanatofautiana katika uainishaji wa aina za maneno. Wapo ambao wanaainisha aina saba (7) tu za maneno katika lugha ya Kiswahili na wengine huainisha aina nane (8) za aina za maneno. Wataalamu wanoainisha aina saba za maneno F. Mkwera (1978), Kapinga (1983) TUMI (1988) Mohamed (1986), Msamba na wanzake (1999) Kihore na wenzake (2001) wataalamu wengine wameainisha aina nane za maneno. MbundaMsokile (1992), J.S Mdee (1988), Ngullu R. (1999), Y. Rubanza (2003), MBadu (2000)

Wataalamu wanaoainisha aina nane za maneno hutofautisha dhana ya kiunganishi na kihisishi lakini wale wanaoainisha aina saba za maneno huona kuwa dhana hizo ni dhana mbili zinazofanana.

## 1. NOMINO /MAJINA (N)

Majina ni aina ya maneno ambayo hutaja vitu, viumbe, hali au matendo ili kuviainisha na kuvitofautisha na vitu vingine.

Mfano: Winnie, Werevu, Wema, Lulu, Mtu, Ubungo, Mungu na n.k

**AINA ZA MAJINA**

**a.Majina ya kawaida**

Majina haya yanataja viumbe kama vile wanyama, miti, watu, ndege, wadudu.

Majina yote hayo yanapoandikwa huanza kwa herufi ndogo kama yanatokea katikati ya sentensi au tungo.

**N:B** Majina hayo sio maalumu kwa vitu Fulani tu bali kwa vitu mbalimbali.

**b. Majina ya Pekee.**

Haya ni majina maalumu kwa watu au mahali ambaye huonesha upekee kwa watu,mahali au vitu, Majina haya hujumuisha majina binafsi ya watu na majina ya mahali.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mfano: Marcus, Halima, James, Abel, Fredy, Anna Ubungo, Manzese, Tanzania, Uingereza, Africa

**N: B** Majina hayo yanapoandikwa huanza kwa herufi kubwa

## C. **Majina ya jamii.**

Haya ni majina ambayo yanataja vitu au watu wakiwa katika makundi au mafungu japo huwa majina hayo yapo katika hali ya umoja. Mfano, Chama , kamati, kadamnasi, timu

## d. Majina dhahania

Haya ni majina yanayotaja dhana zinazofikirika zisizonekana kwa macho wala kushika

**Mfano:**Afya, utajiri, upole ukatili, Mungu, shetani, malaika, Majina yote hao yanapandikwa yapo ambayo huanzia herufi kubwa hata kama huandikwa katikati ya sentensi

## e. Majina ya wingi

Haya ni majina ambayo yanadokeza dhana ya wingi japokuwa majina haya hayana umoja wala umbo la majina haya hufanana na majina yaliyopo kwa wingi ingawa mfanano huo hauwiani moja kwa moja na majina ya wingi, Majina hayo umoja na wingi wake hudhihirika kutokana na upatanishi kisarufi uliopo baina ya majina hayo na vitendo

Mfano: wa majina hayo ni kama vile maziwa,mazungumzo, marashi, maji, mafuta manukato, madhehebu.

**N:B** Majina haya huwa hayana umoja wala wingi japokuwa baadhi ya wazungumzaji huwa wanalazimisha. Dhana ya wingi huwa inadhihirishwa na upatanishi wa kisarufi

**Mfano:** Maziwa yameharibika

Maziwa mengi yameharibika
Mafuta yamemwagika
Mafuta mengi yamemwagika

## II. KIWAKILISHI (W) Kibadala /vijina)

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Huwa ni maneno ambayo hutumika badala ya jina au ni maneno ambayo huwakilisha jina. Aina hii ya maneno huwa haitokei kama majina yametumika bali hutokea endapo tu majina hayapo.

N:B Viwakilishi haviwezi kutokea pamoja na majina katika sentensi

- **Mfano:** **wewe** ni mzuri

  W

- **Wao** wanaogopa matokeo
  W

- **Wangapi** watafaulu mtihani
  W

- **Huyu** aliyekuja amefaulu mtihani
  **W**

**AINA ZA VIWAKILISHI**

Kuna aina kuu tano za viwakilishi katika lugha ya Kiswahili, ingawa baadhi ya wanasarufi huainisha viwakilishi zaidi ya hivyo,

### a. Viwakilishi vya nafsi

Hivi ni viwakilishi ambavyo hutaja nafsi au huwa kilisha nafsi mbalimbali.

Mfano;

- Mimi ninasoma (nafsi ya kwanza umoja)

  W

- Sisi tunasoma (nafsi ya I wingi)

  W

- Wewe unasoma (nafsi ya II umoja)

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

W

- Yeye anasoma (nafsi ya III umoja)

W

- Wao wanasoma (nafsi ya III wingi)

W

**b. Viwakilishi vya Mahala/ vioneshi**

Hivi ni viwakilishi ambavyo huonyesha kitu kilipo

**Mfano:** Hawa ni wafanyakazi wa St. Mery Goreti

W

Huyu ni mlevi sana

W

Yule ni mtoto

W

C**. Viwakilishi viulizi**

Hivi ni viwakilishi ambavyo hutumika kuuliza swali ambalo hurejelea kwenye nomino husika

- Mfano: Lipi linakuchanganya

W

Wangapi wamefaulu?

W

**d.Viwakilishi vimilikishi**

Hivi ni viwakilishi ambavyo huonesha umiliki ambao huvumishwa moja kwa moja na nomino inayohusika

Mfano: Kwetu pazuri

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

W

Wangu ninampenda

W

Kwenu ni pazuri

W

e. **Viwakilishi vya kurejesha**

Hivi ni viwakilishi ambavyo hurejesha tendo kwa mtenda au mtendwa na mara nyingi huundwa na mzizi wa amba – pamoja na viambishi vya urejeshi

Mfano: Ambao wamechelewa wameadhibiwa

W

Ambazo zimejengwa barabarani zibomolewe

W

Ambavyo vimeharibika vitupwe

W

Aliyepotea amepatikana

W

**III VIVUMISHI (V)**

Vivumishi ni maneno au kikundi cha maneno ambacho hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi. Vivumishi ni maneno yanayovumisha majina au viwakilishi vilivyomo katika tungo. Maelezo hayo ambayo huumbwa na majina yanaweza kuwa na tabia ya jina au idadi ya jina n.k

**AINA ZA VIVUMISHI**

Wataalamu wa sarufi ya Kiswahili wanatofautiana na katika uainishaji wa aina za vivumishi lakini pamoja na kutofautiana huko wanaonekana kukubaliana katika aina kuu nane (8) za vivumishi

**a. Vivumishi vya idadi**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Hivi ni vivumishi ambavyo huonesha idadi ya vitu watu au majina mengine yaliyotajwa. Vivumishi hivi huweza kutaja idadi ya vitu waziwazi lakini wakati mwingine hutaja idadi ya vitu katika orodha,

Mfano: Mikate mitano

V

Watu wengi

V

Ghorofa ya kumi

V

Chai kidogo

V

Maji mengi

V

**b. Vivumishi vya sifa**

Hivi ni vivumishi vinayosifia majina wakilishi vilivyopo katika tungo

Mfano: Mkulima hodari

V

Msichana mrembo

V

Nchi masikini

V

Uchumi dhaifu

V

**c. Vivumishi vya kumiliki**

Hivi ni vivumishi ambavyo huonesha umiliki wa kitu watu au wanyama

Mfano: Kitabu changu

V

Shule yake

V

**Vivumishi vioneshi**
Hivi ni vivumishi vinavyoonesha mahali kitu kilipo au mtu alipo huitwa vivumishi vya mahali kwa sababu vinaonesha mahali.
Mfano: **Mtoto** huyo.

V

Mtoto **huyo**
V
Mtoto **yule**
V

**Vivumishi viulizi**
Hivi ni vivumishi amabavyo huuliza ili kupata idadi ya watu au vitu.
Mfano: Vitabu **vingapi** vimenunuliwa?

V

Kiongozi **gani** amekuja?
V

**Vivumishi vya jina kwa jina**
Hivi ni vivumishi amabavyo huwa ni majina yanayovumisha au kutoa maelezo zaidi kuhusu majina mengine.
Mfano: Mtoto **kiziwi**
V

Mpenzi **jini**
V

Mpenzi **bubu**
V

Mzee **bubu**
V

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Vivumishi vya a-unganifu.**
Hivi ni vivumishi ambavyo huwa na jina lenye-a-ya uunganifu.
Mfano: Mambo ya kihuni
V

Chakula cha watoto.
V

Nguo za kichina
V

**Vivumishi vya pekee.**
Hivi ni vivumishi ambavyo huonesha ziada ya kitu, mtu au jina lolote lililotajwa.
Mfano: Mtu mwenyewe haeleweki
V
Sisi sote ni ndugu
V
Ninyi nyote ni wanafunzi
V

**VITENZI**
Kitenzi ni neno ambalo hutaja jambo lilitendwa, linalotendwa au litakalotendwa na kitu, mtu au kiumbe chochote kile chenye uwezo wa kutenda tendo husika. Aidha kitenzi huonesha tabia au hali inayoweza kuwepo au kutokuwepo kwa mtu, kitu au kiumbe kingine chochote kile.

NB; Katika lugha ya kiswahili vitenzi huwa havitumiki pekeake bali huambatana na viambishi ambavyo hudokeza nafsi ya mtendwa au mtenda, wakati tendo lilipofanyika pamoja na kauli ya tendo.
mfano:
Kula - Anakula

**Vivumishi vioneshi**

**c.** Hivi ni vivumishi vinavyoonesha mahali, kitu kilipo au mtu alipo huitwa vivumishi vya mahali kwa sababu vinaonesha mahali.

- Mfano: **Mtot**o huyo

  V

- Mtoto **huyo**

V

- Mtoto **Yule**

V

- Yule mtoto amepotea

V

**e. Vivumishi viulizi**

Hivi ni vivumish ambavyo huuliza ili kupata idadi ya watu au vitu

Mfano: Vitabu **vingapi** vimenununuliwa?
V
Kiongozi **gani** amekuja?
V

**f. Vivumishi vya jina kwa jina**

Hivi ni vivumishi ambavyo huwa ni majina yanayovumisha au kutoa maelezo zaidi kubuni majina mengine

Mfano: Mtoto **kiziwi**
V
Mpenzi **jini**
V
Mpenzi **Bubu**
V
Mzee **bubu**
V

**g. Vivumishi vya a- Unganifu**

Hivi ni vivumishi ambavyo huwa na jina lenye- a – ya uunganifu

Mfano: Mambo ya kihuni
V
Chakula cha watoto
V
Nguzo za kichina

**h. Vivumishi vya pekee**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hivi ni vivumishi ambavyo huonesha ziada ya kitu, mtu au jina lolote lililotajwa
Mfano: Mtu mwenyewe haeleweki
V
Sisi sote ni ndugu
V
Ninyi nyote ni wanafunzi
V

**IV. VITENZI**

Kitenzi ni neno ambalo hutaja jambo lililotendwa, linalotendewa, au litakalotendwa na kitu, mtu au kiumbe chochote kile chenye uwezo wa kutenda tendo husika. Aidha kitenzi huonyesha tabia au hali inayoweza kuwepo au kutokuwepo kwa mtu, kitu au kiumbe kingine chochote kile.

**N.B:** Katika lugha ya Kiswahili vitenzi huwa havitumiki peke yake bali huambatana na viambishi ambavyo hudokeza nafsi ya mtendwa au mtenda, wakati tendo lilipofanyika pamoja na kauli ya tendo.

Mfano:

Lala - Anaimba

Kula - Anakula

**AINA ZA VITENZI**

Wataalamu wa lugha ya Kiswahili wanatofautiana katika uanishaji wa aina za vitenzi, wapo wanaoainisha aina kuu tatu (3) yaani kitenzi kikuu (T) kitenzi kisaidizi (Ts) na kitenzi kishirikishi (t). na wapo wanaoainisha aina kuu (2) yaani kitenzi halisi na kitenzi kishirikishi

**N.B** Katika uainishaji wa vitenzi, tutashughulikia uainishaji wa aina kuu mbili (2) za vitenzi yaani vitenzi halisi na vitenzi vishirikishi.

**a. Kitenzi halisi**

Hivi ni vitenzi ambavyo hueleza matendo. Katika lugha ya Kiswahili kitenzi halisi kinaweza kutumika kimoja au zaidi ya kimoja katika sentensi. Vitenzi vinapotumika humbatana na viambishi ambavyo hudokeza nafsi wakati halisi au kauli ya tendo na hivyo kwa pamoja hufanya kifungu tenzi halisi.

**Aina za vitenzi halisi**

Kuna aina kuu mbili (2) za vifungu tenzi halisi

- Kifungu tenzi halisi kikuu (T)
- Kifungu tenzi halisi kisaidizi (TS)

1. **kifungu tenzi halisi kikuu (T)**

Hiki ni kifungu tenzi ambacho hueleza tendo lililofanywa, litakalofanywa au linalofanywa na mtendo au tendo alilofanyiwa, analofanyiwa au atakalofanyiwa mtendwa kutokana na sifa hii vitenzi hubeba nafsi ya mtenda, mtendwa wakati tendo lilipofanya pamoja. hali kauli ya tendo sifa hizi huzifanya kitenzi kuwa aina ya neno inayobebeshwa mzigo mkubwa katika lugha ya Kiswahili.

- Mfano: Juma alikula chakula

  T

- Juma anakula chakula

  T

- Juma atakula chakula

  T

**II. KIFUNGU TENZI HALISI KISAIDIZI (TS)**

Hiki ni kitenzi ambacho huambatana na kitenzi halisi kikuu na aghalabu huoneshwa wakati tendo lilipofanyika na pia hudokeza uyakinishi au ukanushi wa tendo. Kifungu tenzi halisi kisaidizi hutumika sambamba na kifungu tenzi halisi kikuu.

Kikitumika peke yake bila kuambatana na kitenzi kikuu basi dhima yake hubadilika na kuwa kitenzi kikuu kikiondolewa katika tungo, Kitenzi kisaidizi huchukua dhima ya kitenzi kikuu.

Mfano: Juma anataka kula chakula

Ts T

Juma anataka chakula

T

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**N.B**: Katika sentensi ya pili kitenzi **anataka** kimechukua dhima ya kitenzi kikuu baada ya kuondoa kitenzi kile ambacho kilikuwa kitenzi kikuu katika sentensi ya kwanza. Pia vitenzi visaidizi vinaweza kutumika zaidi ya kimoja katika sentensi visaidizi vinaweza kutumika zaidi ya kimoja katika sentensi.

- **Mfano:** Juma **alikuwa anatak**a **kwend**a kusoma
  TS TS T
-

**b. Kitenzi kishirikishi (t)**

Haya ni maneno yanayoonyesha tabia au hali Fulani iliyopo kwa mtu au kitu Fulani vitenzi vishirikishi ambavyo huonesha tabia au hali Fulani iliyopo kwa mtu au kitu huitwa vitenzi vishirikishi yakinishi. Na vitenzi vishirikishi ambavyo huonesha kutokuwepo kwa hali au tabia kwa mtu au kitu huitwa vitenzi vishirikishi vikanushi.

**N:B** Mara nyingi katika lugha ya Kiswahili kitenzi kishirikishi yakinishi ni "ni" na kitenzi kishirikishi **ni** na kitenzi kishirikishi kanushi "si" Lakini kuna vitenzi vingine vishirikishi zaidi ya hivyo katika lugha ya Kiswahili

Mfano

- Juma **ni** mtoto
  t
- Juma **si** mtoto
  t
- Juma **siyo** mwizi
  t
- Udongo **u** mkavu
  t
- Babu **yu** mkali
  t
- Kitabu **ki** kidogo
  t

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Mchungwa **u** mkubwa
  t
- Midomo **i** minene
  t
- Ubao **u** mpana
  t
- Mbao **zi** pana
  t
- Hapa **pa** pachafu
  t
- Huku **ku** kuzuri
  t
- Humu **mu** mweusi
  t
- Chakula **ndicho** kitamu
  t
- Anna **ndiye** mgonjwa
  t
- Juma **angali** mtoto
  t
- Wanafunzi hawa **wangapi** wadogo
  t

**Maneno yote yaliyopigiwa mstari ni vitenzi vishirikishi**

**KAULI ZA VITENZI**

Vitenzi vya lugha ya Kiswahili vinatabia ya kunyumbuka na hivyo kuzalisha kauli mbalimbali za vitenzi. Kauli hizo ni kama zifuatazo

Mfano:

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

ii. Kauli ya kutendwa

**Mfano**: Pigwa

Somwa

Limwa

Chezwa

iii. Kauli ya kutendeka

**Mfano**: Pigika
Valika
Someka
Limika

iv. Kauli ya kutendana

**Mfano:** Pigana
Vaana
Toana
Somana

v. Kauli ya kutendana

**Mfano:** Iimiana
Someana
Valiana
Toleana

vi. Kauli ya kutendechwa

**Mfano:** Shoneshwa
Someshwa
Limishwa
Valishwa

vii. Kauli ya kutendea

**Mfano:** Pigia
Somea
Limia
Zalia

viii. Kauli ya kutendwa

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Mfano:** Pigiwa
Somewa
Shonewa
Chezewe

**HALI ZA TENDO**

Vitenzi vya lugha ya Kiswahili vinavyotumika huweza kuonesha hali tofauti kutokana na kuambishwa viambishi tofauti. Baadhi ya hali katika vitenda hujitokeza zaidi katika mazungumzo na nyingine mara chache

i. **Hali ya masharti**

Hali hii huonesha kuwa kufanyika kwa tendo Fulani sharti kutanguliwe na tendo lingine. Lazima kuwa na matendo mawili yaliyofuatana.

Mfano: Wangecheza kwa umakini wangepata ushindi

Akija nitamwambia

ii. **Hali ya kuendelea kwa tendo**

Hali hii huonekana katika tendo ambalo linaendelea kufanyika hili huziirishwa na mofu ya wakati "na" ambayo hupachikwa katika vitenzi.
Mfano: Anasoma
Anakula

**N: B** Pia hali ya kuendelea kwa tendo inaweza ikadokezwa na kiambishi "ki" ambacho aghalabu hutokea katika kitenzi cha pili katika sentensi yenye vitenzi sambamba.

**Mfano:** Aliniona nikisoma

**N.B:** Pia hali ya kuendelea kwa tena hudokezwa na kiambishi "Ka" katika masimilizi ya matendo yoliyofululizana katika masimulizi ya matukio mbali mbali, yaliyofanyika moja baada ya jingine kimsingi yalipaswa kutumia kiambishi "li"ambacho hudokeza wakati uliopita lakini matumizi yake humchosha msemaji na msikilizaji lakini pia ni kwa kurudia rudia na kurejesha sentensi bila sababu hivyo kiambishi "ka" hutumika badala ya "li"

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Mfano:** Tulifika chuoni tukapokelewa na mkuu wa chuo, akatupa funguo za bweni akatuonesha pakulala na katupa magodoro na mablanketi akatupeleka kafteria. Akatugawia sahani vijiko na visu akaagiza tugewe chakula kisha tukaenda kulala

**iii. Hali ya mazoea**

Hii ni hali inayoonesha kujirudia rudia kwa tendo au mazoea ya kufanya tendo Fulani

Mfano: Baba huamka asubuhi na mapema
Juma hucheza mpira wa miguu

N.B: Hali ya mazoea hudokezwa na kiambishi "hu"

**iv. Hali timilifu**

Hali timilifu katika vitenzi huonyesha kukamilika kwa tendo yaani tendo limekwisha kufanyika lakini athari za tendo hilo bado zinaonekana, kiambishi kinachotakiwa cha hali timilifu ni “me” katika hali ya uyakinishi katika hali ya ukanushi ni "ja"

**Mfano:**

- Juma amekimbia
- Juma hajakimbia
- Wazazi wake wamehama Tanga
- Mama hajapika chakula

**v. Hali ya kuamuru (amri)**

Hii ni hali ambayo hujitokeza katika kifungu tenzi na kawaida hudokezwa katika vitenzi na kiambish tamati “a” katika umoja nakiambashi tamati “eni” katika wingi paispo kumbatana na viambishi vya wakati.

| Mfano: | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| | Soma | Som – oni |
| | Tokea | Tok – eni |

**vi. Hali ya kuhimiza**

Hii ni hali ambayo hujitokeza kwenye vifungu tenzi kwa lengo la kusihi, au kumuomba mtu afanye jambo Fulani au asifanye jambo Fulani. Hali ya kutimiza hudokezwa na kiambishi “e” ambacho huwekwa mwishoni mwa kitenzi kwenye vitenzi vinayohusu nafsi ya kwanza umoja kwa vitenzi vinayohusu nafsi ya kwanza wingi hali ya kuhimiza huoneshwa na kiambish tamati “eni” ambacho huwekwa mwanzoni mwa kitenzi.

**Mfano**

Nilal-e
Niend –e
Tuend-eni

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

vii. **Hali ya kutarajia**

Hali huonesha matarajio ya kutendeka kwa jambo pasipo kuwa na uhakika wa kutimia kwa nia hiyo

**Mfano:**

Nipende
Tupendane

**N.B**: Hali ya kutarajia pia hudokezwa na kiambishi tamati “e”

**ALAMA ZA WAKATI KATIKA KITENZI**

Maranyingi vitenzi katika lugha ya Kiswahili huambatana na viambishi mbalimbali ambavyo hudokeza dhana mbalimbali na hivyo kufanya kazi kama kifungu tenzi. Kwa ujumla lugha ya Kiswahili ina nyakati kuu tatu zinazotumika zaidi yaani wakati uliopita wakati uliopo na wakati ujao. Nyakati hizi hudokezwa na viambishi mahususi vya matendo yanapokuwa katika yakinifu na yanapo kanushwa.

- **WAKATI ULIOPITA**

Wakati uliopita katika lugha ya Kiswahili hudokezwa na viambishi “–li” vitenzi vinapokuwa katika uyakinishi na kiambishi –ku- vitenzi hukanusha. Viambishi hivyo hutanguliwa na viambishi vingine kama vile viambishi vya nafsi na vya ukanushi.

**Mfano:**

| | |
|---|---|
| Ni-li-kula | si-ku-la |
| Tu-li-kula | ha- tu- kula |
| U-li-kula | hu-kula |
| M-li-kula | ha-m-kula |
| A-li-kula | ha-kula |
| Wa-li-kula | ha-wa-kula |
| Ni-li-soma | si-ku-soma |
| Tu-li-soma | ha-tu-ku-soma |
| U-li-soma | hu-ku-soma |

M-li-soma ha-m-ku-soma

A-li-soma ha-ku-soma

Walisoma ha-wa-ku-soma

**N:B** Hata hivyo vitenzi vya mzizi wa silabi moja huwa wakati uliopita vitenzi hivyo vinakuwa katika ukanushi kwa sababu ya athari za kimatamshi

- **WAKATI ULIOPO**

Wakati uliopita huonesha tendo linaloendelea kufanyika na kiambishi kinachodokeza wakati uliopo ni –na-"vitenzi vinapokuwa katika ukanushi kiambishi –i- hupachikwa mwishoni mwa vitenzi.

**Mfano:**

Ni-na-kula si-l-i

Tu-na-kula ha-tu-l-i

U-na-kula hu-l-i

M-na-kula ha-m-l-i

A-na-kula ha-l-i

Wa-na-kula ha-wa-l-i

- **WAKATI ULIOPO TIMILIFU**

Wakati timilifu katika lugha ya Kiswahili hudokezwa na mofimu –me- vitenzi vinapokuwa ktika uyakinishi na mofimu –ja- vitenzi vinapokuwa katika ukanushi

**Mfano:** ni-me-soma si-ja-soma

Tu-me-soma hu-tu-ja-soma

U-me-soma hu-ja-soma

A-me-soma ha-ja-soma

Wa-me-soma ha-wa-ja-soma

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

## V. VIELEZI (E)

Vielezi ni aina ya maneno ambavyo hutoa maelezo zaidi kuhusu kitenzi, kielezi mara nyingi hujibu maswali kama tendo limefanywa mara ngapi ? tendo limefanywa namna gani ? tendo limefanywa lini ? na wapi ?

**AINA YA VIELEZI**

**Vielezo vipo vya aina kuu tano**

### a. Vielezi vya namna /jinsi

Hivi ni vielezi ambavyo huonesha namna ambavyo tendo lililofanywa, linavyofanywa au litakavyofanywa

**Mfano;** Wanafunzi wanasoma **kwa bidii**

Mwizi alipigwa **sana**

Nilimuona **kwa macho yangu**

### b. Vielezi vya idadi/kiasi

Hivi ni vielezi ambavyo hueleza kiasi ambacho tendo limefanyika, mfano tendo limefanyika mara nyingi au mara chache

**Mfano:** Debe limejaa **pomoni**

**E**

Alianguka chini **mara tatu**

E

Anaenda shuleni **mara chache sana**

**E**

### c. Vielezi vya mahali/vioneshi

Hivi ni vielezi ambayo hueleza mahali ambapo tendo limefanyika

**Mfano:** Tuliambiwa twende **darasani**

E

Juma anaishi **Arusha**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**F**

Mwalimu amekwenda **nyumbani**

E

**d. Vielezi vya wakati**

Hivi vielezi ambavyo hudokeza muda au wakati tendo lilipofanyika

Mfano: Mvua imenyesha **usiku kucha**

**E**

Njoo **kesho** asubuhi

E

Tutafanya mtihani **Alhamisi**

E

**e. Vielezi viingizi**

Hivi ni vielezi ambavyo hueleza tendo lilivyofanyika kwa kuigiza au kufuatisha mlio wa sauti unaajitokeza wakati tendo husika inapotendeka

**Mfano:** Mbwa alilia **bwe**

E

Alidondoka chini **puu**

E

**N: B** Jambo la msingi la kuzingatia katika vielezi ni kwamba kielezi uhusiana na kitenzi, kielezi hutokea baada ya kitenzi au baada ya shamirisho na wakati mwingine kielezi kinaweza kutanguliwa kabla ya kitenzi.

**Mfano**: Juma anacheza **mpira uwanjani**

Sh E

Juma anacheza **uwanjani**

E

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Aliponiona** alikimbia

E

**VI. VIIGIZI/VIINGIZI/VIHISISHI (J)**

Haya ni maneno yanayodokeza vionjo au miguso ya moyoni au akilini aliyokuwa nayo mzungumzaji. Viingizi hudokeza hisia kama vile za furaha, huzuni, uchungu, kushangaa, kushtuka, laana, matumaini au kukata tamaaa, huruma na n.k

**Mfano:** **Ebo!** unaumwa nini?

I

Yanga **zii!**

I

**Lah!** Naipenda kweli

I

**Mmh!** We hujui tu

I

**N.B:** vihisishi mara nyingi vinapotumika katika maandishi huambatana na alama ya mshangao

**VII. VIUNGANISHI (U)**

Ni maneno au kikundi cha maneno, chenye kuunganisha kirai, kishazi au sentensi.

Dhima kubwa ya viunganishi ni kuunganisha vipashio viwili au zaidi vyenye hadhi sawa kisarufi. **Mfano**: Jina na jina kishazi na kishazi, kitenzi na kitenzi, sentensi na sentesi

**Mfano;** Shangazi **na** mjomba wanapendana sana

U

Aje Juma **au** Hamisi

n U

Vitabu vyote **vya** mama yangu

**U**

**AINA ZA VIUNGANISHI**

Viunganishi vinaweza vikagawanywa katika makundi makuu mawili

**a. Viunganishi huru**

Hivi ni viunganishi ambavyo husimama peke yake katika tungo au vipashio vinavyounganishwa.

Kiungo huru kinaweza kutoka katikati ya tungo mbili zinazoziunganisha au mwishoni mwa tungo mbli zinazoziunganishwa

**Mfano:** Nitukane tu **lakini** nakupenda

U

**Hata** ukinitukana nakupenda

U

**AINA ZA VIUNGAISHI HURU**

Viunganishi huru vinaweza vikagawanywa katika makundi madogo madogo.

**a. Viunganishi huru nyongeza**

Hivi ni viunganishi ambavyo huelekeza dhana ya kuongezwa idadi ya vitajwa au matendo yanayosimuliwa

**Mfano:** Juma **na** zaina wanaondoka kesho

U

Aliiba chakula **kisha** akaiba na sahani

U

**b. Viunganishi huru chague**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hivi ni viunganishi huru ambavyo hudokezwa maana ya uchambuzi wa vitajwa au matendo

**Mfano:** Sinywi pombe **wala** kuvuta sigara

U

Utaondoka leo **ama** kesho

U

c. **Viunganishi huru linganishi**

Hivi ni viunganishi ambavyo hudokeza hali ya kulinganisha iliyopo katika tungo mbili au zaidi

Mfano: Nakupenda **ingawa** hunitaki

U

Juma hakufaulu **sembuse** Ali afaulu

U

Aliondoka mapema **lakini** alichelewa kufika

U

d. **Viunganishi huru sababu**

Hivi ni viunganishi ambavyo hudokeza sababu au matokeo ya matendo yaliyofanyika

Mfano: Alifeli mtihani kwa sababu hakusoma

Ijapokuwa nakupenda usininyanyase

Unaongea **kama** hutaki

-Iliopigiwa mstari ni viunganishi.

**AINA ZA VIUNGANISHI TEGEMEZI**

Hivi ni viunganishi ambavyo huwa na kiambishi cha O – ya urejeshi ambayo huwekwa katika kitenzi cha kishazi tegemezi ili kukiunganisha na kitenzi kikuu cha kishazi huru ambavyo kwa pamoja huunda sentensi changamano.

**N.B** Viambishi tegemezi huwa ni viambishi, lakini wakati mwingine pia huweza kuwa ni maneno maalumu. Pia viunganishi tegemezi vinawezakutokea mwanzoni mwa tungo mbili zinazounganishwa

**Mfano:** **Aliponiona** alikimbia

U

Chakula **kilichobaki** kimechacha

U

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Katika sentensi hizo viunganishi tegemezi ni –po- na – cho-, ambapo kiunganishi –po- kinaunganisha chakula kilibaki na chakula kimechacha.

Wakati mwingine pia viunganishi tegemezi huweza kujitokeza kama maneno

Mfano: **Ijapokuwa** nilimkataza alimpiga

U

**Ingawa** hakusoma alifaulu

**U**

**VIII VIHUSISHI (H**)

Haya ni maneno yanayoonesha uhusiano baina ya tungo mbili zenye maadhi tofauti kisanii

**Mfano:** Uhusiano kati ya kitenzi na jina

Anatembea **kwa** miguu

H

Anakula **kwa** kijiko

H

Simama **mbele** ya nyumba

H

Huyu ni mtu **mwenye** maneno mengi

H

**N:B:** Baadhi ya wanasarufi huchanganya dhana ya viunganishi na vihusishi lakini ukweli ni kwamba dhana ya viunganishi na vihusishi hutofautiana. Tofauti hii hutokana na dhima ya dhana hizo katika tungo. Kwamba dhima ya viunganishi ni kuunganisha tungo zenye hadhi sawa kisarufi wakati dhima ya vihusishi ni kuonesha uhusiano uliopo baina ya tungo mbili zenye hadhi tofauti kisarufi.

**AINA ZA VIHUSISHI**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**a. Vihusishi vya Mahala**

Ni vile ambavyo huonesha uhusiano wa Mahala baina ya tungo mbili

**Mfano** Aliweka **katika** sanduku

**H**

Alikaa **mbele** ya mlango

H

**b. Vihusishi vya wakati**

Hivi huonesha uhusiano wa wakati baina ya tungo mbili

**Mfano:** Alifika **baada** ya masaa machache

**H**

**c. Vihusishi vya sababu**

Hivi huonesha sababu au uhusiano uliopo kwa kutokea kwa jambo Fulani baina ya tungo mbili

**Mfano:** Alipigwa kwa ajili ya makosa yake

H

**d. Vihusishi vya ulinganishi**

Hivi huonesha uhusiano wa kimlinganisho baina ya tungo mbili

**Mfano:** Ng'ombe ni mmoja kuliko mbuzi

H

**e. Vihusishi vya namna au jinsi**

Hivi vinaonesha uhusiano wa kinamna baina ya tungo mbili

**Mfano:** nataka maji ya moto

H

**f. Vihusishi vimilikishi**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Hivi honesha uhusiano wa kumiliki baina ya tungo mbili

**Mfano:** Aliiba fedha za kanisa
H

## g. Vihusishi vya ala (chombo kilichohusika)

Hivi huonesha uhusiano uliopo baina ya tendo na kitukilichotumika katika tendo hilo

Mfano: Alipigwa kwa fimbo
H

**Maswali**

1. Nini tofauti kati ya viwakilisi na majina?
2. Kuna uhusiano gani kati ya nomino na vivumishi au viwakilishi na vivumishi
3. Vitenzi vishirikishi katika lugha ya Kiswahili si vingi lakini ni muhimu jadili
4. Si kila kiambishi huambatana na mzizi kwa namna ile ile jadili kwa mifano
5. Kuna tofauti gani kati ya tungo na sentensi?
6. Kirai ndiyo msingi wa muundo wa tungo nyingine Thibitisha kwa mifano
7. Vivumishi katika lugha ya kiswahihi havina uhai nje ya umbo la kirai nomino thibitisha kwa mifano.

## 2. KIRAI/KIKUNDI

Kirai ni kipashio au tungo yenye neno moja au zaidi lakini isiyokuwa na muundo wa kiima na kiarifu. Muundo wa kiima na kiarifu ni muundo uoneshe mtenda na jambo linalotendwa au mtendwa wa jambo na jambo analotendwa. Kuna miundo mbalimbali ya kirai ambayo uhusisha neno moja au zaidi ambayo huwekwa kwa pamoja kwa kuzingatia mpango maalumu ambao huzingatia uhusiano baina ya neno kuu na maneno mengine ambayo huambatana na neno kuu.

**Mfano:** Kirai nomino

Katika kirai nomino neno kuu ni nomino hivyo muundo wake umekitwa kwenye nomino na neno au fungu la maneno.
Mfano: Mtoto yule mwembamba
KN
Miti ile mitatu mirefu
KN

**SIFA ZA KIRAI**

Kirai kina sifa mbalimbali ambazo hukifanya kirai kiweze kutambulika kiurahisi

i. Kirai hakina kiima na kiarifu muundo ambao huonesha mtenda na jambo analolitenda, tungo nyingine ni neno, kishazi na sentensi

ii Kirai hujengwa na neno moja moja au zaidi ya moja kwa kuzingatia uhusiano uliopo baina ya neno kwa maneno mengine

iii Hutegemea uhusiano maalumu baina ya neno, na maneno mengine yanyohusiana na neno kuu (uainishaji wa virai)

**Mfano:** Katika kirai nomino neno kuu ni nomino katika kirai kiunganishi neno kuu ni kiunganishi.

iV. Kirai huweza kutokea upande wa kiima au kiarifu katika sentensi

V. Kirai ni tungo kubwa kuliko neno, lakini ndogo kuliko kishazi

**AINA ZA VIRAI**

**Kuna aina kuu tano za virai. Ambazo ni**

1. Kirai nomino (KN)
2. Krai kivumishi (KV)
3. Kirai kitenzi (KE)
4. Kirai kielezi (KE)
5. Kirai kiunganishi (KU)

**1. KIRAI NOMINO**

ni kirai ambacho muundo wake umekitwa kwenye mahusiano ya nomino na maneno mengine na nomino na maneno mengi ambayo yanamahusiano na nomino. Neno kuu katika kirai nomino ni nomino ambayo ndiyo msingi mkuu wa mahusiano na maneno mangine.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**MIUNDO YA KIRAI NOMINO**

Kirai nomino kina miundo mbalimbali

**I.Muundo wa nomino peke yake**

**Mfano**: Cbaki)

Baba

Mama

Winnie

**b. II.Nomino mbili au zaidi zilizounganishwa**

**Mfano:** Baba na mama

Baba na bibi

Babu na bibi

Mwalimu na wanafunzi

Mjomba na shangazi

**III.Muundo wa nomino na kivumishi kimoja au zaidi**

**Mfano:** Mtoto Mweusi

Watoto wanene wazuri

Watoto na shangazi

**IV. Muundo wa nomino na kivumishi kimoja au zaidi**

**Mfano:** Yule mtoto

Watoto wake watatu wanene wazuri

**d.** v.**Muundo wa kivumishi na jina**

**Mfano:** Yule mtoto

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kile kitabu

**VI. Nomino na kishazi tegemeza kivumishi**

**Mfano:** Mbwa aliyepata kichaa

**f.** VII. **Nomino , kivumishi na kishazi tegemezi kivumishi**

**Mfano:** Msichana Yule mrembo uliyeniona naye jana

**g.** VIII.**Nomino na kirai kivumishi**

**Mfano:** Mzee mwenye duka kubwa kule kijijini

Watu wengi wenye matatizo ya kifedha

**h.** IX. **Kiwakilishi pekee yake**

**Mfano:** Wewe mimi yeye

**i.** X. **Muundo wa kiwakilishi na kivumishi**

**Mfano:** Vyake vyake

Wao wenyewe

**II. KIRAI KIVUMISHI (KV)**

Hiki ni kirai ambacho muundo wake umejikita katika kivumishi pamoja na neno au fungu la maneno linaloambatana na kivumishi.

**N:B:** Ingawa virai vivumishi hujibainisha kimuundo mara nyingi miuundo yake imekuwa ikichukuliwa kama sentensi kwa baadhi ya miundo ya virai nomino

**Mfano:** Watu wengi wana matatizo ya kifedha

KV

Mfano huu ni wa kirai nomino lakini ndani ya kirai nomino hicho kuna kirai kivumishi ambacho kimepigiwa mstari

**MIUNDO YA VIRAI VIVUMISHI**

**a. Kivumishi na kielezi chake**

**Mfano:** baya sana

Zuri sana

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**b. Kivumishi na kirai nomino**
**Mfano:** Enye duka kubwa
Enye nguvu nyingi
Enye macho makubwa

**c. Kivumishi na kirai kitenzi**
**Mfano:** enye kupenda fujo

**d. Kivumish na kirai kitenzi**
**Mfano:** Ingine – enye matatizo

**e. Kivumishi na kirai kiunganishi**
**Mfano**: zuri wa kutamanisha
Pungufu wa akili

**III. KIRAI KITENZI**

Hiki ni kirai ambacho muundo wake umekitwa katika mahusiano na kitenzi au uhusiano baina ya kitenzi na neno au fungu la maneno ambalo huambatana na kitenzi kimahusiano.

**MIUNDO YA KIRAI KITENZI**

**a. Kitenzi peke yake**
**Mfano:** Anaringa

Atapigwa

**b. Kitenzi na nomino**

**Mfano: tumesemewa risala**

KT

**c. Kitenzi na nomino mbili**

**Mfano: Tulimpa mtoto chakula**

KT

**d. Kitenzi na kitenzi**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Mfano: Watoto wanaimba wakicheza**

KT

**e. Kitenzi nomino na kitenzi**

**Mfano: tulimuomba mwalimu afundishe**

KT

**f. Muundo wa ruwaza wa kitenzi "kuwa"**

**Mfano**: a. Unaotokana na kitenzi na kivumishi

- Alikuwa mrefu

b. Kitenzi na kirai kiunganishi

- alikuwa na pesa

c. Kitenzi na nomino pahala (kielezi)

- Alikuwa darasani

d. Kitenzi kielezi na kitenzi

-Itakuwa vizuri uwahi

**IV. KIRAI KIELEZI (KE)**

Tofauti na aina nyingine za virai miundo virai haijakitwa katika mahusiano baina ya neno kuu, yaani kielezi na neno au fungu la maneno linaloandamana na kelezi. Badala yake miundo ya kirai kielezi huwa inahusishwa maneno ambayo hufanya kazi kwa pamoja katika lugha kama misemo tu.

**Mfano:** Mara kwa mara

-Mara nyingi

-Sana sana

-Haraka haraka

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**N:B** Dhima kubwa ya virai vielezi katika sentensi ni kueleza jinsi, mahali wakati na sababu zilizofanya tendo Fulani lifanyike.

Tofauti na virai vingine ambavyo nafasi yake ndani ya sentensi huwa yakudumu, nafasi ya virai vielezi hubadilika yaweza kuwa mwanzoni au mwishoni mwa sentensi

**Mfano**: mwalimu alifundisha **jana jioni**

KE

**Jana jioni** mwalimu alifundisha

KE

V. **KIRAI KIUNGANISHI**

Hiki ni kirai ambacho muundo wake umekitwa katika mahusinano baina ya maneno kama vile; kwa, na, katika, na kwenye katika fungu la maneno linaloambatana nacho. Kirai kiunganishini ni kirai ambacho neno kuu ni kiunganishi

**NB:** Katika lugha ya Kiswahili virai viunganishi vinamuundo mmoja tu nao ni ule wa kiunganishi na kirai nomino

**Mfano:** Kwa miguu

Kwa amri ya jeshi

Kwa baba yake

Katika chumba

Na mama

Kwenye pombe

Japokuwa virai hivi vinamuundo mmoja, yaani kiunganishi na kirai nomino vinatofautiana sana kimaana.

Mfano: Baadhi ya virai viunganishi vinaonesha dhana ya uhusika naVingine vinadokeza dhana ya mahali au

a. Pahala; - Katika chumba

Kwenye pombe

Kwa baba yake

b.Vingine vinadokeza dhana ya utumishi

Kama vile kwa kijiko

Kwa miguu

C.Vingine hudokeza sababu - kwa amri ya jeshi

## 3. KISHAZI

Hii ni tungo yenye kitenzi ambacho huweza kujitosheleza na kutoa taarifa iliyokamili au yaweza kuwa na kitenzi kisichojitosheleza na hivyo kushindwa kutoa taarifa iliyokamili au uliokusudiwa na mzungumzaji

**Mfano**: Msichana uliyemuona jana

Msichana anasoma

Mzee aliyepotea

Mzee amepatikana leo asubuhi

**AINA ZA VISHAZI**

**Kuna aina kuu mbili za vishazi**

### 1. KISHAZI HURU (k/Hr )

Kishazi huru ni kishazi kinachotawaliwa na kitenzi kikuu na hivyo kukifanya kishazi hicho kutoa ujumbe unaojitokeza na kisichohitaji maelezo yoyote ya ziada

**Mfano:** Wanafunzi wanamsikiliza mwalimu

-Mwalimu anafundisha wanafunzi

Vishazi hivi vinajitosheleza kwa sababu vinatoa ujumbe usiohitaji maelezo ya ziada

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**N:B**: Vishazi vinahadhi sawa na sentensi sahili

**II KISHAZI TEGEMEZI (K/TG)**

Kishazi tegemezi ni kishazi ambacho kinatawaliwa na kitenzi ambacho hakikamilishi ujumbe ulokusudiwa na hivyo kukifanya kutegemea kitenzi kikuu cha kishazi huru ili kukamilisha ujumbe ulikusudiwa na mzungumzaji.

**Mfano: -**Wanafunzi waliokuwa darasani

- Mwalimu aliyefundisha

Vishazi hivi ni tegemezi kwa sababu vinatoa ujumbe usiojitosheleza hivyo vinahitaji kuandamana na kisha huru ili kukamilisha ujumbe uliokusudiwa.

**Mfano :** wanafunzi waliokuwa darasani wamefukuzwa shule.

Mwalimu aliyefundisha amesimamishwa kazi.

**N:**B Kishazi tegemezi hakikamilishi ujumbe mpaka kiandamane na kishazi huru. Kishazi tegemezi kinapoambatana na kishazi huru vyote kwa pamoja hutengeneza sentensi changamano.

**AINA ZA VISHAZI TEGEMEZI**

Vishazi tegemezi vinaweza kugawanya katika makundi makuu mawili

a. **Kishazi tegemezi kivumishi (K/TGV au BV)**
b. **Kishazi tegemezi kielezi (K/TgE au BE)**

**KISHAZI TEGEMEZI KIVUMISHI**

Vishazi tegemezi vumishi ni vishazi ambavyo huvumisha au hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino zilizopo katika tungo, yaani nomino ya kiima au nomino ya shamirisho, kishazi tegemezi, kivumishi kinaweza kutokea kwenye kiima au kiima au kiarifu katika sentensi.

Mfano: Wanafunzi waliotoroka jana wanaadhibiwa leo asubuhi

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

BV

Mwalimu amewaadhibu wanafunzi waliotoroka jana

BV

**KISHAZI TEGEMEZI KIELEZI**

Hiki ni kishazi kinachotawaliwa na kitenzi ambacho huwa na utegemezi wa taarifa hiyo huhitaji kukamilisha taarifa hiyo kwa kuambatana na kitenzi kikuu cha kishazi huru. Kishazi tegemezi kielezi hutoa maelezo zaidi kuhusu kitezi kikuu kilichokuwepo katika tungo

**Mfano:** Alikikata alipolima

BE

Waalimu **walipotuma** walitufukuza

BE

**Sifa za kishazi tegemezi**

**Kishazi tegemezi kinasifa bainifu ambazo hukifanya kijulikane kiurahisi**

**i** Hakiwezi kutoa maana kamili kama hakijaambatana na kishazi huru

**Mfano:** Mwalimu alipoanza kufundisha

B

Mzee uliyemuona jana

B

**ii**. Kinaweza kuondolewa katika sentensi na kisiharibu maana ya sentensi nzima

**Mfano:** Mbwa aliyepata kichaa ameuwawa

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Watoto waliponiona walifurahi

Kinaweza kutambulika kwa kuwepo vishazi vingine kama vile, ingawa, kwamba, ili, kwa sababu, au.

**Mfano:** -Mwalimu amesema **kwamb**a wanafunzi wengi wamefaulu

- Wanafunzi ambao hawapo wataadhibiwa

B

- **Ingawa** walifika hatukuwaona

B

- **Ili** tuweze kuendeleza lazima tufanye kazi Kwa bidii

B

Kinaweza kutanguliwa au kikafuatwa na kishazi huru

**Mfano**: nimemuona Rehema nilipokwenda

B

**HADHI YA VISHAZI**

Vishazi huru vinahadhi sawa na sentensi sahili

Mfano: Ng'ombe amechinjwa leo asubuhi

Kishazi tegemezi ambacho huandamana na kishazi huru, hadhi yake hushuka na hivyo kukifanya kuwa na hadhi sawa na kirai /kikundi.

**Mfano:** Ng'ombe aliyenunuliwa jana
Hiki ni kishazi tegemezi na hadhi yake imeshuka kulingan na kirai tena kira nomino

**DHIMA YA VISHAZI**

Vishazi vinapotumika katika tungo huwa na dhima mbalimbali

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Vishazi tegemezi vivumishi hufanya kazi kama vivumishi katika tungo.
  **Mfano:** Mtoto **asiyesikia** amepotea
  **V**

- Baadhi ya vishazi tegemezi hufanya kazi kama vishazi

Mfano: Watoto wanaofurahisha **wanavyoimba**

**E**

## 4. SENTENSI

Sentensi ni kifungu cha maneno kinachoanzia neno moja na kuendelea lakini chenye muundo wa kiima na kiarifu au kikundi nomino na kikundi kitenzi

**N.B;** Sentensi ndiyo tungo kubwa kuliko tungo nyingine zote katika mpangilio wa tungo

**MUUNDO WA SENTENSI**

Sentensi ina sehemu kuu mbili (2) Sentensi ikigawanywa kwa kutumia kigezo cha kidhima ina sehemu kuu mbili ambazo ni KIIMA na KIARIFU

Sentensi ikigawanywa kwa kuangalia muundo wa sentensi basi sentensi hugawanywa katika sehemu kuu mbili yaani KIKUNDI NOMINO na KIKUNDI KITENZI.

Mgawanyo huu hutokana na kanuni kuu ya kisintaksia ambayo hudai kila sentensi iliyosahihi na inayokubaliwa na wazawa wa lugha ya Kiswahili ni lazima iwe na muundo wa kiima na kiarifu au kikundi nomino na kikundi kitenzi.
Kiima hutaja mtenda au mtendwa wa jambo na kiarifu huarifu jambo linalotendwa na kiima au alilotendwa na kiima

**Mfano**: Juma anacheza mpira.

Juma ni kiima yaani mtendwa na kiarifu ni anacheza mpira

Hapa pia nomino **mpira** ndiyo kiima, lakini kiima hiki kinataja kile kinachotendwa yaani mpira

**KIIMA**

Kiima ni sehemu ya sentensi ambayo hujaza na nafasi ya mtenda au mtendwa katika sentensi

**NB:** aghalabu kiima hutokea upande wa kushoto wa kitenzi

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Mfano:Mwalimu**/anafundisha wanafunzi

K

**Wanafunzi/** wanafundishwa na walimu

K

Kwa kawaida kiima hukaliwa na jina au kikundi jina ambalo hujaza nafasi ya mtenda au mtendwa katika sentensi

**VIPASHIO VYA KIIMA**

**Kiima kinajengwa na nini?**

**Kiima hujengwa na vipashio vifuatavyo**

i. **Jina peke yake**

Mfano: Mwalimu / anafundisha wanafunzi

K

ii. **Jina na Jina**

Mfano: Baba na mama/wanakula

K

iii. **Jina na kivumishi**

Mfano: Mtoto mzuri/amepewa zawadi

K

iv. **Kivumishi na jina**

Mfano: Yule mwizi/amekamatwa

K

v. **Kiswahili peke yake**

Mfano: Wewe ni mzembe

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

K

**vi. Kiwakilishi na kivumishi**

Mfano: Yule mzembe / amefukuzwa

K

**vii.Kitenzi jina na jina**

Mfano: Kulia kwa mtoto/kunasikitisha

K

**viii. Kitenzi jina na jina**

Mfano: Kulia kwa mtoto/kunasikitisha

K

**ix. Kitenzi jina na jina**

Mfano: Kuungua kwa mtoto /kunasikitisha

K

**x. Kitenzi jina na kivumishi**

Mfano: Kuimba na kucheza kwake/kunafurahisha

K

**xi. Jina na kishazi tegemezi kivumishi**

Mfano: Mtoto aliyepotea /amepatikana leo asubuhi

K

**xii.Nomino, kivumishi na kishazi tegemezi kivumishi**

Mfano: Mtoto mzuri uliyemuona jana/ni ndugu yangu

K

**xiii. Kivumishi nomino kivumishi na Bv**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mfano, Yule mtoto uliyemuona jana /ni mwanafunzi

K

## KIARIFU (A)

Hii ni sehemu muhimu zaidi katika sentensi na wakati mwingine huweza kusimama peke yake bila kiima kwa kuwa hubeba viwakilishi vya kiima. Kiarifu ni sehemu katika sentensi ambayo hukaliwa na maneno ambayo huarifu tendo lililofanywa, linalofanywa au litakalofanywa na kiima.

Mfano: Mwalimu/anafundisha wanafunzi darasani

A

**VIPASHIO VYA KIARIFU**

i. Kitenzi kikuu peke yake

Mfano: Mtoto anacheza

A

ii. Kitenzi kisaidizi au visaidizi vilivyo sambamba na (T)kitenzi kikuu

Mfano: Mtoto alikuwa anataka kucheza

A

iii. Kitenzi kishirikishi na shamirisho

Mfano: Watoto/wanacheza uwanjani

A

Iv Kitenzi kikuu na chagizo

Mfano: Watoto/wanacheza uwanjani vizuri

A

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

v. Kitenzi kikuu shamirisho na chagizo

Mfano: Mwalimu/anafundisha wanafunzi darasani

A

vi. Kitenzi kisaidizi kikuu na shamirisho
Mfano: Mwalimu /alikuwa anafundisha wanafunzi wengi
A

vii. Kitenzi kisaidizi kikuu na chagizo
Mfano: Mwalimu/alikuwa nafundisha darasani
A

viii. Vitenzi visaidizi kikuu, shamirisho na chagizo
Mfano: Mzazi/alikuwa anataka kuwarudisha watoto wake nyumbani
A

- **SHAMIRISHO (sh)**

Shamirisho ni jina au kikundi jina (kirai nomino) kinachojaza nafasi ya mtendwa au mtenda, mtendwa katika sentensi. Shamirisho hutokea baada ya kitenzi kikuu au kitenzi kishirikishi katika sentensi,

Shamirisho hujibu swali mtenda amemtenda nani, Au mtendwa ametendewa nini?.lakini pia mtendwa ametendwa na nani?

Mfano: Wanafunzi/wanasoma vitabu

Sh

Juma/alimisomea Asha kitabu

Sh

- **CHAGIZO (ch)**

Chagizo ni sehemu ya sentensi ambayo hutokea upande wa kiarifu ambayo huwa na neno au kikundi cha maneno ambacho hujaza nafasi ya kielezi.

Mfano:Mama /amekwenda nyumbani

Ch

Mtoto /anacheza mpira vizuri sana

Ch

N:B Chagizo huwezakutokea mara baada ya kitenzi kikuu au mara baada ya shamirisho

**AINA ZA SENTENSI**

KKuna aina kuu nne za sentensi
Sentensi changamano
Sentensi sahili/ huru.

3. Sentensi shurutia
Sentensi Ambatano

**1.SENTENSI SAHILI/HURU**

Hii ni aina ya sentensi ambayo hutawaliwa na kishazi huru. Kishazi hicho kinaweza kuwa kifungu tenzi kimoja ambacho kinaweza kuwa na kitenzi kikuu au kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu au kitenzi kishirikishi na shamirisho

Mfano: Juma ni mzembe

Juma alikuwa mzembe sana

Mwalimu alikuwa nafundihsa darasani

**MIUNDO YA SENTENSI HURU /SAHILI**

Muundo wa kitenzi kikuu peke yake (tawaliwa)

Mfano: Wanacheza

Alinipiga

Wanasoma

**i.Muundo wa kitenzi kikuu peke yake (tawaliwa)**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mfano: Wanacheza

Alinipiga

Wanasoma

**ii.Muundo wa kitenzi na kitenzi kikuu**

**Mfano**: Alikuwa anasoma

Walikuwa wanataka kufundishwa

**ii Muundo wa kirai na kirai kitenzi**

**Mfano;** Mwalimu anafundisha

Wanafunzi wanamsikiliza

iii. **Muundo wa virai vitenzi vilivyokitwa katika kitenzi kuwa**

**Mfano:** John alikuwa kijana mzuri

Mwalimu atakuwa darasani

Aisha angekuwa wa kwanza

**V.Muundo ambapo virai nomino na virai kitenzi vinaambatana na vijalizo**

**Mfano:** Baba yangu alinunua machungwa mawili usiku

**SIFA ZA SENTENSI SAHILI/HURU**


1. .Inakiima ambacho kinaweza kutajwa wazi au kisitajwe kama kinaeleweka.
2. Inakiungo ambacho kinaunda kitenzi kikuu kimoja au kitenzi kiuu c akitenzi kisaidizi au kitenzi kuku na shamrisha na chagizo
3. Haifungamani na sentensi nyingine na inajitosheleza kimuundo na kimaana

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/


**UCHANGANUZI WA SENTENSI SAHILI**

Kuchanganua sentensi ni kitendo au mbinu ya kuitenga au kuigawa sentensi katika sehemu mbalimbali ambazo hujenga au kuiunda sentensi hiyo. Kuna mikabala mikuu miwili ya uchanganuzi wa sentensi,

1. Kwa kutumia mkabala wa kimapokeo ambapo sentensi hugawanywa katika kiima na kiarifu na baadaye hufuatiwa na vipashio vinavyojenga kiima na kiarifu




iii. Mkabala wa kimuundo/ kisasa ambapo sentensi hugawanywa katika sehemu kuu mbili yaani kirai nomino na kirai kitenzi kisha hufuatwa na vipashio vijengavyo kirai nomino na kirai kitenzi
Mfano; Wanafunzi wale walikua wanasoma darasani




**N:B**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Katika uchanganuzi wa sentensi ni muhimu kutofundishwa mikabala yote miwili (haipaswi)

Lakini kuna baadhi ya wataalamu wanachanganya mikabala yote Miwili katika uchanganuzi wao wa sentensi. Mfano; F.Nkwera (1978) TUMI (1988) J.S.Mdee (1996) Mohamed Taasisi ya dimu (1966)

**UCHANGANUZI WAKE**

i. Kutaja aina ya sentensi

ii Kutaja sehemu za sentensi yaani kiima/kikundi nomino, kiarifu/kikundi kitenzi

iii Kutaja vipashio vinavyojenga kiima na kiarifu

iv.Kutaja aina za maneno yote yaliyomo katika sentensi

v.Kuandika upya sentensi hiyo.

**AINA ZA UCHANGANUZI WA SENTENSI**

**Uchanganuzi wa sentensi hufuata**

i.Mishale/ mistari

ii.Matawi/msonge/ngoe

iii.Maelezo/maneno

iv.Parandesi/mabano

v jedwali/visanduku

## 1. UCHANGANUZI WASENTENSI SAHILI

## NJIA YA MANENO

**A.MKABALA NA KIMPOKEO**

i. Mtoto Yule alikuwa anataka kucheza mpira wake uwanjani
Hii ni sentensi sahili
Kiima ni mtoto Yule

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kiima kinanomino na kivumishi
Nomino ni mtoto
Kivumishi ni Yule
Kiarifu ni alikuwa anataka kucheza mpira wake uwanjani
Kiarifu kina vitenzi visaidizi viwili kitenzi kikuu, shamrisho, chagizo
Kitenzi kisaidizi cha kwanza ni alikuwa
Kitenzi kisaidizi cha pili ni anataka
Kitenzi kikuu ni kuchezea
Shamirisho ni mpira wake
Nomino ni mpira
Kivumishi ni wake
Chagizo ni uwanjani
Kielezi ni uwanjani

B.**MKABALA WA KISIASA**

Mtoto yule alikuwa anataka kuchezea mpira wake uwanjani

Hii ni sentensi sahili

Kirai nomino ni “mtoto Yule”

Kirai nomino kina nomino na kivumishi

Nomino ni mtoto

Kivumishi ni Yule

Kirai kitenzi ni alikuwa anataka kucheza mpira wake uwanjani

Kirai kitenzi kina vitenzi visaidizi viwili kitenzi kikuu kirai,nomino na kirai kielezi

Kitenzi kisaidizi cha kwanza ni alikuwa

Kitenzi kisaidizi cha pili ni anataka

Kitenzi kikuu ni kucheza

Kirai nomino kina nomino na kivumishi

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Nomino ni mpira
Kivumishi ni wake

Kirai kielezi kina kielezi

Kielezi ni uwanjani

### ii. NJIA YA MISHALE

## A. MKABALA WA KIMAPOKEO

Mtoto Yule alikuwa anataka kucheza mpira wake uwanjani


S → Sahihi
S → K+A
K → mtoto yule
K → N+V
N → Mtoto
N → Yule
A → Alikuwa anataka kucheza mpira wake uwanjani
A → Ts +Ts+T+Sh+Ch
Ts → alikuwa
Ts2 → Anataka
T → kuchezea
Sh → mpira
Sh → N+V
N → mpira
V → wake
Ch → wangapi
Ch → E
E → uwanjani

## B. MKABALA WA KISASA


Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

S → Sahili
S → KN+KT
KN → mtoto yule
N → N+V
N → Mtoto
V → Yule
KT → alikuwa anataka kuchezea mpira wake uwanjani
KT → Ts +Ts +T+KN + KE
TS1 → alikuwa
TS2 → anataka
T → Kuchezea
KN → Mpira wake
KN → N+V
N → Mpira
V → Wake
KE → uwanjani
KE → E
E → Uwanjani

## III. NJIA YA MATAWI



Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA




**IV. NJIA YA JEDWALI**

**A. MKABALA WA KIMAPOKEO**

| S.SAHILI | | | |
|---|---|---|---|
| K | A | | |
| | P | SH | |
| N | T | N | V |
| JUMA | NI | MTOTO | MWEMA |

**B. MKABALA WA KISASA**

| S.SAHILI | | | |
|---|---|---|---|
| KN | KT | | |
| | P | KN | |
| N | T | N | V |
| JUMA | NI | MTOTO | MWEMA |

**2.SENTENSI CHANGAMANO**

Ni sentensi inayotawaliwa na kishazi huru kimoja au zaidi, na kishazi tegemezi kimoja au zaidi. Kishazi huru/tegemezi hicho kinaweza kutokea upande wa kiima au kiarifu

Mfano: Wanafunzi waliotoroka jana wameadhibiwa leo asubuhi

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

B

Mwalimu amewaadhibu wanafunzi waliotoroka jana

B

**NB:** Sifa kubwa ya sentensi changamano ni kuwa na kishazi tegemezi ambacho hutegemea kishazi huru kilichomo ndani ya sentensi hiyo.

***MIUNDO YA SENTENSI CHANGAMANO***

Vishazi tegemezi vilivyomo ndani ya sentensi changamano ndiyo hutupatia miundo mbalimbali ya sentensi.

Hii ni miundo ambayo kirai nomino hubeba kishazi tegemezi kirejeshi ambacho hurejesha tendo kwa mtenda au mtendwa

Mfano: **Mbuzi aliyenunuliwa juzi** ameibwa leo asubuhi

BV

**Miundo yenye vishazi tegemezi vielezi**

Hii ni miundo ambayo vishazi tegemezi hurejelewa/hueleza hali ya vitenzi vilivyomo kutoka vishazi huru

Mfano: Mimi sikuvutiwa **alivyosema**

BE

**Juma aliponiona** alikimbia

BE

**UCHANGANUZI WA SENTENSI CHANGAMANO**

**Uchanganuzi wa sentensi changamano huwa na hatua zifuatazo**

i.Kutaja aina ya sentensi

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

ii.Kutaja kiima/kirai nomino na kiarifu/kirai kitenzi

iii.Kutaja vishazi vilivyomo katika sentensi nakishakueleza kazi ya kila kishazi

**Kwa mfano**: Kutaja kama kishazi tegemezi kinavumisha jina au kikundi jina kilichopo katika kiini

**Mfano**: **Mbuzi aliyenunuliwa juzi** ameibwa leo asubuhi

BV

Mwalimu aliwaadhibu **wanafunzi waliotoroka**

Bv

b. Kutaja kama kishazi tegemezi kinavumisha nomino au kikundi nomino kilichopo katika shamirisho.
c. Kutaja kama kishazi tegemezi kinatoa maelezo zaidi kuhusu kitenzi kikuu kilichopo katika kishazi huru
Mfano: **Juma aliponion**a alikimbia
BE
Juma alikimbia **aliponiona**

BE

Iv Kutaja aina zote za maneno katika sentensi hiyo


V.Kurudia kuandika sentensi hiyo

**I. NJIA YA MATAWI.**


**A: MKABALA WA KIMAPOKEO**

Mtoto aliyekuletea maji ya kunywa ni mwanangu

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA




Mtoto aliyekuletea maji ya kunywa n
i mwanangu




Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**NJIA ZA MISHALE**

S ⟶ Changamano
S ⟶ K+A (KN+KT)
K ⟶ Mtoto Yule aliyevunjika
K ⟶ N+V+BV
N ⟶ Mtoto
V ⟶ Yule
BV ⟶ Aliyevunjika
BV ⟶ TS
TS ⟶ Aliyevunjika
A ⟶ Ts+T+Ch (Ts +T+KE)
TS ⟶ Alikuwa
T ⟶ Anapelekwa
Ch ⟶ hospitali
Ch ⟶ E
E ⟶ Hospitali

**SENTENSI SHURUTIA**

Ni sentensi ambayo huwa na vishazi tegemezi viwili ambavyo utegemezi wake hutokana na mofimu "nge"- ngali –ngeli na –ki-. Mofimu hizi hufanya vishazi hivyo vitegemeane yaani kufanyika kwa tendo moja kunategemea tendo jingine au kutokuendeka kwa jambo fulani hutegemea kutokutendeka kwa jambo Fulani,

Mfano: Juma angejibu maswali yote angefaulu mtihani

- Ukisoma kwa bidii utafaulu mtihani

**N:B** Mofimu hizi zinapotumika katika sentensi shurutia huwa hazitakiwi kuchanganywa

**SWALI:** Huku ukitumia mifano onesha tofauti iliyopo kati ya sentensi na tungo

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**NGELI ZA MAJINA (NOMINO)**

Neno ngeli ni neno la Kiswahili lililotolewa kutoka lugha ya kihaya likiwa na maana ya vitu vinavyofanana au vinavyoshabihiana.

Kwa hiyo ngeli za nomino na makundi ya majina yanayofanana au yanayowiana kwa kutuma kigezo Fulani. Nomino za lugha ya Kiswahili zinaweza kuwekwa katika makundi yanayofanananana kwa kutumia vigezo vikuu viwili.

i. ) Kwa kutumia kigezo cha mofolojia ya maneno hayo ambacho huyapanga majina kwa kuangalia maumbo ya umoja na wingi wa majina hayo.

ii.) Ni kigezo cha kisintaksia ambacho huyagawa majina katika makundi yanayowiana kwa kuzingatia uhusiano uliopo baina ya majina na vitenzi.Majina yote yanayohusiana kwa namna moja au kwa namna inayofanaa yanapoishia na vitenzi hufanya kundi moja la ngeli.

**KIGEZO CHA KIMOFOLOJIA/MAUMBO YA UMOJA NA WINGI**

Hiki ni kigezo kilichotumika na wanasarufi wa mwanzo ambao waliainisha majina kulingana na maumbo ya umoja na wingi au viambishi awali vya majina hayo. Majina hayo yanayofanana katika viambishi awali yaliwekwa katika kundi moja na kufanya kundi moja la ngeli. Kama sarufi hao wapo walioyagawa majina katika makundi kumi na nane(18) na uongozi ulioyagawa majina hayo katika makundi tisa (9) lakini kwa kutumia kigezo hicho hicho cha kimafolojia kwa kutumia kigezo hiki tutayafafanua makundi ngeli kumi na nane (18) za majina ya Kiswahili.

| NGELI | SIFA ZA MAJINA | MFANO |
|---|---|---|
| 1.Mu | -Majina ya viumbe hai isipokuwa mimea | m-tu wa –tu |
| 2.Wa | -Vitenzi jina vyote vinavyotaja watu vina | m-toto wa- toto |
| | -Vitenzi jina vyote vinavyotaja watu Vinavyoanza na “m” katika moja na “wa” katika wingi | m-fungaji wa fugaji |
| 3.M- | -Majina ya baadhi ya mimea | m-ti mi –ti |
| 4Mi- | -Majina ya vitu vyote vinavyoanza na “M” katika umoja na “mi”katika wingi | m-papai mi – papai<br>m-pir mi-pira<br>M-sumeno mi-sumeno |

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

| | | |
|---|---|---|
| | -Majina ya matendo/vitenzi jina vinayoanza na "m" katika umoja na "mi" katika umoja na "mi" katika wingi | m-kasi mi-kasi<br>m-chezo mi- chezo<br>m-tupo mi-tupo |
| 5.Ki | | |
| 6 vi- | -Majina yote yanayoanza na "ki-" katika umoja na "vi-" katika wingi | Ki-nu vi-nu<br>Ki-kapu vi-kapu<br>Ki- umbe vi- umbe |
| | -Majina ya vitu vinayoanza na "ch" katika umoja na "vy" katika wingi | ki-goda vi-goda<br>ch-akula vy-akula<br>ch-uma vy-uma |
| | -Majina ya viumbe yanayoambikwa kiambishi"ki" mwanzoni cha kuvumisha | Ki-zee vi-zee<br>Ki-vulana vi-vulana<br>Ki-toto vi-toto |
| 7.Ji- | -yanaingia majina yanayoanza na | |
| 8.Ma | Ji-katika umoja na wingi | Ji-cho ma –we |
| | -Majina ya baadhi ya sehemu sa mwili wa binadamu wanyama au sehemu za mtu | Ji – cho ma-cho<br>Goti ma-goti<br>Ji-no meno |
| | -Majina ya mkopo yenye kuanzana "ma" katika wingi | Sikio ma-sikio<br>Maziwa maziwa |
| | -Majina yenye kueleza dhana ya wingi japokuwa hayahesabiki | Shati ma-shati<br>Bwana ma – bwana<br>Ua ma - ua |
| | -Majina yote yanayoanzia na N-na kufuatwa na konsonati ch, d, g, j, z, y katika umoja na wingi | Njaa,nguo, nchi, ndoa nzi<br>Nje, nyumba |
| 9 N | -Majina yanayoanza na M- na Mb | Mbuga, mboga, mvua mvinyo, mvi, mbao, taa |
| 10 | -Majina ya mkopo | |
| | N:B: Maumbo ya umoja na wingi katika majina haya haya badiliki | Kalamu |
| 11U<br>12N | -Majina yote yanayoanza na<br>U- katika umoja na N-au<br>Mb- katika wingi | U-so N-nyuso<br>U-zi N-yuzi<br>U – bao Mb – ao<br>u-limi ndimi |
| 13 U | -Majina yote yanayoanza na | U-asi ma – asi |
| 14Ma | U – katika umoja -ma- | U-gonjwa ma – gonjwa |

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

| | | |
|---|---|---|
| | Katika wingi | U-gonjwa ma-gonjwa |
| 15 ku | Majina yanayotokana na vitenzi vinavyoonea ku- mwanzoni | Ku – imba<br>Ku –cheza<br>Ku-la |
| 16. Pa | Huonesha mahali pa mbali<br>Kidogo palipo wazi | pahala |
| 17. Mu | Kuonesha mahali pa mbali lakini ndani | Mule |
| 18.ku | Mahali pa mbali zaidi | kule |

**FAIDA ZA UAINISHAJI NGELI KIMOFOLOJIA**

1. Hutumika kuonesha uhusiano wa lugha zenye asili moja

   Mfano: Lugha ya Kiswahili na lugha mbalimbali za kibantu. Majina mengi ya lugha ya Kiswahili yana maumbo dhahiri ya umoja na wingi pia majina mbalimbali ya lugha za kibantu yana sifa hiyo.

2. Ni rahisi kugawanya majina hasa yale yenye maumbo ya umoja na wingi katika makundi mbali mbali kwa kutumia kigezo hiki.

3. Kutumika kuonesha maumbo ya umoja na wingi katika nomino

**MATATIZO YA UAINISHAJI KIMOFOLOJIA**

1. - Ni vigumu kuyapanga majina yasiyokuwa na maumbo ya umoja na wingi katika makundi yake kwa kutumia vigezo hiki.

2. - Hakitilii maanani miundo ya sentensi kwa mfano nomino kama kipofu, kiongozi, kijana, zilipaswa kuwa katika ngeli ya **ki-vi** lakini zimepelekewa katika ngeli ya kwanza kwa kuwa zinaoana kimuundo na nomino nyingine za kundi hilo. Nomino hizo kimefolojia zinatofautiana na nomino nyingine za ngeli ya kwanza na ya pili.

3. - Hakikidhi mahitaji ya sulubu na sentensi .

   Mfano: Kitabu changu kimepotea

   Vitabu vingi vimepotea

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Kisu changu kimepotea

Visu vyangu vimepotea

Kijana wangu amepotea

Vijana wangu wamepotea

Baadhi ya nomino hazikidhi sababu za sentensi

4. Kuna viambishi vya ngeli vinavyofanana na kujirudia rudia kwa baadhi ya makundi ya majina. Mfano kiambishi mu – kinajitokeza katika ngeli ya makundi ya majina. Mfano kiambishi mu – kinajitokeza katika ngeli 3; ngeli kiwakilishi ma-cha ngeli ya 8; kinajitokeza katika ngeli ya 1

Kiambishi N. Kinajitokeza katika ngeli ya kumi na mbili pia kinatumika katika ngeli ya tisa na ya kumi.

**KIGEZO CH A KISINTAKSIA**

Hiki ni kigezo ambacho huyagawa majina katika makundi mbalimbali kutokana na kigezo cha upatanisho wa kisarufi uliopo kati ya maji na viambishi awali vilivyopo katika vitenzi ambavyo huyapatanisha majina hayo na vitenzi.

Majina yote yanayotumia viambishi awali vipatanishi vinavyofanana huwekwa katika kundi moja na kufanya kundi moja la ngeli. Kwa kutumia kigezo hiki kuna jumla ya ngeli tisa za nomino

| NGELI | Viambishi awali vipatanishi | Mfano |
|---|---|---|
| a -wa | a -wa | Kiongozi amepotea/viongozi wamepata |
| | a-umoja, | Simba amepotea/simba wamepotea |
| | wa-wingi | |
| u-i | u-(umoja) | Mto umefunika |
| | i-(wingi) | Mito imefunika |
| | | Mti umeanguka |
| | | Miti imeanguka |
| Li - ya | li-(umoja) | Yai limevunjika |
| | Ya-(wingi) | Mayai yamevunjika |
| | | Gari limetengenezwa |
| | | Magari yamebaribika |
| Ki-vi | Ki – (umoja) | Kiti kimevunjika |

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

| | | |
|---|---|---|
| | Vi-(wingi) | Viti vimevunjika |
| | | Chakula kimemwagika |
| | | Vyakula vimemwagika |
| i-zi | i-(umoja) | Nchi imefilisika |
| | Zi-(wingi) | Nchi zimefilisika |
| u-zi | u-(umoja) | Ukuta umebomoka |
| | Zi(wingi) | Kuta zimebomoka |
| | | Ubao umechafuka |
| | | Mbao zimechafuka |
| u-ya | u-(wingi) | Ugonjwa umeenea |
| | Ya-(wingi) | Magonjwa yameenea |
| | | Ubaya umeongezeka |
| | | Mabaya yameongezeka |
| ku | Ku- | Kucheza kunafurahisha |
| | | Kula kwake kunasikitisha |
| | | Kuimba kwao kunapendeza |
| Pa | | Pale panapendeza |
| Mu | | Mule mwanagiea |
| Ku | | Kule kunapendeza |

**FAIDA ZA KIGEZO HIKI**

1. - Hutumika kama kigezo cha ulinganifu wa lugha haswa Kiswahili na lugha za kibantu

2. - Hutumika kuyapanga majina katika makundi yanayofanana

3. -Huweza kuyaweka majina katika makundi kiurahisi zaidi hata yake yasiyokuwa na maumbo ya umoja na wengi ilimradi yahusiane kisarufi

**MATATIZO YA KIGEZO HIKI**

1. Katika ngeli ya kwanza kuna vipatanishi viwili vya umoja ambavyo ni yu na-a- kiambishi yu – ni cha Kiswahili cha kilahaja sio Kiswahili sanifu.

2. Huyaweka majina yenye maumbo na sifa tofauti katika kundi moja. Mfano nomino za kipekee kama vile Juma Amina Latifa na zile za kawaida kama vile chura, kaka ,mama , baba

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

3. Kuna baadhi ya majina ambayo viambishi vipatanishi vina utata hivyo inakuwa vigumu kuyainisha mfano: Jambazi amepigwa risasi /majambazi yamepigwa risasi

4. Kuna vipatanishi vinavyofanana katika ngeli.Mfano kiambishi -u- cha umoja katika ngeli ya pili kinajitokeza katika ngeli ya sita na ngeli ya saba. Kiambishi kipatanishi i – cha wingi cha ngeli ya pili kinajitokeza katika ngeli ya tano umoja na kiambishi patanishi "zi" wingi cha ngeli ya tano kinajitokeza katika ngeli ya sita wingi

**MATUMIZI YA NGELI**

1. Hutumika kuyapanga majina katika makundi yanayoshabihiana kwa kutumia kigezo maalumu mfano: kimofolojia na kisintaksia

2. Hutumika kutambulisha maumbo ya umoja na wingi katika nomino na vivumishi. Mfano;

   M-toto, m-zuri

   Ki-tabu ki-zuri

3. Hutumika kuonesha upatanishi wa kisarufi uliopo kati nomino, vivumishi na vitenzi mfano: Mtoto mzuri amepata
   -Kitu kizuri kimepotea

4. Hutumika kuonesha uhusiano baina ya lugha ya Kiswahili lugha mbalimbali za kibantu

Mfano:
KISHWAHILI – Mtoto analia
KIMARANGU-Mana naifira
KINYAKYUSA-Omwana ilolea
} kigezo cha kisintaksia

Kigezo cha kimofolojia {
M-toto - KISWHAHILI
m-wana - KIMARANGU
Omw - ana- -KINYAKYUSA

---

# UTUNGAJI

**Maana ya utungaji**

Utungaji ni pato la akili ya mtu binafsi ambayo hurejeshwa kwa fani kama vile macho, ushairi, tamthiliya au hadithi. Utungaji ni kitendo cha kuyatoa mawazo ubongoni, kuyakusanya na kisha

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

kuyadhihirisha kwa kuyaandika au kuyazungumza. Ni kitendo cha kuunda hoja na kuyapanga katika mtiririko unaofaa katika lugha kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii husika.

## SIFA ZA MTUNGAJI

1. Mtunzi analazimika kuelewa kikamilifu mada inayoshughulikiwa.
2. Mtungaji lazima azingatie kanuni na taratibu za uandishi.
3. Mtungaji anatakiwa kuzingatia mpango mzuri na wenye mantiki wa mawazo kutoka mwanzoni hadi mwishoni.
4. Mtungaji anapaswa kuwa na msamiati wa kutosha ili kumwezesha kutumia lugha bora, sanifu, na fasaha.
5. Mtunzi anapaswa kuzingatia sarufi ya lugha anayoitumia.
6. Mtunzi anapaswa kujali nyakati zinazofaa.
7. Mtunzi anapaswa kuwa na uwezo wa kutosha wa kuhusisha yanayoelezwa na hali halisi ilivyo katika jamii kwa mifano dhahiri.

## AINA ZA UTUNGAJI:-

1. Utungaji wa mazungumzo
2. Utungaji wa maandishi

## UTUNGAJI WA MAZUNGUMZO

Utungaji wa mazungumzo unahusisha kujieleza kwa njia ya mdomo kwa lengo la kueleweka.

## LENGO

-Hutuwezesha kujieleza kwa ufasaha katika kila fani.

-Hutuwezesha kutumia lugha inayotakiwa katika jamii.

-Hujenga moyo/hali ya kujiamini katika kuzungumza

-Kukuza kiwango cha wasikilizaji kwa makini kutoa uamuzi unaofaa.

-Kutuwezesha kutambua lugha inayofaa katika kujieleza kutokana na lafudhi, shada, matamshi na miundo.

## MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UTUNGAJI WA MAZUNGUMZO

1. Kusikiliza kwa makini, kuchambua na kuelewa vema mada inayozungumzwa. Kuzungumza kwa umakini na kufafanua kwa umakini mada unayozungumza, anapaswa kuzingatia mpango mzuri wa mawazo wenye mantiki kutoka mwanzo mpaka mwisho.
2. Mtunzi anapaswa azingatie hadhira anayozungumza nayo.

3. Mzungumzaji lazima awe na uwezo wa kufafanua na kuhusisha anayozungumza na hali halisi ilivyo katika jamii yetu.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

4. Mzungumzaji anapaswa awe na msamiati wa kutosha utakaomwezesha kutumia lugha bora, kujieleza vizuri na kutunza lugha sanifu na fasaha.

5. Ni vizuri mzungumzaji akazingatia sarufi ya lugha anayotumia na kujali nyakati.

## UTUNGAJI WA KUANDIKA

Ni uwezo wa kujieleza katika maandishi au uwezo wa kutoa mawazo binafsi na kuyaweka katika kiwakilishi cha maandishi. Utungaji wa kuandika tofauti kidogo na utungaji wa kuzungumza. Tofauti hizo hujitokeza katika kiwakilishi uwasilishaji wake.

Mazungumzo ya chanzo na kikomo na uhusiano baina ya mwandishi na msomaji. Kutokana na tofauti hizo katika utungaji wa kuandika maandishi zaidi yanahitajika ukilinganisha na utungaji wa kuzungumza.

## MAMBO YA KUZINGATIWA KATIKA UTUNGAJI WA KUANDIKA

1. Mwandishi aelewe vema mambo anayoandika.
2. Mwandishi anatakiwa kuzingatia mpango mzuri wa mawazo wenye mantiki kutoka mwanzo hadi mwisho.
3. Mtungaji anapaswa awe na msamiati wa kutosha utakaomuwezesha kutumia lugha iliyobora, sanifu na fasaha.
4. Mtungaji anapaswa awe na uwezo wa kubebesha yale anayoyaeleza na hali halisi ilivyo katika jamii yetu. Ni vizuri akatoa mifano dhahiri.
5. Kuzingatia matumizi bora ya vituo na alama mbalimbali za uandishi kuwa na utangulizi mzuri wenye kuvutia… ya watu na hitimisho zuri.
6. Mtungaji anapaswa kuzingatia sarufi ya lugha anayoitumia na kujali nyakati.

## Matumizi ya vituo na alama mbalimbali za uandishi:-

1. **Alama ya mkato (,)**

### Alama hii hutumika kwa kazi zifuatazo:-

(a) Kuweka pumziko fupi katika sentensi.

***Mfano:*** tulipofika nyumbani, tulikula chakula.

(b) Kutenga maneno yaliyo katika orodha.

***Mfano:*** ukifika sokoni nunua matunda, dagaa, mkaa, unga, na sabuni ya kufulia.

(c) Kuonesha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume.

***Mfano:-*** Sisi wanadamu hupanga, Mungu hupangua.

-Ulisema utakuja, hukuja

(d) Kutumiwa kabla ya alama za mtajo.

***Mfano:*** Juma alimwambia Khadija, Nakupenda kama pipi.

(e) Kuonesha vyeo, viwili au masikani baada ya jina la mtajwa

***Mfano:*** Philemon Ndesamburo

Mbunge wa Moshi mjini,

S.L.P 11646,

Ngangamfumuni,

**2. Nukta ( . )**

Alama hii hutumika kama ifuatavyo:-

(a) Hutumika kukamilisha sentensi na hivyo kuweka pumziko kubwa tunaposema.

***Mfano:*** Mtoto wangu nampenda sana.

(b) Kuonesha ufupisho wa maneno.

***Mfano:*** S.L.P - Sanduku la posta

n.k - nakadhalika

(c) Kuonesha vipimo mbalimbali katika desimali

***Mfano:*** kg. 80. 3

-Saa 2.30

**3. Nukta mkato ( ; )**

**Alama hii hutumika kama ifuatavyo:-**

(a) Kuunganisha sentensi mbili zinazoweza kusimama zenyewe bila kutumia kiunganishi.

***Mfano:*** Hapo zamani watu walijiheshimu sana; Siku hizi hawajiheshimu kabisa

(b) Hutumika ili kupumzika katika sentensi iliyondefu sana, kuliko unapotumika mkato.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

***Mfano:*** Alipomtazama alibaini kuwa alikuwa Malaya wa kutupwa; Hivyo aliamua kuachana naye.

4. **Nukta mbili / pacha (:)**

**Alama hii hutumika kama ifuatavyo,**

**(a) Hutumika kutaja maneno yaliyo katika orodha.**

***Mfano:*** Niletee vitu hivi: wino, karatasi, kalamu, kiberiti, daftari, wembe, ndimu, chungwa na ndizi.

(b) Hutumika badala ya alama ya mkato.

***Mfano:*** Alipomwona alianza kumshambulia kwa maneno:

-“Nakujua wewe huna lolote, mlevi kama wewe!”

(c) Hutumika baada ya kuandika jina la mhusika katika tamthiliya.

***Mfano:*** Julia: Kwani hujui kuwa Nungungungu anavusha kahawa na almasi kwenda nje kwa magendo?

***Mlemeta:*** Sijui

***Julia:*** Hujui kuwa Nungunungu anaakaunti na hoteli Uswizi?

(d) Kutenganisha dakika na sekunde.

***Mfano:*** Saa 8:30:48

(e) Kuonesha uwiano baina ya namba.

***Mfano:*** Juma na Hamisi waligawana machungwa 20 kwa uwiano ufuatao: 3:7. Je, kila mmoja alipata machungwa mangapi?

5. **Alama ya kushangaa ( ! )**

**Alama hii kutumika kama ifuatavyo:-**

(a) Hutumika kuonesha vionjo vya moyo kama vile furaha, huzuni , chuki.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

***Mfano:*** Kumbe Juma alikuwa mwizi wa mitumba!

(b) Hutumika wakati wa kusisitiza, kubeza, kutunza n.k

***Mfano:*** Kwenda! Mwone kwanza alivyo! Uso umemshuka!.

6. **Alama ya kuuliza (?)**

**Alama hii hutumika kama ifuatavyo:-**

(a) Hutumika kuuliza maswali.

***Mfano:*** Mwalimu leo tutafanya mtihani?

7. **Alama ya mabano [ ( ) ]**

**Alama hii hutumika kama:-**

(a) Hutumika kuonesha maana ya ziada katika sentensi.

***Mfano:*** Wale watoto wangu (Robson, Karen, na Maurene) nawapenda sana.

8. **Alama ya kistari ( - )**

(a) Alama hii hutumika kuonesha kuwa neno linaendelea katika mstari unao fuata-------

***Mfano:*** wafanya ka-

zi wa shu-

le wote.

(b) Hutumiwa kuzungumza maneno au kujenga neno moja na mtindo huu hutumika zaidi katika maneno yenye asili ya kigeni.

***Mfano***: Idd - Al- Haji

Dar – Es – Salaam

(c) Hutumika kuunganisha sentensi mbili, sentensi ya pili ikiwa ni ufafanuzi wa sentensi ya kwanza.

***Mfano:*** Tulipofika hifadhi ya manyara, tuliwakuta simba wamelala – simba dume, jike na watoto wanne.

(d) Hutumika badala ya nukta mbili.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

***Mfano***: Nenda kanunue –dagaa, muhogo, maharage, kuni .

9. **Alama ya mtaja ( “ ”  )**

(a)  Hutumika katika kukazia maneno aliyosema au aliyoandika mtu mwingine.

***Mfano:***  “Mwalimu Nyerere alisema, “Enzi za utawala wangu nilifanya mambo mengi mazuri na mengine ya kujenga kwa kuwa nchi yetu ilikuwa bado changa.  Lakini cha kushangaza ninyi mmechukua mambo ya kijinga niliyofanya na mnaacha mazuri niliyofanya.  Serikali imeshindwa hata kukusanya kodi!

(b)  Hutumika kubainisha maneno ya kigeni yanayotumika katika lugha fulani.

**Mfano**:  Ilituwia vigumu “kujiexpress” mbele za watu.

Tumefikishana mahakamani tatizo ni ugomvi wa “kiamba”

(c)  Hutumika kubainisha maneno ya msimu katika lugha fulani.

***Mfano:*** “Alipomcheki” aligundua kuwa ni “changudoa”

1. **Ritifaa  / kibainishi (‘ )**

(a)  Kutofautisha “ng” na “ng” katika baadhi ya maneno .

***Mfano:***  ngambo   - n’gombe ng’ambo

Ngangania   - ng’ang’ania

Ngarisha   - ng’arisha

(b)  Kuonesha kuwa herufi fulani imeachwa katika neno.

***Mfano***:  Vuta N’kuvute   - vuta n’kuvute

Watoto wa mama N’tilie  -

1. **Nukta katishi / nukta dukuduku ( ……….)**

(a)  Hutumika kubainisha mdokezo.

***Mfano:***  Nakupenda sana lakini…………………

(b)  Hutumika kuonesha kuwa kuna maneno yaliyotangulia katika tungo.

M***fano***:………………fika ofisini mara moja.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

2. **Matumizi ya herufi kubwa**

(a) Hutumika kila mwanzo wa sentensi

***Mfano:-*** Mama njoo

(b) Hutumika baada ya alama ya nukta, kuuliza, kushangaa.

***Mfano***: "Nani huyo?" Aliuliza mama.

Wewe ndiyo! Mwanga sana wewe.

(c) Hutumika kutaja majina ya kipekee

***Mfano:*** Winnie, Abel, Ade, Marco, Concepta, Manoza.

(d) Majina ya dira

***Mfano:*** Mashariki, Kaskazini

(e) Majina ya vyeo

***Mfano:*** Sheikh, Rais, Mwenyekiti

(f) Ufupisho wa vyama, mashirika, jumuiya

***Mfano***: UN, CHADEMA, HKL, ECOWAS

(g) Majina ya vitabu na mada …..

**Mfano:** "JE, TUTAFIKA?" "USHUHUDA WA MIFUPA", Mfadhili.

(h) Majina ya sikukuu

***Mfano:*** Krismass, siku ya wapendanao

(i) Majina ya nafsi yanapotumika kuleta maana maalum.

3. **Aya**

**Ni jumla ya sentensi zinazoelezea wazo moja na hufanya kazi zifuatayo:-**

(a) Hueleza au kufafanua wazo maalum

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(b) Kuwa na mawazo yaliyo katika mantiki

(c) Kuwa na mifano ya kutolea ufafanuzi.

4. **Mkwaju ( / )**

Kutenga maneno mawili yenye maana sawa yanapotumika kwa pamoja.

***Mfano:*** mofimu ya njeo / wakati

Hutumika kutenga namba za kumbukumbu na tarehe.

***Mfano:*** Kumb. 03/DA/20078

11/08/2014

**INSHA**

Insha ni maandishi au masimulizi juu ya jambo au kitu fulani. Uandishi wa insha huwa katika aya.

**MADHUMUNI YA UANDISHI WA INSHA**

1. Kujua ni jinsi gani mwandishi anaweza kujitegemea katika kuwaza na kujenga mawazo yake kwa makini.
2. Kujua ni jinsi gani mwandishi anaweza kuandika mawazo yake kwa ufupi au kwa urefu kwa watu wengine.

**MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UANDISHI WA INSHA**

1. Kuweka vidokezo vya msingi vinavyohusiana na habari uliyopewa.
2. Kugawanya insha katika aya mbalimbali.
3. Kuwa na mpangilio mzuri wa matumizi ya maneno.
4. Kutumia lugha inayoeleweka.
5. Mpangilio mzuri wa mawazo wenye kuzingatia mantiki.
6. Kutokutumia lugha ya mkato
7. Kutumia msamiati wa kutosha.
8. Kuzingatia sarufi ya lugha
9. Kuzingatia matumizi ya alama mbalimbali za uandishi.
10. kuhakikisha insha inafuata na kujali matumizi ya nyakati mbalimbali.
11. Insha lazima iwe na sehemu kuu tatu:- Mwanzo

- Kiini

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Mwisho

12. Lazima kuwa na utangulizi mzuri unaovuta umakini.

13. Kuandika kiini cha insha kwa mpangilio unaofaa na kila wazo lipewe aya yake.

**AINA ZA INSHA**

Kuna aina nyingi za insha lakini zinaweza zikawekwa katika makundi makuu mawili,

(i) Insha za wasifu / kitawasifu

(ii) Insha za hoja

***NB:*** Baadhi ya wataalam huzigawa insha katika makundi makuu matatu.

(i) Insha za wasifu

(ii) Insha za kisanaa

(iii) Insha za hoja.

**Nini maana ya insha za wasifu:-**

Insha za wasifu ni insha ambazo huelezea sifa za kitu, hali au mtu fulani. Sifa zinaweza zikawa nzuri au Mbaya

**Insha za Hoja:-**

Hizi ni insha ambazo hutetea mawazo ya aina fulani na kupinga mengine kwa uthibitisho dhahiri.

**Insha za kisanaa;-**

Hizi ni insha ambazo hutumia vipengele mbalimbali vya kifasihi katika kuwasilisha ujumbe. Mbinu hizo ni kama vile nahau, methali, misemo, tamadhali za semi na mbinu nyingine za kisanaa.

***NB:*** Insha zisizo za kisanaa ni insha ambazo hazitumii lugha ya kifasihi katika kufikisha ujumbe wake.

**MUUNDO WA INSHA**

Insha kwa kawaida hugawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni:

1. Utangulizi / Mwanzo wa insha

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

2. Kiini cha insha / kati
3. Mwisho wa insha / hitimisho

1. **MWANZO WA INSHA**

Katika sehemu hii inapasa kuwa na maelezo mafupi yanayozingatia fasihi ya jambo linalozungumzwa, uhusiano wake na vitu vingine na muhtasari wa insha inayotungwa.

***NB:*** Kwa kawaida utangulizi huwa na aya moja

2. **KIINI CHA INSHA**

Hii ndiyo sehemu muhimu zaidi katika insha ambayo huzingatia mawazo makuu na kupangwa katika aya zenye mtiririko wa mantiki wa mawazo. Ufafanuzi wa mawazo makuu kuzingatia kichwa cha habari cha insha, mifano dhahiri kutumia kuonesha uhalisi wa jambo linalofafanuliwa.

3. **HITIMISHO**

Katika sehemu hii kunakuwa kuna msisitizo wa yale yaliyojadiliwa, msimamo, maoni au mapendekezo kuhusu jambo linalozungumzwa.

***NB:*** Mara nyingi hitimisho huwa ni muhtasari wa yaliyozungumzwa katika insha. Insha ni lazima ianze na kichwa cha habari na kuandikwa kwa herufi kubwa, juu katikati ya insha. Kichwa cha habari kiwe kifupi na kijitosheleze. Mara nyingi maneno yasizidi matano (5), ni vizuri kichwa cha habari kipigiwe mstari.

***NB:*** Ni vizuri insha ikazingatia idadi ya mawazo.

**UTUNGAJI WA BARUA**

***(i)kipengele cha uandishi wa Barua, mambo yafuatayo yazingatiwe***
. ***Afuate ufafanuzi wa kila aina ya Barua kwa kufuata mpanglio sahihi yani***

(i) Barua za kirafiki

(ii)Barua za kiofisi / kikazi

(iii) Barua za simu

(iv) Barua za mialiko.

(v) Barua za magazeti

(vi) Barua za kutoa taarifa.

* Mifano iongezwe katika ya kikazi na magazeti.
*katika Barua za mwalik0 mfano utolewe uonyeshwe.
*utungaji wa matangzo mfanoitolewe / uonyeshwe.

**1. Barua za Kiofisi:-**

Hizi ni barua rasmi ambazo huandikwa kwa madhumuni mbalimbali kama vile kuomba kazi, kutuma na kupokea taarifa rasmi, kuomba nafasi ya kusoma, kuomba likizo, kuomba uhamisho.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

(i) Anuani ya mwandishi ambayo hukaa juu upande wa kulia.

(ii) Tarehe inayokaa chini ya anuani ya mwandishi

(iii) Anuani moja au zaidi ya mwandishi inayokaa upande wa kushoto baada ya kumbukumbu namba

(iv) Salamu "Ndimi"

(v) Barua yenyewe ufafanuzi wa kusudio la barua

(vi) Mwisho wa barua

(vii) Sahihi ya mwandishi

(viii) Jina la mwandishi (kamili)

(ix) Cheo cha mwandishi.

**Mfano**:

**MTAA WA MTAKUJA,**

**S.L.P 14631,**

**MAJENGO – MOSHI.**

**13/11/2012.**

**MENEJA MKUU,**

**KIWANDA CHA MATOFALI,**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**S.L.P 87,**

**MOSHI.**

Ndugu,

YAH: **OMBI LA KUJA KUJIFUNZA KUFYATUA MATOFALI**

Kichwa cha habari hapo juu chahusika . Sisi ni kikundi cha vijana kumi na tano (15) ambao tumeamua kujiarijiri wenyewe kwa kufanya kazi ya kufyatua matofali.

Tunaomba kutembelea kiwanda chako kwa lengo la kujifunza zaidi.

Ni matumaini yetu kwamba ombi letu litakubaliwa.

**Wako mtiifu,**

**………………….**

**Vai Selis Chalamila**

**(Katibu wa kikundi)**

**2. Barua za magazetini**

Hizi ni barua ambazo huandikwa na wasomaji mbalimbali wa magazeti na kupelekwa au kutumwa kwa mhariri wa gazeti husika.

**MADHUMUNI:-**

- Kupongeza kuhusu jambo fulani

- Kufichua maovu fulani

- Kutoa maoni / mapendekezo kuhusu jambo fulani

**MAMBO YA KUZINGATIA / MUUNDO**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. Kuwa na kichwa cha barua ambacho huandikwa mwanzoni kwa herufi kubwa au kwa wino mzito.
2. Mwanzo wa barua ambao huanza na “Ndugu Mhariri,” Lazima kuwe na salamu.
3. Barua yenyewe na huwa na ufafanuzi wa hoja kwa kutolewa katika sehemu hii.
4. Mwisho wa barua mara nyingi huwa na maoni, maombi au mapendekezo.
5. Jambo la mwisho ni jina la mwandishi, anwani, na tarehe. Hivi huandikwa chini ya barua upande wa kushoto.

***Mfano:***

**SHULE ZITUMIKE KUKUZA VIPAJI**

***Ndugu Mhariri***,

Miaka ya nyuma swala la kukuza michezo shuleni lilikuwa linapatiwa kipaumbele. Hii ilidhihirishwa na kila shule kuwa na viwanja kwa ajili ya michezo mbalimbali.

Kwa miaka ya karibuni mambo siyo hivyo tena kwenye baadhi ya shule, viwanja hivyo vimeongezwa majengo kiasi kwamba sasa kunabakia sehemu finyu kwa ajili ya kufanya michezo hiyo. Wanapolazimika kufanya hivyo hutakiwa kwenda eneo la mbali, jambo ambalo linakuwa sio rahisi kulitekeleza mara nyingi.

Hata hivyo, kwa ushauri wangu naona kuwa shuleni ambapo wanafunzi bado ni wadogo wana nafasi nzuri ya kuendeleza vipaji vyao vya michezo.

Hii inawezekana sio kwa kusoma darasani bali kwa kufanya mazoezi ya michezo husika.

Tunaomba waalimu na mamlaka husika waliweke hilo maanani ili vijana waweze kweli kukuza vipaji vyao vya michezo. Ni kwa njia hiyo pekee ndiyo tutaweza kupata wanamuziki bora, wanariadha makini, waigizaji hodari wacheza mpira wa kiwango kinachoastahili na mabondia wa kiwango cha kimataifa. Hapo tunaweza tukawapata wakina Filbert Bayi wapya, wakina Abdallah Kibasen wapya, akina Mbaraka Mwishekhe wapya nk.

Fausta John,

S.L.P 514,

**3. Barua za Mialiko**

Ni barua ambayo aghalabu huandikwa kumualika mtu katika jambo fulani mfano harambee, sherehe, mkutano, semina, dhifa, warsha, kongamano.

**MAMBO YA KUZINGATIA:-**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(i) Jina la mwandishi na anuani yake

(ii) Jina la mwandikiwa / mwalikwa

(iii) Lengo la mwalikaji kwa ufupi

(iv) Tarehe ya mwaliko

(v) Mahali pa mwaliko

(vi) Siku na wakati wa kukutana

(vii) Mahali pa kupeleka jibu

**MFANO:-**

Bwana na bibi John wanayofuraha kukualika bibi Vai kwenye shehere ya kumpongeza mtoto wao mpendwa Samweli kwa kumaliza darasa la saba, siku ya Jumapili tarehe 28/07/2013 kwenye ukumbi wa Uhuru Park Majengo saa kumi jioni.

Jibu kwa:

Emerco Mashelle

0713 – 208123

**NB:** Wakati mwingine barua za mialiko huandikwa kama barua za kindugu ila huwa na maneno machache ili zisipoteze lengo maalumu.

**MFANO:**

**Kijiji cha Kafule,**

**S.L.P 15,**

**Itumba – Mbey**a

18/07/2013

Kwako mpendwa Vai,

Salam, Tarehe 11/08/2013 ninaadhimisha sikukuu ya kuzaliwa kwangu, nakualika ufike tufurahi pamoja kwenye chakula kuanzia saa tano usiku nyumbani kwangu, Tafadhali naomba unijibu. Kufika kwako ndiyo furaha yangu

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Rafiki yako,

Halima

***NB:*** Kama barua ya mwaliko ni rasmi, yaani ya kiofisi, majina ya mwandikiwa huambatana na cheo chake. Mfano Profesa, Sheik, Mchungaji, Dakrati n.k ambayo hutumika sambamba na maneno ndugu, bwana, na bibi. Wakati mwingine barua za mwaliko huandikwa katika karatasi maalum na kuitwa kadi za mwaliko.

4. **Barua za simu**

Simu za maandishi ni njia mojawapo ya mawasiliano ya haraka miongoni mwa watu. Mtu anayeandika huipata haraka iwezekanayo kulingana na barua za kawaida. Barua za simu huwa ni fupi, lakini zenye ujumbe uliowazi na unaoeleweka. Ufupi wa barua za simu hutokana na gharama za malipo kwa sababu gharama za simu hulipiwa kulingana na idadi ya maneno yanayoandikwa.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

1. **Anuani ya anayepelekwa taarifa.** Hii ni kazima iwe kamili na wazi ili kuziwezesha barua hiyo imfikie mlengwa bila ya matatizo yoyote.
2. **Taarifa au ujumbe**. Hiki ndio kiini cha simu, ni vizuri kikaandikwa kwa ufupi na kueleweka, epuka kuandika mambo yasiyokuwa ya lazima.
3. **Jina la mwandishi**

***NB:*** (i) Ni vizuri kuandika kwa herufi kubwa kurahisisha usomaji.

(ii) Barua ya simu huandikwa katika karatasi maalumu

(iii) Hakuna barua ya simu ambayo husafirishwa bila kulipiwa.

***Mfano:*** ASHA MWANASEFU SLB 404060 MOSHI

FIKA HARAKA BABA ANAUMWA HAMISI

5. **Hotuba**

Hotuba ni maelezo ambayo hutolewa na mtu mbele ya halaiki ya watu (watu wengine) kwa madhumuni mbalimbali kama vile kubainisha watu kufanya kazi , kutoa taarifa fulani, kufanya kampeni fulani n.k

**SIFA ZA HOTUBA**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Hotuba yoyote nzuri ni lazima izingatie mambo yafuatayo:-**

(i) Ukweli wa habari na taarifa inayotolewa.

(ii) Ufasaha wa lugha ili kuifanya hotuba iweze kupendeza na kueleweka vizuri.

(iii) Nidhamu yaani kuwa na adabu njema unapohutubia na unapokuwa umesimama mbele ya watu.

(iv) Mantiki nzuri yaani mfuatano mzuri wa mawazo na fikra.

(v) Sauti ya kusikika wazi pamoja na ishara zinazoeleweka iwapo hotuba inatolewa mbele ya watu.

**AINA ZA HOTUBA**

**(i) Mahubiri**

Hizi ni hotuba zinazohusu mafundisho ya dini na hutolewa makanisani, misikitini, mbele ya waumini na pia kwa njia ya redio au televisheni.

**(ii) Hotuba za kisiasa na za kiserikali**

Hizi ni hotuba zinazohusu mambo ya kiserikali na vyama vya siasa kwa lengo la kufafanua maazio au sheria, kampeni za kisiasa, kuhimiza watu kutenda jambo fulani n.k.

**(iii) Mihadhara au masomo ya darasani:-**

Hizi ni hotuba au mafundisho yanayotolewa na waalimu shuleni hasa wanapokuwa wanafundisha kundi kubwa la wanafunzi hasa vyuo vikuu.

**(iv) Risala**

Hii ni hotuba au taarifa fupi ambayo husomwa mbele ya kiongozi kwa niaba ya kundi fulani la watu ili kutoa maelezo au kuonesha msimamo wa kundi hilo kwa kiongozi husika.

***NB:*** Baada ya kusomwa , kwa kawaida risala hiyo hukabidhiwa kwa mhusika katika maandishi kama kumbukumbu ya kudumu.

**MUUNDO WA HOTUBA**

**Kwa kawaida hotuba huwa na muundo ufuatao:-**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**(i) Mwanzo**

- Huwa na salamu ambazo hutegemea hadhara iliyopo na lengo la hotuba.

**(ii) Utangulizi:-**

- Huwa na utambulisho kulingana na vyeo vya hadhara iliyopo.

Mfano; Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa wabunge, Waheshimiwa madiwani, Waheshimiwa wakuu wa shule, Waheshimiwa Waalimu, mabibi na mabwana

***NB:*** Katika utambulisho kunaweza kuwa na shukrani pamoja na muhtasari wa hotuba itakayotolewa.

**(iii) Kiini cha hotuba / kati**

- Sehemu hii ndiyo hutoa ujumbe kwa wasikilizaji na ndiyo sehemu muhimu zaidi katika hotuba. Kutoka sehemu hii mhutubiaji hueleza na kutoa ufafanuzi wa yale yote yaliyomsukuma kutoa hotuba kwa hadhira husika.

**(iv) Mwisho**

- Huwa ni muhtasari wa yale yaliyoelezwa kwa lengo la ….

6. **Risala**

**Kamusi ya Kiswahili sanifu (*TUK: 1981)* Inafafanua risala kuwa:-**

(i) Taarifa inayopelekwa kwa mtu au watu fulani, aghalabu inayoeleza hoja inayotakiwa.

(ii) Hotuba fupi inayosomwa mbele ya kingozi kwa niaba ya kundi fulani la watu ili kutoa maelezo au kuonesha msimamo wa kundi hilo kwa kiongozi.

**MUUNDO WA RISALA**

**Risala huwa na sehemu kuu tatu:-**

(i) Mwanzo wa risala

(ii) Kati au kiini cha risala

(iii) Mwisho / hitimisho la risala

**MWANZO**

Huwa unahusisha utangulizi, salamu, ukaribisho na lengo risala.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**KATI / KIINI**

Hii ndiyo sehemu muhimu zaidi katika risala , ambapo masuala mbalimbali hufafanuliwa. Mfano: mafanikio, matatizo, changamoto mbalimbali, mapendekezo, maombi n.k

**MWISHO**

Huwa ni msisitizo wa yale yaliyofafanuliwa kwenye kiini cha risala, shukrani , pamoja na hitimisho.

**NB:** Kwa kuwa risala huandikwa basi sharti ianze na kichwa cha habari. Tena kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigiwe mstari.

7. **Matangazo**

**MAMBO YA KUZINGATIA**

(i) Kichwa cha habari (huandikwa kwa herufi kubwa)

(ii) Kutaja aina ya biashara au huduma zinazotakiwa na bei zake.

(iii) Kutaja aina za bidhaa au huduma zinazotolewa na bei zake.

(iv) Kutaja mahali inapotolewa huduma / bidhaa hizo yaani mji, mtaa, kijiji n.k

(v) Kutaja namna ya kuwasiliana

Mfano wa tangazo:-

**TANGAZO**

**Vitabu, Vitabu, Vitabu.**

**Wale wauzaji maarufu wa vitabu vya Injili/Dini wameleta Ingizo jipya. Fika dukani kwao Mtaa wa Malapa, Buguruni, Dsm.**

**Kwa mawasiliano zaidi;**
**Piga simu zifuatazo;**
**0765000724**
**0713000725**

**UANDISHI WA KAZI ZA FASIHI.**

Dhana ya utungaji:
Kutunga ni kitendo cha kutoa mawazo ubongoni kisha kuyadhihirisha kwa kuyaandika au kuyasimulia.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**Hatua za Mwanzo za kuzingatia katika kutunga kazi za kifasihi**.

i). Kuwa na jambo ambalo unaona linasababisha au lina mvuto kwa jamii.Kisha unafanyia utafiti kujua chanzo chake na kwa nini linaendelea kuwepo.

ii).Baada ya utafiti ni kufanya maamuzi ya njia gani au tanzu gani aitumie kufikisha ujumbe kati ya ushairi , hadithi, semi na maigizo.

iii).Atumie kipera gani kutoa kutoka katika tanzu aliyochagua .Mfano kama ni ushairi atumie nyimbo au ngonjera.

iv).Kulijenga jambo jambo katika fani na maudhui ili kupata mbinu sahihi ya uwasilishaji wa kazi yako kwa hadhira.

v). Mtunzi kujikita hasa katika maudhui ya jambo lako unalotaka kuliwasilisha .Mfano nini dhamira yako.

vi).Mtunzi unaangalia namna ya kuwasilisha maudhui yako, hapa unashughulikia vipengele vya fani yaani muundo , mtindo ,mandhari ,wahusika na matumizi ya lugha.

Hapa mtunzi anatakiwa atumie ufundi na ubunifu wa hali ya juu ili kazi yake ielimishe na kusisimua.

vii).Baada ya fani na maudhui kushughulilkiwa mtunzi aangalie namna ya uwasilishaji wake.Kuangalia kanuni na taratibu za kipera ulichotumia.

viii).Mtunzi unaanza kuandika yale unayotaka kuelimisha jamii kwa kufuata taratibu za uandishi.

ix). Mtunzi unasoma kuangalia kama kile ulichokidhamiria ndicho ulichikitunga.

x).Fanya mazoezi namna ya kuwaslisha hiyo kazi.

Mfano:-

Namna ya kutunga igizo la kifasihi simulizi

i.Kwanza kuteua wahusika watakao sawiri matendo ya tabia zao:-

-Mhusika mkuu hujitokeza mara kwa mara na matendo mengi yanamuhusu yeye.

-Wahusika wadogo huwa wengi.

- -Kuteua waigizaji wazuri watakaofanya vizuri katika kuiwasilisha.
  -Wahusika wajengwe kwa kuzingatia utendaji wao.
- ii.Kuteua lugha itakayotumika.
- iii.Kuteua mandhari nzuri katika uwasilishaji wake.
- iv.Kuangalia muundo na mtindo wa igizo lake.

---

# UTUMIZI WA LUGHA

Matumizi ya lugha ni namna yakutumia lugha kulingana na mila, desturi na taratibu zilizopo katika jamii husika. Ni jinsi ambavyo mzungumzaji anatunza lugha kwa kuzingatia uhusiano wake na yule anayezungumza naye. Matumizi ya lugha hutegemea mambo kadhaa Kama vile: Uhusiano baina ya wazungumzaji.

-Mada inayozungumzwa

-Mazingira waliyomo wazungumzaji n.k

**Umuhimu wa matumizi ya lugha**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

1. Kuwasaidia watumiaji wa lugha kutumia lugha kwa ufasaha
2. Kumsadia mzungumzaji kuweza kutambua kutofautiana na kutumia mitindo mbalimbali ya lugha

## MTINDO WA LUGHA

Mtindo wa lugha ni mabadiliko yanayojitokeza katika kutumia lugha mabadiliko ya lugha katika mitindo mbalimbali yaani mitindo mbalimbali ya lugha. Kwa kawaida mtindo wa lugha / mabadiliko katika kutumia lugha ndiyo inayomwongoza mzungumzaji katika kuelewa maneno na mitindo ya tungo,

**Matumizi katika lugha hutawaliwa na mambo yafuatayo.**

- Uhusiano baina ya wazungumzaji
- Mada ya mazungumzo
- Lengo au madhumuni ya mazungumzo
- Sifa za wazungumzaji
- Jinsi mazungumzo yanavyofanywa
- Utanzu wa mawasiliano

### A.Mazingira /muktadha

Ni wazi kwamba wazungumzaji huzungumza wakiwa katika mazingira Fulani yanayotawala katika maisha yao ya kila siku. Mazingira hayo yanaweza yakawa ya hotelini shuleni, ofisini, mahakamani na n.k

### B.Uhusiano baina ya wahusika

Uhusiano baina ya wahusika huathiri mtindo wa uzungumzaji katika lugha. Mzungumzaji atatumia lugha kwa kutegemea anaongea na nani na kutokana na sababu hiyo tunapata lugha ya baba na mtoto, watu wa rika moja, mtu na mpenzi wake, mtu na mwanafunzi wake mfanyakazi wa kawaida na mkuu wake wa kazi na n.k.

### C.Mada ya mazungumzo

Kimsingi mada ya mazungumzo hutawala usemaji na namna ya uzungumzaji kwa ujumla na kutokana na mada ya mazungumzo tunapata lugha ya kibiashara, kitaalamu, kitabibu, kitaaluma na kisiasa na n.k

### D.Madhumuni ya mazungumzo

Wakati mwingine mitindo wa lugha hutawaliwa na madhumuni ya mazungumzo na kutokana na madhumuni ya mazungumzo uzungumzaji utategemea mazingira, uhusiano baina ya wahusika pamoja na mada ya mazungumzo.

### E. Jinsi mazungumzo/mawasiliano yanavyozungumzwa

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Namna mawasiliano yanavyofanyiwa inaweza kuathiri mtindo wa uzungumzaji. Mawasiliano yanawezakufanywa kwa njia ya maandishi au mazungumzo ya mdomo yanaweza kufanyiwa kwa njia ya simu au televisheni au redio. Njia hizi huathiri mtindo wa uzungumzaji.

**F. Utanzu wa mawasiliano**

Mtindo wa uzungumzaji unaweza kuathiriwa pia na utanzu wa mawasiliano yaani kama ni hotuba, majadiliano masimulizi, mazungumzo ya kawaida au maelezo, vitathiri mtindo wa uzungumzaji

1. **Sifa ya mzungumzaji**

Wakati mwingine mtindo wa lugha huathiriwa na sifa za wazungumzaji, Sifa hizo zaweza kuwa; kiwango cha elimu, cheo, uwezo wa kipato, heshima ya mtu katika jamii na n.k

**I. Rejesta**

Ni mtindo wa lugha ambayo hutumika mahali penye shughuli fulani, mf: bandarini, shuleni, hospitali, hotelini, kanisani nk.

**AINA ZA REJESTA**

Kuna aina mbalimbali za rejesta kulingana na mahali au shughuli inapofanyika.
i. Rejesta za hotelini:- huu ni mtindo utumikao hotelini mf:- Nani wali kuku? Chai moja chapati moja
ii.Rejesta za mitaani:- ni mazungumzo yatumiwayo na aina fulani ya watu katika magenge, vijiweni na hueleweka na watu au wahusika wenyewe. Mf: mshikaji- rafiki, Demu-msichana, umenoa- umekosa, dili maiti -mpango usiofanikiwa.
iii.Rejesta za hospitalini:- ni lugha itumiwayo na manesi, madaktari na wagonjwa hospitali. Lengo lake ni kupunguza muda kuwashughulikia wateja wengi. mf: kutwa mara tatu yaani kunywa kimoja asubuhi, mchana na jioni.
iv.Rejesta kanisani:- ni lugha ya mahubiri. Sifa yake kubwa haibadiliki badiliki. mf: Mapendo - daima, Bwana yesu asifiwe - Amina.
Msikitini, mf: Asalam aleikum - Aleikum asalaam
v.Rejesta mahakamani:- mtindo huu hutumika mahakamani. Mf: Mheshimiwa hakimu, Mtuhumiwa, kesi nk.

**DHIMA ZA REJESTA**

i. Hutumika kama kitambulisho kwa wazungumzaji, mtu huweza kutambua shughuli baada ya kusikia lugha itumikayo, mtindo wa sokoni ni tofauti na mahakamani hivyo hutambulisha wazungumzaji.
ii. Hutumika kurahisisha mawasiliano kwa kupunguza muda wa kuhudumia, mf: Hotelini kama wateja wengi, Nani wali samaki?, Chai wapi?
iii. Hukuza lugha, msamiati wa lugha huongezeka kupitia rejesta mf: dawa mpya - ikimaanisha dawa za kupunguza makali ya ukimwi.
iv. Huficha jambo kwa wasiohusika, mf: daktari amuandikiapo majibu mgonjwa sio rahisi mtu asiye katika kada hiyo kuelewa.
Mf: BS - kupima malaria

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Stool - kupima choo
Inj - Sindano
5/7 - kunywa dawa kwa siku 5 katika wiki
v. Hupamba lugha, mikato ya maneno katika rejesta, inapamba lugha. mf: wali kuku, wapi mkia
vi. Hutumika kupunguza ukali wa maneno mf: kujifungua - kuzaa

**II. MISIMU (SIMU)**

Misimu ni maneno yanayounda na kutumiwa na watu kwa muda fulani na baadaye kupotea. Misimu ni maneno yasiyokuwa sanifu yanayozushwa na kikundi cha watu wachache wenye utamaduni mmoja ili kuelezea mahusiano yao kama kikundi na hatimaye maneno yale hutumiwa na watu kwa muda fulani yale yanayodumu husanifiwa na kuwa sehemu ya msamiati rasmi katika luha husika.

Misimu husuka na kutoweka ingawa baadhi ya misimu inaweza ikatumika kwa muda mrefu na kusanifiwa kuwa lugha rasmi.

Misimu hutumiwa na makundi maalum katika jamii, yaliyojitenga kufuatana na mambo yanayoendelea, mazoezi, kazi au shughuli.

**CHANZO CHA MISIMU**

1. Misimu huzuka kutokana na mabadiliko na matukio mbalimbali yanayojitoleza katika jamii kama vile hali ngumu ya maisha, mabadiliko ya tabia za watu.

2. Baadhi ya misimu huzuka kutokana na hali ya utani miongoni mwa watu mbalimbali kwa lengo la kukebehi, kubeza, kudharau, kudhihaki, kukejeli au kusifia kusiko kuwa kwa kawaida.

**SABABU ZA KUTUMIA MISIMU**

1. Kutaka kuyafanya mazungumzo yawe ya siri. Kuna baadhi ya watu wanapozungumza ili kuyafanya mazungumzo yao yasieleweke kwa watu wengine hutunza misimu ili kuyafanya mazungumzo yao yawe ya siri.

2. Baadhi huitimiza kwa kudhani matumizi ya misimu ndiyo ujuzi wa lugha. Hali hii hujitokeza hasa kwa vijana ambao hupenda kutumia misimu kama sifa mojawapo ya kuonesha ujana wao. Ni vigumu kuwasikia wazee wa makamo tena wenye heshima zao wakitumia misimu.
3. Kufanya mambo mazito na ya maana yaonekane mepesi na ya kawaida.

**AINA ZA MISIMU**

**Misimu inaweza ikagawanywa katika makundi mbalimbali kwa kutumia vigezo tofauti:-**

**(a) MADA**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(i) Misimu inayohusiana na pesa. Upungufu wa pesa madeni, rushwa, utajiri na mambo yanayowakumba watu katika jamii. Ili kuelezea hali hizo watu wamezusha misimu kama vile kuchacha, kupigika, kufulia, pedeshee, kumkamua mtu, kuchuna.

(ii)Misimu inayohusika na vyakula. Kwa kawaida misimu hii husifu chakula kilicho kizuri na kitamu, cha watoto – wali, wali mchafu, -pilau, kodrai ukoko, zege – chipsi mayai , kiepe – chipsi.

iii Misimu ya ulevini. Hii hutumika katika mazingira ya ulevi ili kuyafanya mazingira hayo yawe ya msisimko na yenye starehe kwa walevi.

***Mfano:*** Leta kama tulivyo

-Moja baridi, moja moto

-Leta kisichana

-Kupiga mtindi

(iii) Misimu ya nguo. Uvaaji wa nguo na mitindo mbalimbali ya nguo imezalisha misimu kama vile:-

***Mfano:*** pedo

Kitopu

Mnyonyo

Kibamba

Tentemeke

Wanchoma kumoyo

Mayenu

Kutupia

(iv) ***Usafiri:* -** Hii hutumika mahali penye shughuli za usafiri.

***Mfano:*** daladala

Vipanya

Bodaboda

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Pipa – ndege

Gogo

(b) **MAKUNDI YA WATU-**

Kwa kutumia kigezo hiki misimu kinaweza kugawanywa katika makundi yafuatayo:-

(i) Misimu ya wanafunzi

(ii) Misimu ya wafanyabiashara

(iii) Misimu ya majangili

(iv) Misimu ya majambazi

(v) Misimu ya wanamichezo

(vi) Misimu ya mafundi

(vii) Misimu ya wanawake.

(c) **Kwa kutumia kigezo cha kawaida kuna misimu hii.**

(i) **Misimu ya pekee**, ambayo huelezea mahusiano ya kikundi kimoja kutoka katika utamaduni mmoja. Misimu hii hupatikana sehemu moja ya kazi au mahali waishipo watu wa aina moja. Misimu hii kimatumizi eneo lake huwa ni dogo na inaitwa misimu ya pekee kwa sababu haijulikani zaidi nje ya eneo ilimozuka na kutumika.

(ii) **Misimu ya kitarafa** ambayo eneo lake kimatumizi ni kubwa kidogo kulingana na lile la misimu ya kipekee

Misimu hii inaweza ikapatikana katika kata, tarafa, wilaya , mkoa. Watu waliopo katika kundi hili wanamchanganyiko wa utamaduni na si rahisi kutambua mipaka ya maeneo haya ya kitarafa ingawa kimsingi yanaweza kuwa ya kijografia kilugha. Kuenea kwa misimu hii kunategemea hali au tabia ya kuingiliana kwa watu katika shughuli zao za kila siku kama vile kuoana n.k. Mara nyingi hutokana na vitu vilivyo katika sehemu husika, lugha itumikayo uzoefu wa mazingira na uwezo wa lugha wa wahusika (umahiri)

(iii) **Misimu zagao**

Hii ni misimu ambayo imeenea nchi nzima na wakati mwingine kuvuka mipaka ya nchi, Hutumika katika radio, televisheni, magazeti lakini pia hutumika katika baadhi ya vitabu. Inapotumika kwa muda mrefu huweza kusanifiwa na kuwa msamiati rasmi.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

***Mfano:*** buzi, changudoa, wafurukutwa, kuchakachua , ngangari , mafataki, Serengeti boy, nyumba ndogo, kuchuna, daladala, shangingi, dingi, mshua, mahanjumati, mkorogo.

## MATUMIZI YA MISIMU

1. Misimu hutumika kama kiungo cha ukuzaji wa lugha. Baadhi ya misimu hasa ile inayodumu kwa muda mrefu huweza kusanifiwa na kuwa sehemu ya lugha rasmi. Mfano: marupurupu, chungu mbovu, magendo, daladala, mitumba, changudoa.
2. Kupamba lugha hasa katika maongezi na katika maandishi hasa katika fasihi. Matumizi ya misimu katika kuipamba lugha huifanya lugha isisimke na kufurahisha.
3. Kufanya mawasiliano yawe mafupi na yanayoelezwa kwa haraka. Misimu

inawezesha watu kuwasiliana kwa kutumia maneno machache na muda mchache. Mfano: daladala

4. Kuficha lugha ya matusi. Baadhi ya misimu hutumika kupunguza ukali wa maneno katika mazungumzo ya kawaida. Mfano: mada inayohusiana na mapenzi misimu hutumika sana ili kupunguza ukali wa maneno hayo. Kula – uroda.
5. Kuunganisha watu wa makundi mbalimbali. Mfano:- makundi ya maprofesa, wanasheria, wasomi, madaktari wanapotumia misimu huwekwa katika kundi moja.
6. Kuhifadhi historia ya jamii. Kwa kuwa misimu huzuka na kutoweka kutokana na mabadiliko yanayojitokeza katika jamii, mara nyingi misimu hiyo hutumika kuonesha historia ya jamii husika.

***Mfano:*** bwanyenye wapambe

| | |
|---|---|
| Ukupe | wazawa |
| Ubeberu | ngangari |
| Utaifishaji | ngunguri |
| Ukereketwa | |
| Mfurukuwa | |

7. Kuibua hisia mbalimbali:- Misimu huwa na maneno yenye kubeba hisia za chuki, furaha, huzuni, kejeli n.k
8. Misimu inafurahisha na kuchekesha. Kwa kuwa hazina chumvi nyingi na hivyo kufurahisha na kuchekesha.
9. Kukosoa na kuiasa jamii kwa kuwa hubeba hisia za kebehi, dhihaka,, chuki, kejeli, mabezo, dharau na kusifu kusikokuwa kwa kawaida.

## MATATIZO YA MISIMU

1. Misimu siyo lugha sanifu kwa hiyo kwa namna moja au nyingine huchangia kuharibu lugha.
2. Misimu hupunguza hadhira ya watumiaji wa lugha fulani.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

3. Misimu huzuka na kutoweka, Misimu iliyozuka na kutoweka ni mingi zaidi ukilinganisha na ile iliyodumu na kuingizwa katika msamiati rasmi hivyo mchango wake katika kukuza ni mdogo.
4. Misimu ina maana nyingi, Maana hizi huweza kuwepo,
5. Misimu huwa na chuku nyingi. Hali hii husababisha misimu kutokuaminika katika jamii na hivyo kusababisha mawasiliano kutenguka.
6. Misimu ni lugha ya mafumbo.Kutokana na hali hii misimu hufahamika na watu wanaoitumia na hivyo kusababisha mawasiliano kuwa kidogo.

***NB:*** Nafasi ya misimu katika kuikuza lugha ya Kiswahili na kubwa kwa sababu matumizi ya misimu yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku na imekuwa ikitumika katika mazungumzo ya kawaida na hata katika maandishi. Kwa kiasi kikubwa kuenea kwa misimu kumesababishwa na vyombo vya habari kama vile magazeti, televisheni. Kwa upande wa magazeti misimu imeenezwa sana na magazeti ya udaku. Pia vipindi mbalimbali katika televisheni na redio vimekuwa vikichangia kuenea kwa kasi kwa misimu hii, matokeo yake ni kwamba baadhi ya misimu imepata nguvu na kushamiri na mengine imevuka mipaka ya nchi. Hali hii imechangiwa na matumizi ya mara kwa mara ya misimu hiyo katika kutolea habari. Kutokana na hali hii hata kamusi za Kiswahili zilizotengenezwa hivi karibuni zimejumuisha baadhi ya misimu kama misamiati inayomchango katika kuikwea lugha ya Kiswahili.

***Swali:-*** Lugha izungumzwapo mitaani na vijana huchukiwa sana na wazazi lakini wasanifu wa lugha wanaipenda sana lugha hiyo. Toa sababu za mkungazo wa mawazo kati ya wazazi na wasanifu wa lugha.

## III. UMAHIRI WA LUGHA

Umahiri katika lugha ni ujuzi wa kiwango cha juu katika lugha fulani ambao hukita katika stadi nne za lugha yaani kusoma, kuzungumza, kuandika na kusikia.

**Umahiri unaweza kugawanyika katika makundi makuu mawili**

(i) Umahiri katika lugha

(ii) Umahiri wa lugha

1. **UMAHIRI KATIKA LUGHA**

Umahiri katika lugha ni ujuzi wa kiwango cha juu katika lugha fulani kwa viwango vyote vya lugha yaani kuzungumza, kusikia, kusoma na kuandika.

Aidha umahiri katika lugha huhusiana na ujuzi wa hali ya juu katika lugha moja tu.

Mfano, Kiswahili peke yake, kiingereza peke yake au lugha za kilugha peke yake

II **UMAHIRI WA LUGHA**

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Umahiri wa lugha ni ujuzi wa hali ya juu wa lugha zaidi ya moja katika staidi zake zote yaani kuzungumza, kusikia, kusoma na kuandika. Umahiri wa lugha unahusu ujuzi wa lugha zaidi ya moja. Mfano, Kiswahili na lugha za kikabila, Kiswahili na kiingereza. Mtu mwenye ujuzi wa umahiri huitwa mmahiri, katika nchi yetu kundi kubwa la watu ni wamahiri, wanafahamu lugha zao za kikabila, na Kiswahili na hata lugha za kigeni.

## SABABU ZINAZOSABABISHA UMAHIRI

### Umahiri kusababishwa na mambo kadhaa:-

1. **Elimu**

Mtu anaweza akawa mahiri wa lugha katika kusomea lugha husika au kuitunza lugha husika anapokuwa anasoma. Elimu humwezesha mtu kupata ujuzi wa msamiati, matamshi yake, sarufi, maana na mbinu nyingine za lugha hiyo. Mambo haya humwezesha mtu kuwa mahiri katika lugha au mahiri wa lugha.

2. **Matumizi ya lugha ya kila siku:-**

Matumizi ya kila siku humwezesha mtu kuwa mahiri na hii hutegemea lini wakati gani, mara ngapi, na kwa kiwango gani mtu huitimiza lugha hiyo katika shughuli zake za kila siku kama vile mawasiliano, sherehe n.k

3. **Hamahama ya watu** kutokana na sababu mbalimbali kama vile vita, ajira, biashara dini n.k

4. **Mabadiliko katika sera ya lugha:-**

Maamuzi yanayofanywa na serikali katika matumizi ya lugha yanaweza kusababisha mtu kuwa mmahiri wa lugha. Mfano: kama serikali itaamua kufuta katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kuhimiza matumizi ya lugha za kigeni kama vile kiingereza na kifaransa ni wazi kuwa watu watalazimika kujifunza lugha hizo na hivyo kuwa wamahiri wa lugha hizo.

## ATHARI ZA UMAHIRI

Watu wengi katika nchi yetu ni wamahiri wa lugha kwamba wengi wanazungumza lugha zao mama pamoja na za kigeni kama vile kiarabu, kihindi, kifaranza n.k

Kutokana na kuzungumza lugha zaidi ya moja huwa kunakuwa na mwingiliano wa lugha hizo unajitolea katika matamshi, msamiati, miundo na maana.

## I. MATAMSHI:-

Kwa kawaida matamshi ndiyo humbainisha mzungumzaji kuwa lugha yake ya kwanza ni ipi. Watanzania wengi waliozaliwa vijijini huanza kujifunza lugha za kikabila kabla ya Kiswahili na wale waliozaliwa mjini hujifunza lugha ya Kiswahili na baadaye lugha nyingine za kigeni au za kikabila.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mambo haya hupelekea athari ya lugha ya kwanza kujitokeza unapozungumza lugha ya pili. Kwa mfano Wakurya wanapozungumza hushindwa kutofautisha herufi ya 'r' na 'l. Wanyakyusa huchanganya kati ya herufi 'f' na 'v'. Wamakonde kuchanganya 'n' na 'm'. Kuongeza vitamkwa baadhi ya wazungumzaji ambao wazungumzapo Kiswahili huongeza vitamkwa kutokana na kuathiriwa na lugha zao mama. Mfano; Nakwendaga, hakunaga – hutumiwa sana na wasukuma, Bukubwa badala mkubwa, Ndada badala ya dada

**II. MSAMIATI**

Baadhi ya wazungumzaji wanapozungumza huchanganya misamiati, Mfano msamiati wa kiingereza na Kiswahili au Kiswahili na lugha za kikabila.

**III. MIUNDO**

Wakati mwingine muundo wa lugha ya kwanza hujitokeza mtu anapozungumza lugha ya pili. ***Mfano:*** Mama Kaondoka mjini. Wanyamwezi wamakua, wamatengo unapozungumza na mtu unayemweshimu sana unatumia wingi badala ya umoja.

**IV. MAANA**

Mara nyingi mahiri wa lugha huonesha athari katika maana anapokuwa anazungumza.

Mfano: Kuna baadhi ya watu wanapozungumza, maana za maneno za lugha fulani wanazozumgumza hujitokeza katika lugha nyingine.

- Wangoni hutumia neno kuchacha wakimaanisha kuwa kichachu, kichungu, kikali na ukakasi. Ni wazi kuwa wangoni wananeno moja tu katika lugha yao ambalo kubeba maana hizi zote.

- Wanyamwezi wanapozungumza Kiswahili hawawezi kutofautisha neno jana na kesho kutwa kutokana na sababu kuwa katika lugha yao wana neno moja tu ambalo huwa na maana zote mbili za neno hilo ni 'igolo'

**LUGHA YA MAZUNGUMZO NA LUGHA YA MAANDISHI:-**

Kwa ujumla lugha huwa ni moja yaani lugha ya mazungumzo tu. Lakini kutokana na namna lugha inayowasilishwa inaweza kugawanywa katika makundi makuu mawili:-

(i) Lugha inayowasilishwa kwa njia ya maandishi ya mdomo / lugha ya mazungumzo.

(ii) Lugha inayowasilishwa kwa njia ya maandishi (lugha ya maandishi).

**LUGHA YA MAZUNGUMZO:-**

Hii ni lugha inayowasilishwa kwa njia ya mazungumzo ya mdomo. Chanzo chake ni kuzungumza mawasiliano kati ya chanzo / mzungumzaji na kikomo /msikilizaji ni lazima wawe na sifa mahususi.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

## SIFA ZA MZUNGUMZAJI

1. Inatakiwa azingatie ufasaha na usanifu wa lugha.
2. Azingatie mpango mzuri wa mawazo.
3. Awe muwazi na mkweli katika maelezo yake.
4. Asiwe na hitilafu katika viungo vinavyotumika kuzungumza na kusikiliza.

## SIFA ZA MSIKILIZAJI:-

1. Anatakiwa awe mtulivu na msikivu. Pia inategemea viungo vya mwili.
2. Aweze kufahamu yanayozungumzwa.
3. Aweze kutafsiri yanayozungumzwa.
4. Aweze kupima yale aliyoyasikia na uzoefu wake wa siku zote.

## LUGHA YA MAANDISHI

Hii ni lugha inayomwezesha mtu kujieleza kwa njia ya maandishi. Chanzo chake ni kuandika na kikomo chake ni kusoma. Ili mawasiliano yaweze kuwepo kati ya mwandishi na msomaji ni lazima kanuni za uandishi zizingatiwe na mwandishi na msomaji afahamu kusoma.

## TOFAUTI KATI YA LUGHA YA MAZUNGUMZO NA

## LUGHA YA MAANDISHI

**Lugha ya mazungumzo na ya maandishi zinatofauti kadhaa:-**

### 1. UWASILISHAJI

Lugha ya mazungumzo huwasilishwa kwa mazungumzo ya mdomo, kwa sauti. Lakini lugha ya maandishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi au kwa njia ya kuandika.

### 2. CHANZO NA KIKOMO:-

Chanzo cha lugha ya mazungumzo ni kuzungumza yaani mzungumzaji na kikomo chake ni kusikiliza yaani msikilizaji. Lakini chanzo cha lugha ya maandishi ni kuandika yaani mwandishi na kikomo chake ni kusoma .

### 3. UHUSIANO NA HADHIRA

Lugha ya mazungumzo huwakutanisha ana kwa ana mzungumzaji na msikilizaji. Lakini lugha ya maandishi mara nyingi haiwakutanishi ana kwa ana mwandishi na msomaji.

### 4. MABADILIKO

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Lugha ya mazungumzo hubadilika badilika kutokana na mazingira, mahusiano baina ya watu wanaozungumza, pamoja na wakati na hapo tunaweza kupata rejesta mbalimbali. Lakini lugha ya maandishi ikishaandikwa haibadiliki kutokana na mazingira, wahusika wala wakati.

5. **UHAI**

Lugha ya mazungumzo huwa ni hai zaidi kuliko lugha ya maandishi kwa sababu huonesha hali ya mzungumzaji kama vile furaha, huzuni, chuki au hasira . Lakini lugha ya maandishi haioneshi wazi hisia.

6. Lugha ya mazungumzo humweka mtu huru zaidi na hapo tunaweza tukapata

umahiri wa lugha ya mzungumzaji kama vile matumizi ya misimu, semi, athari za lugha yake ya kwanza, kiimbo n.k. Lakini lugha ya maandishi huzingatia zaidi usanifu wa lugha.

7. **GHARAMA**

Lugha ya mazungumzo haina gharama kubwa kwa sababu hutumia viungo vya mwili. Lakini lugha ya maandishi inagharama kubwa katika muda wa kuandika na vifaa vingine kama kalamu, karatasi n.k

**8. UHIFADHI**

Lugha ya mazungumzo ni vigumu kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye ikiwa vile vile kama ilizungumzwa lakini lugha ya maandishi ni rahisi kuhifadhiwa na hudumu kwa muda mrefu kwa matumizi ya baadaye.

**9.** Lugha ya mazungumzo huonesha shada, kiimbo, na lafudhi si rahisi kubaini mambo yao.

**10. WAHUSIKA**

Lugha ya mazungumzo inawahusika wengi kuanzia watoto hadi watu wazima, vichaa na wenye akili timamu. Lakini lugha ya maandishi wahusika wake ni wachache, yaani wanaojua kusoma na kuandika tu.

## KUFANANA KWA LUGHA YA MAZUNGUMZO NA LUGHA YA MAANDISHI

1. Lugha zote hizi mbili humuhusu mwanadamu.
2. Lugha zote mbili hutumiwa na mwanadamu kwa lengo la kukidhi haja ya mawasiliano.
3. Lugha zote mbili huwa na chanzo na kikomo.
4. Lugha zote hutumiwa kama alama ya utambulisho wa jamii fulani.
5. Zote huwa zinahitaji maandishi ingawa mwandalizi ya lugha ya mazungumzo huwa ni kidogo sana.

## MAKOSA YA KISARUFI NA MAKOSA YA KIMANTIKI KATIKA

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

**LUGHA YA KISARUFI**

Haya ni makosa yanayotokana na kukiukwa kwa taratibu za kisarufi yaani matamshi ya maneno, miundo ya tungo, miundo ya maneno na maana za maneno. Mara nyingi makosa haya hutokana na utumiaji mbaya wa lugha miongoni mwa wazungumzaji. Kwa ujumla makosa ya kisarufi yanaweza kugawanyika katika makundi yafuatayo:-

***Makosa ya matamshi***:- Makosa hayo hujitokeza watu wanapozungumza kwa kushindwa kutamka baadhi ya sauti za Kiswahili au kuzichanganya na wakati mwingine ….

**Mfano:-** Kuna baadhi ya watu huchanganya 'r' na 'l.'

- Naenda kurara

Wengine wanatumia's' badala ya 'z', 'dh' na 'Hi'

- Sahabu badala ya dhahabu

- Samani sile badala ya zamani zile

- Sambi badala ya dhambi.

- Dhibiti badala ya thibiti

- Anapashwa badala ya paswa.

Kwa kawaida makosa haya hutokana na athari ya lugha ya kwanza.

- **Kuongeza vitamkwa:-**

Makosa haya hufanya na wazungumzaji wanapokuwa wanazungumza kwa kuongeza vitamkwa katika maneno ambayo huwa havihitajiki katika maneno hayo na hivyo kuiharibu lugha hiyo.

***Mfano:*** Tunakwendaga kwao mara kwa mara.

Hakunaga kitu kama hicho.

Yule mbaba jamani!

- **Kosa la kuacha maneno:-**

Wazungumzaji baadhi wanapozungumza Kiswahili huacha maneno fulani katika sentensi na bado wakifikiri wanatoa ujumbe ulio kamili.

***Mfano:*** - Mama ameondoka mjini

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

Mama ameenda mjini.

- Baba yako amerudi kazini?

Baba amerudi kutoka kazini?

- **Kosa la tafsiri sisisi:-**

Makosa yanatokana na tafsiri moja kwa moja na hivyo kusababisha makosa ya kisarufi katika lugha.

***Mfano:*** aidha …….au

Mama aidha atakuwa mjini au kazini.

Osha uso wako badala ya nawa uso wako.

- **Makosa ya kimuundo:-**

Makosa yanayojitokeza katika muundo, kwa kawaida miundo ya lugha ya Kiswahili huanza na nomino ya mtenda au mtendwa na kufuatwa na jambo analotendwa au analotenda yaani vitenzi.

***Mfano:*** Sikuwa ninajua kuwa Grace ni dada yako

Sikujua kuwa Grace ni dada yako.

**MAKOSA YA KIMANTIKI**

**Mantiki** ni utaratibu mzuri wa kufikiri. Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili sanifu toleo la pili (2004) inafasili mantiki kuwa ni mtiririko wa fikra zilizopangwa ili kujenga hoja yenye kukubalika. Kutokana na fasihi hizi makosa ya kimantiki ni yake yanayoonesha kukosekana kwa utaratibu mzuri wa fikra au makosa yanayotokana na upotofu wa mawazo ya mzungumzaji. Kwa maneno mengine ni makosayanayotokana na kukosekana kwa mtiririko mzuri wa fikra zilizopangwa ili kujenga hoja zenye kukubadilika.Kwa kawaida wazungumzaji na waandishi hufanya makosa ya kimantiki.

***Mfano:*** Nyumba yangu imeingia siafu

Nyumba haiwezi kuingia siafubali siafu huingia ndani ya nyumba

- Siafu wameingia ndani ya nyumba yangu.

- Gari yangu imeibiwa

- Gari ndiyo imetedwa

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- Gari yangu imeibwa

***NB:*** Makosa ya kisarufi nay a kimantiki ni ya kawaida ambayo yapo na yataendelea kuwepo katika lugha. Jambo la msingi ni kuendelea kujazwa kabisa yasitumike katika taasisi rasmi kama vile shule barua rasmi na madhara na mikutano ya kitaaluma n.k Ni vizuri katika kutekeleza azima hii ya kuzuia makosa ya kimantiki na kisarufi mkazo wa marekebisho …. Tangu kiwango cha awali,

Hii itasaidia kupunguza makkosa hayo kwa siku za baadaye. Kwa upande mwingine makosa haya husambazwa na vyombo vya habari na baadhi ya waalimu. Kwa hiyo ni vizuri walimu pamoja na vyombo vya habari kusisitiza matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili.

**UTATA KATIKA MATUMIZI YA LUGHA**

**Utata ni nini?**

Utata ni kitendo cha tungo kuwa na maana zaidi ya moja au kueleweka kwa namna mbili zaidi tofauti. Mara nyingi utata hujitokeza katika maana za maneno au maana za sentensi.

**SABABU ZINAZOSABABISHA UTATA**

1. Matumizi ya maneno yenye maana zaidi ya moja bila kuyapa muktadha wa kimatumizi.

***Mfano:*** Mama ana mbuzi

Neno mbuzi lina maana mbili na hivyo hufanya sentensi zieleweke kuwa na namna mbili tofauti.

2. Kutozingatiwa kwa taratibu za uandishi.

***Mfano:*** Nilimkuta Juma na rafiki yake George

-Mama John amekuja

3. Katika lugha ya mazunguzo utata unaweza ukasababishwa na kutokuweka mkazo wa sauti mahali panapostahili katika neno.

***Mfano:*** - Mbuzi

- Mbuni

- Mbuni

4. Utata unaweza ukasababishwa na matumizi ya mashina lugha ya picha au lugha ya mtaani au lugha iliyojificha.

***Mfano:*** Juma anaua chumbani mwake

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/
Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

- anatoa uhai
- Ana msichana mzuri chumbani mwake
- Ana maua chumbani mwake

**NAMNA YA KUONDOA UTATA**

1. Kuyapa maktadha wa kimatumizi maneno yenye maana zaidi ya moja.

***Mfano:*** Mama ana mbuzi wengi

Mama ana mbuzi ya kukuna nazi.

2. Kuweka mkazo wa sauti katika silabi stahiki katika neno.

***Mfano:*** Mbuni - Mbuni ni mzuri

Mbuni – Mbuni ni mzuri

3. Utata unaweza ukaondolewa kwa kuzingatia matumizi sahihi ya alama za uandishi.

***Mfano:*** Baba, John amefika

Baba John, amefika

4. Kuepuka matumizi ya lugha ya picha.

***Mfano:*** Juma anaua chumbani mwake

- Mzungumzaji aliyetumia sentensi hii akiwa anakusudia kuonesha kuwa Juma ana mchumba mzuri nyumbani kwake alipaswa kuepuka matumizi ya picha kwa kusema "Juma ana mchumba mzuri nyumbani kwake" Kwa kufanya hivyo angekuwa ameondoa utata uliokuwepo katika sentensi ya awali

***NB:*** Wakati mwingine utata unaweza ukasababishwa na matumizi ya kutanguliza nomino ya mtendwa badala ya kutangulia nomino ya mtenda.

***Mfano:*** Simba ameuawa na askari pori

- Sentensi hii ni tata kwa sababu ina maana zaidi ya moja.

(i) Simba na askari pori wote wameuawa.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/

Teacher.ac
FREE EDUCATION RESOURCES FOR AFRICA

(ii) Askari ndiye aliyemuua samba

Kama nomino ya mtenda ingetangulia kusingegkuwa na utata.

- Askari pori ameua simba.

Download this and more free notes and revision resources from https://teacher.ac/tanzania/